# MWINGILIANO MATINI WA MAUMBO YA FASIHI SIMULIZI YA KIAFRIKA NA MATINI TEULE ZA BIBLIA

**NA**

**YUNIA AGISO OTIENO**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**SHULE YA SANAA NA SAYANSI YA JAMII**

**CHUO KIKUU CHA MASENO**

**2017**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa ajili ya kutuzwa shahada katika chuo kikuu kinginecho. Hapana ruhusa ya kunakili sehemu yoyote bila idhini ya, ama mwandishi au Chuo Kikuu cha Maseno.

Yunia Agiso Otieno

Tarehe

PG/MA/00002/2013

Tasnifu hii imetolewa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Maseno.

Dkt. Deborah Amukowa

Tarehe
Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika
Chuo Kikuu cha Maseno.

Dkt. Beverlyne Asiko

Tarehe
Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika
Chuo Kikuu cha Maseno.

# SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru mkuu wa Idara ya Kiswahili, Prof. Florence Indede kwa kunielekeza vilivyo hasa nilipoanza utafiti huu. Msukumo wake ulinipa azma ya kujitahidi na kufanya kazi yangu kwa bidii zaidi. Shukrani zangu za dhati aidha ziwaendee wasimamizi wangu ambao ni Dkt. Deborah Amukowa na Dkt. Beverlyne Asiko kwa kuniongoza katika uandishi hadi ufanisi wa kazi hii. Walifanya kazi usiku na mchana na kunipa msukumo na motisha ya kumaliza tasnifu hii kwa wakati ufaao. Mungu na awabariki kwa moyo walio nao. Vilevile, nawashukuru wazamili wenzangu wa mwaka wa 2013, kwa kuwa marafiki wa karibu kila tulipohitajiana. Zaidi miongoni mwao ni bi. Christine Apopo ambaye pamoja tilitiana shime na motisha ya kutozembea kazi zetu. Nawashukuru wazazi wangu, Jorum Mbeka na marehemu mamangu mpendwa Phelesia Oginga aliyejitolea mhanga kuhakikisha kwamba nimepata kisomo changu hata ingawa hakuwa na fedha za kutosha. Shukrani zaidi ni kwa chuo kikuu cha Maseno kwa kunisaidia katika utafiti huu. Nisingefaulu katika utafiti wangu pasingekuwa na msukumo na kujitolea kwa wale wote waliohakikisha kwamba nimeifanya kazi yangu kwa wakati ufaao. Siwezi kumsahau mume wangu mpendwa Benson Otieno kwa kunihimiza na kuniliwaza wakati mgumu nilipokuwa masomoni na pia kunifadhili kifedha. Shukrani aidha ni kwa wanangu wapendwa Joy na Victorine pamoja na mpwa wangu Laura, hasa Joy kwa kunikumbusha kila wakati nisome kwa bidii ili watoto wangu wafurahie maishani. Siwezi nikamsahau dada Rachel Imoru kwa kusaidiana nami kuipiga chapa kazi hii. Shukrani kubwa zaidi ni kwa Mungu Mwenyezi aliyenijalia afya njema na uhai na kunipa neema ya kuendeleza kazi yangu. Jina lake na lihimidiwe.

# TABARUKU

Kwa mpendwa marehemu mamangu Phelesia Oginga aliyejitolea mhanga kuhakikisha kwamba nimepata elimu ingawa hakuishi kusherehekea matunda ya jasho lake. Mpendwa babangu Jorum Mbeka, mume wangu Benson Otieno, wanangu Joy Akinyi na Victorine Anyango pamoja na mpwa wangu Laura Ambiyo.

# IKISIRI

Biblia takatifu inayo misingi yake mikuu katika tamaduni za Wayahudi, yaani ni mkusanyiko wa vitabu vyenye maumbo ya fasihi simulizi. Ingawa kumekuwa na tafiti anuai kuhusu maumbo ya fasihi simulizi, chache zimefanywa kuhusu mwingiliano matini wa maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia. Utafiti huu ulidhamiria kutathmini maumbo ya fasihi simulizi katika vitabu teule vya Biblia ili kuziba hili pengo. Utafiti huu ulilenga kuhakiki mwingiliano matini kati ya fasihi simulizi na Biblia. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa: kuchanganua maumbo ya fasihi simulizi katika matini teule katika Biblia; kupambanua mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule ya Biblia; kutathmini mchango wa Biblia katika ukuzaji wa fasihi simulizi. Upeo wa utafiti huu ni maumbo ya fasihi simulizi katika vitabu saba vya Biblia ya Tafsiri Jipya la Kimataifa; kitabu cha Mwanzo, Wafalme wa kwanza na Wafalme wa pili, Zaburi, Mithali, Mathayo na Luka. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya mwingiliano matini iliyoasisiwa na Julia Kristeva mwaka wa 1969. Mihimili mitatu ya nadharia hii ni; kazi za kifasihi huingiliana na kuhusiana; matini hupeana umatini ambamo matini nyingine zinaweza kuundwa na kufasiriwa; fasihi hutokana na fasihi. Muundo wa kimaelezo ulizingatiwa. Ili kupata sampuli yenye sifa zifaazo, usampulishaji dhamirifu ulitumiwa. Data ilikusanywa maktabani kwa kusoma na kudondoa maumbo ya fasihi simulizi yaliyoafiki madhumuni ya utafiti kwa kutumia orodha ya uchunzaji. Uchanganuzi wa yaliyomo ulifanywa. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo nayo matokeo yakafasiriwa kuzingatia swala la utafiti, mihimili ya nadharia na madhumuni ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa ifuatavyo; kwanza, maumbo manne makuu ya fasihi simulizi yalidhihirika katika vitabu vilivyoteuliwa; pili, ilibainika kwamba fasihi simulizi huingiliana na matini teule ya Biblia; tatu, Biblia ina mchango mkubwa katika fasihi simulizi hivyo husaidia katika ukuzaji na uhifadhi wake. Utafiti ulihitimisha kuwa kuna mwingiliano matini kati ya fasihi simulizi na matini teule za Biblia. Mwingiliano huu ulidhihirika kutokana na jinsi maumbo ya fasihi simulizi yalivyoingiliana na matini teule za Biblia. Utafiti unatarajiwa kupanua uwanja wa fasihi simulizi kwa kukuza swala la mwingiliano matini. Utafiti unapendekeza kuwa Biblia itumiwe kama rejea ya maumbo ya fasihi simulizi. Hii itachochea wasomi wa fasihi simulizi na watafiti wa baadaye kusoma Biblia kama kitabu cha fasihi simulizi, hasa wanapochanganua maumbo ya fasihi simulizi.

**ABSTRACT**

The Holy Bible has its major pillars in the traditions of the Jews, thus, it is a collection of books that have genres of oral literature. Though a lot of research has been done on the genres of oral literature, very little has been done on the intertextuality of the genres of oral literature in the Bible. This study intended to evaluate the genres of oral literature in selected books of the Bible so as to fill this gap. The research aimed at analyzing the interxtuality nature of oral literature and the Bible. The objectives of this research were to: analyse the genres of oral literature found in the Bible; establish the intertextuality nature of oral literature genres in selected texts of the Bible; evaluate the contribution of the Bible in the growth of oral literature. The scopes of the research were the forms of oral literature in the New International Bible version. This research was guided by the theory of intertextuality which was coined by Julia Kristeva in 1969. The three tenets of this theory are; literary works intermingle and relate with each other; all literary work is re-written; any text is the absorption and transformation of another. The research design was descriptive. The study areas were the sixty six books of the Bible. To get the right sample, purposive sampling was done. Data collection was done in the library by reading and identifying the genres of oral literature in line with the objectives using the observation schedule. Textual analysis was done. Data was presentated descriptively. The results were interpreted according to the problem statement of research, tenets of the theory and objectives of the research. The results of this research were as follows; First, the four major genres of oral literature were identified; second, the intertextuality of oral literature genres in selected texts of the Bible were established; Third, the Bible contributes greatly to oral literature there by expanding its field. The study concluded that there is intertextuality between oral literature and the Bible. The intertextuality was established in the way the genres of oral literature were identified in the Bible. This research suggests that the Bible be used as a reference book for genres of oral literature. It is hoped to expand the field of oral literature and show the intertextuality nature of oral literature and other disciplines and so challenge literature scholars, analysts and researchers to read the Bible as a literature book, especially when analyzing the genres of oral literature.

## YALIYOMO

**MADA**


Ikirari ........................................ ii
Shukrani ........................................ iii
Tabaruku ........................................ iv
Ikisiri ........................................ v
Abstract ........................................ vi
Yaliyomo ........................................ vii
Orodha ya Vifungu vya Biblia ........................................ x
Dhana zilizotumika ........................................ xiv

**SURA YA KWANZA** ........................................ 1
**UTANGULIZI........................................ 1**
1.1Usuli wa utafiti ........................................ 1
1.2 Swala la utafiti ........................................ 5
1.3Maswali ya utafiti ........................................ 5
1.4 Madhumuni ya utafit ........................................ 6
1.5 Misingi ya uteuzi ........................................ 6
1.6 Upeo wa utafiti ........................................ 8
1.7 Misingi ya Nadharia ........................................ 8

**SURA YA PILI…………………………………. 14**
**MAPITIO YA MAANDISHI………………………….. 14**
2.1 Utangulizi ........................................ 14
2.2 Dhana ya fasihi simulizi ........................................ 14
2.3 Fasihi simulizi na matini teule za Biblia ........................................ 16
2.4 Mchango wa Biblia katika fasihi simulizi ........................................ 18
2.5 Mapitio kuhusu Nadharia ........................................ 20

**SURA YA TATU……………………………………………………………………. 22**
**NJIA NA MBINU ZA UTAFITI ............................................................................ 22**
3.1 Muundo wa Utafiti .......................................................................................... 22
3.2 Eneo la utafiti ................................................................................................. 22
3.3 Kundi Tafitiwa ................................................................................................ 22
3.4 Sampuli na Usampulishaji .............................................................................. 23
3.5 Ukusanyaji Data ............................................................................................. 23
3.6 Uaminifu na Uthabiti wa vifaa vya kukusanya data ....................................... 23
3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji Data ................................................................. 23
3.8 Maadili ya Utafiti ............................................................................................ 25
3.9 Hitimisho ........................................................................................................ 25
**SURA YA NNE………………………………………………………………………. 26**
**UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA ........................................ 26**
4.1 Utangulizi ........................................................................................................ 26
4.2 Maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia ......................................................... 26
4.2.1 Hadithi/ Simulizi .......................................................................................... 26
4.2.1.1 Visasili ....................................................................................................... 27
4.2.1.2 Hekaya ....................................................................................................... 30
4.2.1.3 Mighani/Visakali ........................................................................................ 36
4.2.1.4 Mbazi ......................................................................................................... 38
4.2.2 Maigizo ........................................................................................................ 45
4.2.2.1 Mazungumzo .............................................................................................. 45
4.2.2.2 Mawaidha ................................................................................................... 47
4.2.2.3 Sanaa ya maonyesho .................................................................................. 51
4.2.2.4 Miviga ........................................................................................................ 55
4.2.3 Tanzu bainifu/ Semi ..................................................................................... 58
4.2.3.1 Methali ....................................................................................................... 58
4.2.3.2 Vitendawili ................................................................................................. 60
4.2.3.3 Misemo/ Nahau .......................................................................................... 63
4.2.4 Ushairi simulizi ............................................................................................ 66
4.2.4.1 Maghani ..................................................................................................... 66

4.2.4.2 Nyimbo .......................................................................................... 69
4.3 Mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia ........................ 74
4.3.1 Mwingiliano matini kwa kuzingatia mtindo .................................................. 75
4.3.1.1 Mtindo wa ishara na taswira ........................................................ 79
4.3.2 mwingiliano kwa kuzingatia sifa za fasihi simulizi ........................................ 80
4.3.3 Mwingiliano kwa kuzingatia dhima ya fasihi simulizi katika jamii ................ 82
4.3.3.1 Kuburudisha ............................................................................ 82
4.3.3.2 kuelimisha ................................................................................ 84
4.3.3.3 Kuhifadhi historia ..................................................................... 85
4.3.3.4 Kuhifadhi utamaduni .................................................................. 89
4.4 Mchango wa Biblia katika udumishaji wa fasihi simulizi .................................. 91
4.4.1 Usanii wa watunzi wa Biblia ........................................................... 91
4.4.2 Ufasihi wa Biblia ........................................................................ 95
4.4.3 Uhalisia na uhai wa Biblia ............................................................... 98
4.4.4 Ukuzaji na uendelezaji wa stadi za lugha ................................................ 101
4.4.4.1 Tashisi ..................................................................................... 102
4.4.4.2 Takriri ..................................................................................... 103
4.4.4.3 Tashbihi ................................................................................... 105
4.4.5 Uhifadhi wa fasihi simulizi ............................................................. 106
4.5 Hitimisho......................................................................................... 107
**SURA YA TANO………………………………………………………………….. 108**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................ 108**
5.1 Muhtasari wa tasnifu……………………………………………………………. 108
5.1.1 Maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia ....................................................... 109
5.1.2 Mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia ................... 110
5.1.3 Mchango wa Biblia katika udumishaji wa fasihi simulizi .............................. 111
5.2 Mahitimisho ...................................................................................... 111
5.3 Mapendekezo .................................................................................... 112
5.4 Mapendekezo kuhusu utafiti wa baadaye ........................................................ 112
**MAREJELEO ................................................................................... 113**
**VIAMBATISHI................................................................................... 119**

**ORODHA YA VIFUNGU VYA BIBLIA.**

1.Mwanzo3:1-6,17-19

2.Mwanzo11:1-9

3.Mwanzo27:18-29

4.Mwanzo29:16-27

5.Mwanzo37:13-36

6.1Wafalme14:1-5

7.2Wafalme6:1-7

8.Mwanzo32:24-29

9.1Wafalme18:36-40

10.2Wafalme2:1-18

11.Mathayo12:38-41

12.Luka9:10-17

13.Luka8:22-24

14.Mathayo13:31-32

15.Mathayo18:21-35

16.Luka10:25-37

17.Luka18:9-14

18.Mwanzo3:1-6

19.Mwanzo25:29-34

20.Mathayo4:1-11

21.Mathayo19:3-11

22.1Wafalme2:1-9

23.Mithali1:8-19

24.Mathayo18:21-35

25.Luka10:25-37

26.Luka18:9-14

27.Mwanzo3:1-6

28.Mwanzo25:29-34

29.Mathayo4:1-11

30.Mathayo19:3-11

31.1Wafalme2:1-9

32.Mithali1:8-19

33.Mwanzo49:1-33

34.Luka6:20-26

35.1Wafalme3:6-28

36.2Wafalme4:1-6

37.Mathayo14:6-12

38.Luka22:47-62

39.Mwanzo22:1-14

40.1Wafalme8:1-5

41.Luka2:21-24

42.Mithali10:1-Mithali126:5

43.Mithali16:18-Mithali12:33

44.Luka7:41-42

45.Zaburi91:1-Zaburi140:3

46.Mithali6:14-Mithali31:20

47.Zaburi91:1

48.Zaburi45:1

49.Mithali6:21

50.Mithali31:20

51.Zaburi98:7-8

52.Zaburi90:2

53.Zaburi104:13

54.Mithali6:24

55.Mithali8:1

56.Zaburi124:1-2

57.Zaburi124:3-5

58.Zaburi129:1-2

59.Zaburi131:1-3

60.Zaburi89:13

61.Zaburi97:1-13

62.Zaburi117:1-2

63.Zaburi89:6-13

64.Zaburi8:1-9

65.Zaburi33:1-9

66.Zaburi136:1-15

67.Zaburi96:1-8

68.Zaburi118:1-4

69.Zaburi150

70.Mwanzo27:27-29

71.Luka3:4-6

72.Zaburi89:13

73.Zaburi97:1

74.Zaburi98:7-8

75.Mithali6:22

76.Mithali7:4

77.Mithali14:4-Mithali27:10

78.2Wafalme6:26-30

79.Mwanzo28:1-3

80.Mwanzo49:29-31

81.Mwanzo80:24

82.Zaburi33:1-3

83.1Wafalme2:1-4

84.Luka2:21-24

85.Luka16:19-31

86.Zaburi118:10-12

87.Mithali4:5-8

88.Zaburi106:7

89.Zaburi106:23

90.Zaburi106:47-48

91.Mathayo15:14

92.Mithali9:7-Mithali17:13

93.Luka8:18

94.Zaburi45:1;44:25

95.Mithali1:32-1:9

96.Mathayo26:47-52

97.1Wafalme12:28-30

98.1Wafalme2:11-14

99.Mwanzo25:30-34

100.Zaburi125:1

101.Mithali7:2

102.Zaburi93:3

103.Zaburi131:1

## DHANA ZILIZOTUMIKA

Vifungu vya Biblia – Sehemu za Biblia zilizonukuliwa.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

Sehemu hii inashughulikia usuli wa utafiti, swala la utafiti, maswali ya utafiti, madhumuni ya utafiti, misingi ya uteuzi, upeo wa utafiti na misingi ya nadharia.

## 1.1 Usuli wa utafiti.

Biblia takatifu si kitabu kimoja wala si maandishi ya mtu mmoja. Ni mkusanyiko wa kazi za fasihi za watu wengi zenye mada mbalimbali. Kwa mujibu wa Harold na Charles (1983), Biblia ni maktaba ya vitabu sitini na sita ambavyo vimegawika katika sehemu mbili, Agano la Kale na Agano Jipya. Maandishi haya ya Biblia yalitolewa, yakatumiwa kimasimulizi, yakakusanywa na kuhaririwa kisha baadaye yakakubalika kuwa matakatifu na yenye mamlaka. Jamii ya Biblia ya Kenya na Tanzania (1997) inasema kwamba ufasiri wa Biblia ulianza kabla ya maandishi. Upashaji wa masimulizi kwa njia ya mdomo baadaye uliwekwa katika maandishi ya vitabu vya Biblia baada ya kufasiriwa tena kwa mujibu wa hali ilivyokuwa wakati huo, kulingana na mahitaji ya jamii. Maana ziliwekwa na kila kizazi kipya na hii imechangia katika uwanja mpana wa maana ya matukio ya mwanzo yaliyohifadhiwa katika Biblia. Kwa hivyo, masimulizi ya Biblia ni dayolojia iliyo hai kati ya tamaduni iliyokumbukika na maisha yanayoendelea ya jamii ya waumini.

Kwa mujibu wa Bediako (2001), Biblia ni maktaba ya vitabu kwani ni mkusanyiko wa vitabu mbalimbali vya aina tofauti za tanzu za fasihi. Kuna ushairi ambao umejumlisha tenzi, nyimbo za mapenzi, maombi na maombolezi. Kuna methali, vitendawili na istiari. Masimulizi ya kihistoria ni pamoja na mila na desturi, wasifu, historia ya kidini, nasaba, visasili, visakale na mbazi. Kila aina ya fasihi inayo historia yake ya maendeleo. Maandishi matakatifu ni kumbukumbu ya ahadi ya Mungu na utamaduni. Bediako anaendelea kusema kwamba Biblia ni zaidi ya historia na dini ya Wayahudi na kanisa asilia. Inaonyesha uhusiano wa Mungu na watu wake pamoja na desturi zao, huku ikiwa kama kipimo ama kifani cha kutia moyo na kutambua uhusiano wote wa dini na desturi za mwanadamu. Vile jamii haiwezi kukua na kuendelea bila dini ndivyo ilivyo katika fasihi simulizi, yaani jamii haiwezi kukua na kuendelea bila fasihi

simulizi. Fasihi simulizi kwa upande mwingine imekuwa chombo cha kuhifadhi, kulinda, kutunza na kuendeleza amali za jamii ambazo ni tamaduni, mila, desturi, dini, siasa na uchumi. Amali hizi sharti zihifadhiwe katika uasili wake. Ndiposa imekuwa vyema kutafitia mwingiliano matini wa maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia ili kuendelea kuhifadhi, kutunza na kuendeleza amali za jamii ili zizidi kuhifadhiwa katika uasilia wake.

Historia ya utafiti wa fasihi simulizi ni mojawapo ya misingi inayothibitisha dhana ya kutothaminiwa kwa taaluma hii. Kwa mujibu wa Ighile (2013), fasihi simulizi ya Kiafrika ilishughulikiwa kwa mara ya kwanza na wasafiri Waingereza waliotoa maelezo kuhusu utamaduni na hali ya Afrika waliokumbana nayo katika miaka ya 1550. Kulingana naye, mfaransa kwa jina Rodger ndiye aliyekusanya masimulizi ya awali Kusini mwa Sahara, ndipo kazi nyingine zikafuata. Kutokana na kazi hizi za Kihistoria maoni mbalimbali yalitolewa kukiwemo maoni kuwa maaandishi ya awali yaliweka msingi wa kukataliwa kwa fasihi simulizi za Kiafrika. Kulingana na Finnegan (1970), taswira maarufu ya Waingereza kuhusu Afrika haikuwa na mashiko. Aliendelea kueleza kuwa ufufuaji wa motisha kwa fasihi simulizi ya Kiafrika ulitokana na utambuzi wa uwepo wa hadithi simulizi na sanaa zingine za Kiafrika.

Plekanov (1957) anaonyesha mwingiliano kati ya fasihi simulizi na taaluma ya dini. Anaeleza kwamba fasihi ni chombo mojawapo katika harakati dhidi ya mazingira na kwamba sanaa haina budi kutumiwa kumzindua mwanajamii ili apambane na mazingira machafu. Ili fasihi simulizi iwe na manufaa katika jamii, ni lazima iwe na jukumu la kuieleza jamii, kuichambua, kuikosoa na kuingoza katika lengo lake la kuupindua unyonge na uchafu uliosakini katika jamii. Fasihi simulizi hutekeleza haya kupitia kwa maumbo yake. Katika Biblia, ujumbe unaojitokeza au dhima yake ni ile ya kuonya,kufunza, kutahadharisha na kuadilisha. Ili kuweza kumzindua mwanajamii zaidi anaposoma Biblia, ilikuwa vyema kuchanganua maumbo ya fasihi simulizi katika matini teule katika Biblia ili kumsaidia kuweza kupambana zaidi na mazingira machafu yanayomzingira.

Msokile (1992) anasema kwamba fasihi simulizi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha. Kazi hii huhifadhiwa kwa kichwa na kusambazwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo. Anamalizia kwa kusema kwamba fasihi simulizi imekuwa ikirithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Vilevile,

wasomi wengi wakiwemo Harold na Charles (1983) wanaamini kwamba sehemu kubwa ya Biblia ilipitishwa kwa njia ya mdomo kwa muda mrefu sana kabla ya kuandikwa. Kwao hadithi za Biblia zinaeleweka vizuri kama ngano zilizosimuliwa kwa miaka mingi na watu wengi tofauti katika makao mbalimbali. Matini ya Biblia tuliyo nayo sasa ilitokana na masimulizi ya mdomo

Bray (1996) anaeleza kwamba mbinu mbalimbali zilizotumiwa na waandishi wa Biblia kuhusisha taarifa za hapo awali zimepewa majina mengi yakiwemo mwingiliano matini. Anaendelea kusema kwamba mwingiliano matini hutokea wakati maandishi Fulani yanapohusishwa na maandishi mengine kwa mada, mandhari, sifa bainifu au mpangilio wa masimulizi, ama kitabu kinapotaja jamii ya matini nyingine kama vile hadithi za kitamaduni. Huu ukopaji husababisha ulinganisho na uelewaji wa matini nje ya kitabu na matumizi yake ndani ya maandishi ambayo ni mwingiliano matini.

Wamitila (2003) anaeleza kwamba tanzu za fasihi simulizi huingiliana kwa kiasi kikubwa sana. Kwa mfano, hadithi huwa na ufundi wa kisanaa ambao hujitokeza kwa matumizi ya lugha yenye mvuto na iliyochanganya matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi kama vile tashbihi, methali, takriri na istiara. Mwingiliano matini kwa mujibu wa Senkoro (2011) ni ule uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya fasihi. Tunaposema kuingiliana kwa matini katika kazi za fasihi tunamaanisha kazi moja ya fasihi kuwa na sifa za tanzu nyingine ndani mwake. Escarpit (1973) anaeleza kwamba matini za Biblia hutumia lugha kuwasilisha maisha ya binadamu. Kwa mfano, utungo wa kwanza katika Biblia unasimulia mwanzo wa dunia ukitumia umbo la hadithi. Ili kuelewa hadithi, msomaji lazima azingatie umbo lake kwani maumbo huonyesha usanii.

Ntarangwi (2004) anasema kwamba kazi nyingi za fasihi simulizi hapo awali zilikuwa katika masimulizi lakini sasa zimehifadhiwa katika maandishi na huratibiwa kama kazi za fasihi. Hivyo ndivyo ilivyo hata katika Biblia takatifu. Kimball (2008) anasema kwamba maandishi ya Biblia yalitumika kama masimulizi ya mdomo kwa muda mrefu sana, yakahaririwa na kuhaririwa tena ndipo baadaye yakawekwa katika maandishi. Hii inamaanisha kuwa maandishi hayo yanatumiwa kama hifadhi ya maumbo haya ya fasihi simulizi.

Njogu (2006) anatueleza kuwa fasihi simulizi ina ubunifu wa uhai wa kipekee wenye kutoa fursa njema ya kuibua nadharia za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Aidha, kwa mujibu wa Cross (1974), katika Biblia, historia ya usomaji wa kitabu cha Wimbo ulio bora huonyesha jinsi kitabu hiki kilivyo na fasihi simulizi yenye ubunifu wa hali ya juu. Hapa tunapata jinsi maumbo ya ushairi na nyimbo yalivyotumiwa kwa ustadi na hivyo mwingiliano taaluma kati ya matini za Biblia na fasihi simulizi. Mbali na ushairi na nyimbo, utafiti huu ulinuia kuchunguza maumbo manne makuu ya fasihi simulizi yanayopatikana katika vitabu teule vya Biblia.

Mrikaria (2007) anasema kwamba fasihi simulizi ndiyo fasihi ya awali. Ilianza wakati binadamu alipoanza kutumia lugha kama chombo cha mawasiliano. Hapo ndipo mwanadamu alipoanza kuimba, kutumia methali, vitendawili, hadithi na mashairi. Fasihi hii imejengwa katika mfumo uliozoeleka wa kufikisha ujumbe kwa hadhira, na ulilenga zaidi katika kurithishana mila, desturi na tamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Fasihi hii ilirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia nyimbo, hadithi, mashairi na hata michezo ya ujasiri na majigambo. Zamani ilihifadhiwa kichwani, lakini baada ya mwingiliano wa wageni toka pande mbalimbali za dunia, ilianza kubadilika kutokana na kuingizwa kwa mila, desturi na tamaduni toka kwa wageni hawa. Wageni hawa walifanikiwa kwa kiasi kikubwa kuathiri fasihi simulizi na kuipa mkondo mpya, wanajamii wakaamini kwamba amali za wageni zilikuwa za maana kuliko zao, hivyo kutothamini fasihi simulizi yao. Hizo nyimbo, hadithi, mashairi na hata majigambo, ni maumbo ya fasihi simulizi yanayopatikana katika Biblia.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1989) tanzu za fasihi simulizi zimegawika kwa kutumia vigezo viwili ambavyo ni kigezo cha umbile na tabia ya kazi inayohusika, na kigezo cha muktadha na namna ya uwasilishaji wake. Kwa kutumia vigezo hivi, Mulokozi amezigawa tanzu na vipera vya fasihi simulizi kama masimulizi, semi, ushairi, mazungumzo, maigizo na ngomezi. Utafiti huu ulizingatia kigezo cha umbo kwani ulichunguza maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia. Ili kuonyesha jinsi fasihi simulizi ilivyojihidhirisha katika Biblia, tulichunguza maumbo ya fasihi simulizi katika vitabu teule vya Biblia tukizingatia kwamba Biblia ndicho kitabu cha mwanzo cha fasihi kilichowahi kuandikwa na kusambazwa kote ulimwenguni, (Lee 1998). Aidha Biblia ni maktaba ya vitabu vya fasihi kwa sababu ina vitabu vingi sana ambavyo vina aina mbalimbali

za maumbo ya fasihi simulizi. Ushairi ulio pamoja na tenzi, maombi, maombolezi na nyimbo za mapenzi, vitendawili, methali na istiari pamoja na hadithi za kihistoria, kila mojawapo ikiwa na historia yake ya maendeleo.

Maumbo ya fasihi simulizi hapa inamaanisha tanzu au vipengee vya fasihi simulizi vinavyopatikana katika fasihi simulizi kama taaluma; na muundo hujaribu kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ishara na vipashio mbalimbali vinavyopatikana katika kazi ya sanaa. Finnegan (1970) anathibitisha kwamba kuna maumbo mbalimbali ya fasihi simulizi. Utafiti huu ulizingatia maumbo manne makuu ambayo ni ushairi simulizi, semi, mazungumzo na masimulizi katika kuchunguza mwingiliano matini wa maumbo ya fasihi simulizi na matini matini teule za Biblia.

### 1.2 Swala la Utafiti

Biblia takatifu ni mkusanyiko wa vitabu mbalimbali vya aina tofauti tofauti za fasihi. Kuna vitabu vya Biblia ambavyo vimepewa majina ya maumbo ya fasihi simulizi kama vile kitabu cha Methali, na Wimbo ulio bora. Vitabu vingine hata ingawa havijapewa hayo majina vinao utajiri mwingi wa fasihi simulizi kwani vinaonyesha uhusiano wa binadamu pamoja na desturi zao. Kuna ushairi, methali, vitendawili na masimulizi ya kihistoria, zote ambazo ni tanzu za fasihi simulizi. Ingawa kumekuwa na tafiti anuai kuhusu maumbo ya fasihi simulizi kiujumla, chache zimefanywa kuhusu mwingiliano matini wa maumbo ya fasihi simulizi ya Kiafrika na matini teule za Biblia. Utambuzi wa maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia unatoa uelewa mzuri kuhusu umbo la matini simulizi, kwa hivyo kuna haja ya kuyatathmini maumbo haya katika vitabu teule vya Biblia na kuchunguza jinsi fasihi simulizi inavyojitokeza kama sehemu ya kuwasilisha maana katika Biblia. Kwa kuhusisha Biblia na fasihi simulizi, utafiti huu uliweka msingi wa kuelewa maumbo ya fasihi simulizi kwa wepesi tunaposoma Biblia. Utafiti huu aidha, utaweza kupanua uwanja wa fasihi simulizi kwa kukuza swala la mwingiliano matini hasa matini ya fasihi simulizi na dini kupitia kwa matini za Biblia.

### 1.3 Maswali ya utafiti

Maswali ya utafiti yaliyoongoza utafiti huu ni haya:

1. Ni vipengee vipi vya fasihi simulizi ambavyo vinapatikana katika Biblia?
2. Ni vipi taaluma ya fasihi simulizi inavyoingiliana na matini teule za Biblia?

3. Ni upi mchango wa  Biblia katika ukuzaji wa fasihi simulizi?

**1.4 Madhumuni ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuhakiki kwa kina jinsi maumbo ya fasihi simulizi yanavyodhirihika katika vitabu teule vya Biblia. Ili kufikia lengo hili, madhumuni maalum yafuatayo yalishugulikiwa.

1. Kuchanganua vipengee vya fasihi simulizi  katika matini teule katika Biblia
2. Kupambanua  mwingiliano taaluma wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia
3. Kutathmini mchango wa Biblia katika ukuzaji wa fasihi simulizi.

**1.5 Misingi ya Uteuzi**

Biblia ingawa ni kitabu kitakatifu cha dini ya Kikristo, misingi yake mikuu ni tamaduni za Wayahudi. Ni mkusanyiko wa vitabu vyenye maumbo kadha ya fasihi simulizi. Aina mbalimbali za fasihi ya Biblia zinawakilisha maumbo kama vile masimulizi, historia, sheria, ushairi, utabiri, nyimbo na barua. Maumbo haya yalinuiwa kutumika katika mkao maalum na kukamilisha kazi maalum. Kwa mujibu wa Gunkell (1832)  utambuzi wa maumbo ya Biblia ulitoa ufahamu/uelewa mzuri kuhusu umbo la matini simulizi. Kuna haja ya uhariri tangulizi katika Biblia kumwelekeza msomaji kuhusu maumbo yenyewe. Vilevile wasomi wengi wanaamini kwamba sehemu kubwa ya Biblia ilisimuliwa kwa mdomo, ama kupitishwa kwa mdomo kupitia desturi simulizi kitambo kabla ya kuandikwa. Kulingana na Gunkel (1862) hadithi za Biblia zinaeleweka vizuri sana kama ngano ambazo ziliganwa kwa miaka mingi na watu wa aina mbalimbali, katika makao anuwai. Matini ya Biblia tuliyo nayo sasa ilitokana na maendeleo marefu ya mfumo huu. Mwingiliano matini wa maumbo ya fasihi simulizi na matini teule za Biblia ni swala ambalo lilifaa kubainishwa kikamilifu.

Robert (1981) anaeleza kwamba Biblia inazo hadithi za kuvutia na lugha yenye mvuto. Inamaanisha vitu vingi kwa watu wengi. Sio kitabu cha wakristo na wayahudi pekee, bali ni fasihi iliyo na mgongano wa kina kwa fasihi zingine, kuhusu maoni ya historia ya binadamu na jamii na maisha ya watu binafsi. Utafiti huu utawafaa hata wale wasio wa dini ya kikristo ama kiyahudi kusoma Biblia kwani watagundua kwamba Biblia ni mkusanyiko wa vitabu vya fasihi.

Bediako (2001) anasema kwamba vitabu vya Biblia vinaweza kusomwa na yeyote yule anayetumai kujiendeleza kifasihi hasa fasihi simulizi. Utafiti huu pia kwa kuihusisha Biblia na fasihi simulizi umeweka msingi wa kuelewa maumbo ya fasihi simulizi kwa wepesi wakati tunaposoma Biblia. Itaeleweka ya kwamba mbali na vitabu vilivyoandikwa hasa kusomwa kama fasihi simulizi, Biblia vilevile inaweza kusomwa kama kitabu cha fasihi na tanzu zote za fasihi simulizi pamoja na vipera vyake vipatikane humo.

Msokile (1993) anaeleza kuwa mhakiki wa fasihi simulizi husaidia katika ujenzi wa jamii kwa kuzingatia maadili, ujumbe, falsafa na jumla ya kazi inayohusika. Katika Biblia, ujumbe unaojitokeza, au dhima yake ni ile ya kufunza, kuonya, kutahadharisha na kuadilisha. Kulingana na maelezo haya, utafiti huu utamwezesha mhakiki kusaidia katika kujenga maadili, ujumbe na falsafa ya jamii kama inavyotendeka katika fasihi simulizi na pia kumsaidia kutumia maumbo ya fasihi simulizi kama mojawapo ya vigezo vya kutathmini ufanisi wa usanii kwani maumbo ndiyo usanii wa matini. Ili kutathmini kazi ya sanaa ni vyema kuchunguza maumbo. Aidha, utafiti huu unaazimia kupanua mipaka ya fasihi simulizi kwa mujibu wa kubainisha mwingiliano taaluma wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia. Hii itachochea wasomi wengi, wakiwemo wanafunzi na hata walimu wa shule kusoma Biblia ili kubainisha mwingiliano huo, hivyo kupanua mipaka ya fasihi simulizi.

Utafiti huu kupitia nadharia ya mwingiliano matini umeonyesha jinsi fasihi simulizi inavyoweza kukuzwa kwa kuzingatia mchango wa Biblia. Umeonyesha jinsi kazi za kifasihi zinavyoingiliana na kuhusiana, na jinsi waandishi wa vitabu teule vya Biblia walivyotumia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi katika kazi zao. Njogu na Wafula (2007) wanasema kuwa kazi ya fasihi ina sauti kadhaa zinazoingiliana na hupiga mangwi katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo na zitakazokuja baadaye.

Utafiti huu utakuwa muhimu hasa kwa wasomi mbalimbali kwani watagundua mitazamo tofauti ya Biblia takatifu, kwamba ni mkusanyiko wa vitabu vya kifasihi ambavyo vinaweza kutumiwa na yeyote anayesomea fasihi hasa fasihi simulizi. Si kitabu cha kiroho tu. Aidha, utafiti huu utachangia mno ukuaji wa fasihi simulizi katika Kiswahili na hivyo basi kuwa changamoto kwa utafiti linganishi kufanywa kuhusu maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia, kwani matini ya

Biblia itaweza kutazamwa kama matini ya fasihi simulizi. Hapa utafiti umeonyesha mwingiliano taaluma na jinsi taaluma mbalimbali zinavyochangiana, huku mchango wa vitabu teule vya Biblia katika fasihi simulizi ukionekana, nao mchango wa fasihi simulizi katika Biblia pia ukionyeshwa.

**1.6 Upeo wa utafiti**

Utafiti huu ulichunguza vitabu teule vya Biblia takatifu kutoka Agano la kale na Agano jipya. Upeo wa utafiti huu ni vitabu saba vya Biblia ambavyo ni; kitabu cha Mwanzo, Wafalme wa kwanza na Wafalme wa pili, Zaburi na kitabu cha Methali kutoka Agano la kale; na Matayo na Luka mtakatifu kutoka Agano jipya. Mtafiti alichunguza jinsi maumbo manne makuu ya fasihi simulizi ambayo ni: hadithi, maigizo, semi na ushairi simulizi, pamoja na vipera vyao yanavyojitokeza katika Biblia. Vilevile alipambanua mwingiliano taaluma wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia, kisha akatathmini mchango wa Biblia katika ukuzaji wa fasihi simulizi.

**1.7 Misingi ya Nadharia**

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya mwingiliano matini iliyoasisiwa na Julia Kristeva (1969) ambaye aliizua kutokana na nadharia ya usemezano ya Mikhail Bakhtin (1968). Kwa mujibu wa Bakhtin (1968) mawazo na kazi zozote za usanii, hazitungwi kutokana na ombwe, na wala si mali kamili ya mtunzi, bali ni matokeo ya usemezano unaoendelea kati ya mtunzi na wasanii wa awali. Kristeva (1969) anaeleza kuwa matini inabuniwa na matini zilizopo. Watunzi hawabuni matini kutokana na fikra zao wenyewe, ila hukusanya mawazo kutoka kwa matini zilizopo. Kwake, matini si kitu huru, ila ni mkusanyiko wa matini za kitamaduni. Hali hii ilibainika katika kazi hii kutokana na jinsi Biblia takatifu inavyojengwa na maumbo ya fasihi simulizi.

Kristeva (1978) anaeleza kwamba hakuna matini yoyote ya kifasihi inayoweza kujitegemea bila kuhusiana na matini nyingine; kwamba kila usanii ni mwingiliano mchanganyiko au upangaji mpya wa mawazo yaliyokuwepo hapo awali.  Anadai kwamba waandishi hawabuni matini kutokana na fikra zao wenyewe, bali hukusanya mawazo kutoka kwa matini zilizopo. Hii hupelekea matini kuwa ugeuzaji taratibu wa matini au mwingiliano matini katika nafasi ya matini maalum.

Kwa mujibu wa Saussure (1959), matini hujengwa kutoka matini nyingine. Anadai kwamba matini haiwezi kukaa pekee yake, bali huundwa kutokana na kurudia rudia na kubadilishwa na kuingizwa katika matini nyingine. Hii inatokana na dai kwamba kwa kuwa mwandishi ni msomaji wa matini kabla ya kuandika matini yake, kazi yake bila shaka huathiriwa na kazi nyingine kupitia marejeleo na miingiliano tofauti tofauti. Kwa Saussure, mtunzi asilia hatazamwi kama muasisi, bali hutazamwa kama mdokoaji wa vipengee mbalimbali vya kifasihi na kuviweka katika kazi moja ya fasihi. Mtazamo huu ulifaa utafiti huu kwa vile ulichunguza jinsi matini ya fasihi simulizi inavyoingiliana na matini teule ya Biblia

Kristeva (1978) anaendelea kueleza kwamba matini si kitu binafsi ila ni mkusanyiko wa matini za kitamaduni. Akirejelea dhana ya usemezano wa Bakhtin, anaeleza kwamba matini maalum na matini ya kitamaduni hubuniwa kutokana na malighafi sawa ya kimatini ambayo haiwezi kutenganishwa. Dhana hii ilizua uhusiano baina ya mtunzi, kazi, msomaji, jamii na historia. Njogu na Wafula (2007) vilevile wakimrejelea Bakhtin wanasema kuwa kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mangwi katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo na zitakazokuja baadaye. Kulingana kwa matini katika kazi za fasihi humaanisha kazi moja ya kifasihi kuwa na sifa za kazi nyingine za kifasihi. Mtazamo huu ulifaa utafiti huu kwa vile ulichunguza jinsi maumbo ya tanzu za fasihi simulizi yanavyoingiliana na matini ya vitabu teule vya Biblia na kufanya maumbo hayo yaonekane wazi wakati wa usomaji wa Biblia.

Kristeva (1986) aidha, anaeleza kwamba matini hujengwa kutokana na matini za awali kwa sababu matini ni sehemu muhimu ya historia; kwamba matini hujengwa upya, hutilia mkazo na ni mangwi wa matini za awali hivyo hujenga historia ya kuchangia mabadiliko mengi katika matini huku zikitazamia kujenga matini za baadaye. Kristeva anaendelea kusema kwamba mwingiliano matini ni kuweka historia katika matini na matini katika historia. Kwake, kuweka historia katika matini kunamaanisha kuwa matini huhusishwa na kujengwa na matini za awali. Kwa hivyo kutegemea nadharia hii, tuliazimia kuangalia jinsi matini huhusisha na kujengwa kutokana na matini za awali tukizingatia kwamba matini ni sehemu muhimu ya historia; hujenga historia na kuchangia mabadiliko mengi katika matini aidha, zikitazamia kujenga matini za

baadaye. Ili kujadili vipengee vya fasihi simulizi vinavyopatikana katika vitabu teule vya Biblia, na kutathmini mchango wa Biblia katika ukuzaji wa fasihi simulizi,mawazo haya yalifaa.

Mushenyezi (2003) anasema kwamba kuna uhusiano wa vipengele vingine nje ya muktadha wa usomaji na usimulizi wa kazi ya fasihi. Anaeleza kwamba dhana ya kuingiza vipengele hivi ndiyo inayoitwa mwingiliano matini. Anashikilia kuwa kazi ya kifasihi huingiliana na kuhusiana katika kile kinachoweza kuitwa mwanda wa kimwingiliano matini. Mawazo haya yalifaa utafiti huu kwani mbali na vipengele mbalimbali vya fasihi simulizi vinavyopatikana katika Biblia kutambuliwa na kujadiliwa, mwingiliano taaluma wa fasihi simulizi na dini kupitia matini teule za Biblia ulipambanuliwa.

Aidha, uhusiano wa vipengele vingine nje ya muktadha wa usomaji na usimulizi umeonyeshwa. Kristeva (1986) anaendelea kusema kuwa mwingiliano matini ni hali ambapo matini huingiliana na matini nyingine huku ikifanya matini moja kumezwa na matini nyingine. Kwake, msomaji wa kipekee ni yule mwandishi anayesoma matini nyingine, ambayo ni sawa na matini kujisoma yenyewe huku ikijiandika yenyewe. Mwingiliano matini vilevile huhusishwa na maudhui yanayohusiana na kuingiliana katika miktadha mbalimbali ya utunzi. Hauhusishwi na muktadha mmoja wala mtunzi maalum, ila unahusishwa na kuwepo kwa tatizo linalolingana katika muktadha mmoja wa kitamaduni na kijamii. Maudhui pekee yanaweza kuwa kipengee kinachohusisha matini ambazo kwa kawaida ni tofauti kabisa. Ni vyema kuelewa kwamba uandishi wa Biblia uliathiriwa na tamaduni mbalimbali.

Wamitila (2006) akimrejelea Bakhtin, anasema kwamba utanzu wa fasihi una uwezo wa kuingiza vipengele vya tanzu nyingine lakini ukabakia na sifa zake kama utanzu. Kwake, utanzu wa fasihi kuwa na vipengele vingine ndani yake hakuondoi hadhi ya utanzu huo, bali kuingiliana kwa matini katika kazi za fasihi kunamaanisha kazi moja ya kifasihi kuwa na sifa za tanzu nyingine ndani yake.

Miruka (2013) akitumia nadharia ya mwingiliano matini katika utafiti wake alizingatia nguzo tatu za nadharia hii: mwingiliano matini maumbo ambayo ilimsaidia kuchunguza maumbo na miundo asilia ya tanzu za fasihi simulizi katika mashairi andishi ya Kiswahili; mwingiliano tanzu

ambayo ilimsaidia kuchunguza maumbo mbalimbali na jinsi yalivyomezwa na utanzu changamano wa ushairi andishi wa Kiswahili; na mwingiliano matini wa kitamaduni uliomwezesha kuchunguza maumbo simulizi yanayoainishika kutokana na maudhui yaliyowasilishwa.

Nadharia hii imeibua mitazamo mbalimbali kutoka kwa wataalamu mbalimbali. Allen (2000) anaeleza kwamba kwa mujibu wa kazi za fasihi, nadharia ya mwingiliano matini na kazi za fasihi zimejengwa kutokana na mifumo, kanuni na taratibu zilizokubaliwa na jamii na tamaduni zilizojengwa na kazi za zamani za fasihi. Tendo la kusoma humtosa msomaji katika mfumo wa uhusiano wa kimatini unaohusiana na matini zingine. Kufasiri matini na kuelewa maana yake husaidia kugundua hayo mahusiano. Kusoma kunakuwa mfumo wa kusonga kutoka matini moja hadi nyingine. Maana hupatikana kati ya matini moja na matini nyingine, zote ambazo zinahusiana. Mtazamo huu kwa hivyo ulifaa utafiti huu kwani unahusu mwingiliano matini kati ya fasihi simulizi na matini teule za Biblia. Uliazimia kuangalia jinsi maumbo ya fasihi simulizi na matini teule za Biblia zinavyoingiliana. Mtazamo huu vilevile uliazimia kuangalia jinsi tanzu kama vile mashairi, hadithi, mazungumzo na maigizo katika fasihi simulizi huhusiana na kuingiliana na zile za Biblia.

Nadharia ya mwingiliano matini si ngeni kwa fasihi simulizi ya kiafrika. Fasihi simulizi ya Afrika inajulikana kwamba haina mtunzi maalum, yaani, tanzu za fasihi simulizi za kiafrika zinachukuliwa kwamba hazina mtunzi maalum, bali ni mali ya jamii ambayo inapitishwa kutoka kizazi hadi kizazi (Finnegan, 1970). Kwa wanaounga mkono nadharia hii, fasihi hutokana na fasihi. Waandishi wa fasihi simulizi aidha hutumia matini za awali katika uandishi wao. Uelewa huu ulitusaidia katika utafiti huu kwa kutuwezesha kutambua uhusiano wa maumbo ya fasihi simulizi na Biblia. Bodumbe (1994) anaeleza kwamba nadharia ya mwingiliano matini inafaa historia ya fasihi kwani inasaidia katika kufafanua matukio ya kazi ya fasihi, kwa sababu kila fasihi au matini ina uwezo wa kuathiri na kupanua maana ya nyingine.

Nadharia ya mwingiliano matini pia hutumiwa kuhakiki tofauti na desturi za kitamaduni katika fasihi. Mambo waliyopitia waafrika wakati wa ukoloni yaliathiri utamaduni wao kupitia kwa mifumo ya kikoloni ya shule, dini, utamaduni wa mkoloni na kadhalika; na hivyo kuathiri fasihi

simulizi yao kupitia kwa tanzu kama hadithi, ushairi, mazungumzo na kadhalika. Mwingiliano matini huzingatia historia ya matini nyingine na athari zake kwa matini iliyopo.

Nadharia hii inayo mihimili mbalimbali ingawa utafiti huu ulizingatia mihimili mitatu. Mhimili wa kwanza kwa mujibu wa Kristeva (1978) ni kwamba kila matini ina uhusiano na matini nyingine, yaani matini zote zinafaidika zaidi kutoka kwa matini nyingine kuliko watunzi wake. Hapa, matini huchukua sifa na maumbo asilia ya kitamaduni ya tanzu zingine na kubadilishwa na tanzu hizo, hivyo maumbo ya matini yakiwa yameingizwa katika matini nyingine, (Kristeva 1969). Kwa kuwa utafiti huu ulichunguza maumbo asilia ya tanzu za fasihi simulizi katika Biblia, hii iliweza kutumika.

Mhimili wa pili ni kwamba matini huundwa na watunzi wengine kwa njia nyingi. Matini hupeana umatini ambamo matini nyingine zinaweza kuundwa na kufasiriwa. Hapa mwingiliano unahusu mazungumzo baina ya matini au watunzi wa matini mbalimbali. Kumaanisha kwamba matini huundwa kutokana na vipengele vya mazungumzo au dayalojia anavyoeleza Kristeva (1985). Mhimili huu ulitusaidia kubainisha jinsi fasihi simulizi na matini teule ya Biblia zinavyoingiliana.

Mhimili wa tatu ni kwamba fasihi hutokana na fasihi, kumaanisha kwamba waandishi wa fasihi simulizi hutumia matini za awali katika uandishi wao. Kulingana na jinsi anavyoielewa matini, mwandishi au mtunzi huweza kudokeza vipengle vya mwingiliano katika matini mbalimbali. Hapa, hoja hubuniwa kutegemea watu wengine, matini na mazingira. Hoja zenyewe zinaweza kubadilika na kuundwa tena kutegemea mazingira. Mhimili huu ulifaa katika utafiti huu kwani ulituwezesha kutathmini mchango wa Biblia katika ukuzaji wa fasihi simulizi kwani Biblia ilitumika kama kitabu cha fasihi simulizi.

Worthrop (1957) anaeleza kwamba usanii huiga usanii, na kwamba uhai vilevile huiga usanii. Matini husaidia sio tu kwa kutunga matini nyingine, bali pia huondoa mipaka kati ya matini na matini, na pia kati ya matini na yale yanayoshuhudiwa duniani. Matini ya maumbo ya fasihi simulizi yanahusiana sana na yale yanayotendeka ulimwenguni, ambayo ni sawa na matini ya Biblia. Kwa hivyo mwingilian o matini kati ya maumbo ya fasihi simulizi na matini teule ya

Biblia ilitathminiwa. Nadharia ya mwingiliano matini kwa jumla ilifaa utafiti huu kutokana na dhana yake kuu kuwa hakuna matini yoyote inayoweza kujisimamia bila kuhusishwa na matini nyingine. Kwa sababu hii, vitabu teule vya Biblia vilihusishwa na fasihi simulizi ili kuonyesha jinsi vinavyotegemeana kimaumbo

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii ilishughulikia tahakiki ya maandishi mbalimbali yanayohusiana na mwigiliano wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia. Ili kuchunguza swala hili, vipengele vinne vimeshughulikiwa, ambavyo ni ; Dhana ya fasihi simulizi; Fasihi simulizi na matini teule za Biblia; Mchango wa Biblia katika fasihi simulizi na mapitio kuhusu nadharia. Michango, mitazamo na matokeo ya tafiti za awali imetolewa ili kuonyesha pengo.

## 2.2 Dhana ya fasihi simulizi

Fasihi simulizi ni dhana ambayo imeelezwa na wataalamu wengi kutegemea nadharia na mitazamo mbalimbali. Finnegan (1970) anaeleza kuwa fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutegemea msanii ambaye huimba kwa maneno katika tukio maalum. Balisidya (1983) anafasili fasihi simulizi kama aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo katika kuimba, kuiwasilisha na kusambaza kwa wasikilizaji na watumiaji wake. Fasili hii ina upungufu kwani haijafafanua juu ya ubunifu alio nao msanii katika kuikamilisha na pia katika swala la uwasilishaji.

Msokile (1992) anafafanua kwamba fasihi simulizi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha. Kazi hii huhifadhiwa kwa kichwa na kusambazwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo kupitia kwa maumbo tofauti tofauti. Anamalizia kwa kusema kwamba fasihi simulizi imekuwa ikirithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Uelewa wa dhana hii ya fasihi simulizi ulituwezesha kuelewa maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia kwani vipengee vya fasihi simulizi vinavyopatikana katika Biblia vilijadiliwa.

Mulokozi (1996) anasema fasihi simulizi ni fasihi inayotendwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo bila kutumia maandishi, hivyo fasihi simulizi ni tukio linalofungamana na muktadha (mazingira) fulani wa kijamii, hasa muktadha wa Kidini, na kutawaliwa na mwingiliano wa fanani, hadhira, fani inayotendwa, tukio, mahali na wakati. Anaendelea kusema kuwa fasihi simulizi ni ile inayotendwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo.

Ngure (2003) anaeleza fasihi simulizi kama sanaa itumiayo maudhui yake kwa lugha ya maneno ambayo hutamkwa ama kutendwa. Anasisitiza kwamba fasihi ni namna ya utoaji maudhui kisanaa na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo ambayo huweza kutamkwa au kutendwa.Kwa mujibu wa TUKI (2004) fasihi simulizi ni kazi ya fasihi inayohifadhiwa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kusemwa kwa njia ya mdomo kama vile hadithi, ngano na vitendawili. Kutokana na maelezo hayo tunaweza kusema kuwa fasihi simulizi ni kazi ya sanaa inayotumia mazungumzo ikihusisha utendaji na njia nyingine za mawasiliano ili kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Sehemu hii vile vile ilitusaidia katika kuelewa fasihi simulizi na kujadili vipengee vyake vinavyopatikana katika Biblia na jinsi inavyotumia mazungumzo ikihusisha utendaji na njia nyingine za mawasiliano ili kufikisha ujumbe kwa jamii husika.

Njogu (2006) anaeleza kuwa fasihi simulizi ina ubunifu na uhai wa kipekee wenye kutoa fursa njema na kuibua nadharia za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Anaifananisha fasihi simulizi na uti wa mgongo wa maendeleo ya binadamu kwani ndani yake kuna masimulizi, maigizo, tathmini za mazingira na mahusiano ya kijamii.

M'Ngaruti (2008) anaeleza kuwa fasihi simulizi huhusisha semi. Hizi ni tungo au kauli fupi fupi za kisanaa zenye kubeba maana au mafunzo muhimu ya jamii. Semi hujumuisha tanzu kama vile methali, vitendawili, mafumbo, misimu, lakabu na kauli tauria. Alexlord & Cooper (1988) vile vile anaeleza kwamba katika fasihi, lugha hutumika kwa njia ya kiubunifu na inahusisha matumizi ya methali, sitiari, vitendawili, mafumbo na tamathali nyinginezo. Anaendelea kusema kuwa lugha katika fasihi hutumiwa kisanaa na kiufundi. Mbali na semi, utafiti huu ulijadili maumbo mengine ya fasihi simulizi kama vile hadithi, ushairi na mazungumzo katika Biblia, wala sio katika fasihi simulizi kwa jumla. Sehemu hii kwa hivyo iliwezesha utafiti huu kutathmini vipengee vya fasihi simulizi vinavyopatikana katika Biblia.

Finnegan (2012) anaonyesha jinsi taswira mpya ilivyoanza kujengeka katika uwanja wa fasihi simulizi hata ikahimiza kutambuliwa kwa kazi za watu wengine walioanza kutafitia fasihi simulizi katika bara la Afrika. Ili kujaribu kutoa mwelekeo thabiti kwa uchunguzi wa fasihi simulizi, Okpewho (1979), alichapisha kazi yake kama jaribio la kuelekeza katika uchunguzi wa fasihi simulizi. Tangu wakati huo waandishi na wasomi mbalimbali wamekuwa wakifanya utafiti

kuhusu fasihi simulizi ya Kiafrika. Kwa kuwa tafiti anuwai zimefanywa kuhusu fasihi simulizi za Kiafrika, kulikuwa na haja ya kuendeleza utafiti wa fasihi simulizi hasa kwa kujadili vipengee vyake vinavyopatikana katika Biblia. Ndiyo sababu utafiti huu unaendelezwa ili kuendelea kupanua uwanja wa fasihi simulizi.

**2.3Fasihi simulizi na matini teule za Biblia.**

Mwingiliano matini katika kazi za fasihi simulizi ni dhana ambayo imekuwa ikijitokeza sana. Mulokozi (1989) anasema kwamba mojawapo ya sifa kuu za fasihi simulizi ni vipera vyake kuingiliana katika utendaji. Naye Senkoro (2011) anasema kuwa mwingiliano matini ni ule uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya fasihi.

Tanzu ni istilahi inayotumiwa kueleza au kurejelea aina ya kazi mbalimbali za kifasihi. Inawezekana utanzu mkuu kuwa na vitanzu vingine mbalimbali (Wamitila 2003). Kuna tanzu nyingi za fasihi simulizi ambazo zimewekwa katika makundi au tanzu nne kuu ambazo ni hadithi, semi, maigizo na ushairi simulizi. Kwa kuziainisha tanzu hizo katika makundi manne makuu, Wamitila ametuachia nafasi ya kuzitafitia zaidi. Kwa hivyo utafiti huu ulitambua tanzu za fasihi simulizi katika matini teule za Biblia na hivyo kuweza kupambanua mwingiliano taaluma wa fasihi simulizi na dini kupitia kwa matini teule za Biblia.

Gunkel (1862 – 1932) alijaribu kupanga maandishi ya Biblia kulingana na maumbo yake. Gunkel alichochewa na Grimm ambaye alikusanya ngano za kijerumani na akaziainisha katika makundi kama visasili, visakale na mighani. Kwa mujibu wa Gunkel, utambuzi/ uainishaji wa maumbo ya Biblia ulitupa habari muhimu kuhusu simulizi za hapo awali na kazi yake katika Israeli ya zamani.

Matteru (1987) amesema kwamba katika muktadha wa fasihi simulizi ushairi ni fungu linalojumlisha tungo zote za fasihi simulizi zenye kutumia mapigo kwa utaratibu maalumu. Mapigo haya yanaweza kuwa ya kimuziki au yoyote yale yaliyopangwa kwa muwala wa uwazi. Tanzu kama nyimbo, maghani, methali, vitendawili na misimu hupatikana katika kundi hili.

Kwa upande mwingine Matteru (1987) anasema kwamba tanzu za kinathari zinajumuisha tungo zote za fasihi simulizi zenye kutumia lugha ya kawaida ya maongezi. Matteru anamalizia kwa

kusema kwamba nathari hujumuisha tanzu kama hadithi, ngano, tarihi, visasili, vigoma, na masimulizi. Matteru anazitambua tanzu za fasihi simulizi kama vile ushairi na nathari na kufafanua vipera vyake kwa jumla. Utafiti huu ulidhamiria kuzijadili hizi tanzu katika matini teule ya Biblia na kupambanua jinsi fasihi simulizi na matini teule za Biblia huingiliana.

Mulokozi (1989) ameainisha tanzu za fasihi simulizi kwa kutumia vigezo viwili ambavyo ni umbile na tabia ya kazi inayohusika, na muktadha na namna ya uwasilishaji wake kwa hadhira. Katika kigezo cha umbile na tabia ya kazi inayohusika Mulokozi ameangalia vipengele kama mashairi, nathari, nyimbo, mafumbo na mighani. Katika muktadha na namna ya uwasilishaji, amezingatia kuwa, fasihi simulizi ni tukio hivyo huambatana na mwingiliano wa mambo matatu ambayo ni muktadha, watu na mahali. Mwingiliano huu ndio unaotupa muktadha na muktadha ndio huamua fani fulani ya fasihi simulizi ichukue umbo lipi, iwasilishwe vipi kwa hadhira. Kwa kutumia vigezo hivi Mulokozi (1989) amezigawa tanzu za fasihi simulizi katika utanzu wa fasihi simulizi wenye kusimulia habari fulani, semi, ushairi , mazungumzo, maigizo na ngomezi

Wamitila (2003) anasema kwamba kuna maumbo makuu manne ya fasihi simulizi. Uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi hutegemea misingi kadhaa, ikiwemo matumizi ya lugha kwa jumla na uwasilishaji kwa hadhira ambapo mada na viini vya tanzu huchunguzwa. Ameainisha maumbo manne ambayo ni simulizi / hadithi, maigizo, ushairi, na semi au tanzu bainifu. Kila kundi lina vipera vyake. Utafiti huu ulichunguza hayo maumbo na jinsi yanavyojidhihirisha katika vitabu teule vya Biblia. Hii ilisaidia katika kupambanua mwingiliano taaluma wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia.

Peter (2012) anachunguza muziki wa kizazi kipya kama utanzu wa fasihi simulizi ya Kiswahili. Anafafanua jinsi muziki ulivyo utanzu wa fasihi simulizi. Amehakiki mchango wa muziki wa kizazi kipya kwa fasihi simulizi ya Kiswahili na pia kutawaza muziki wa kizazi kipya kama tawi la fasihi simulizi. Kwa jumla, ameweza kuonyesha jinsi fasihi simulizi inavyoweza kugawika kwa vipera na tanzu tofauti tofauti katika lugha ya Kiswahili kama vile ushairi ambao unahusisha nyimbo na maghani. Utafiti huu ulikuwa tofauti kwa sababu haukushughulikia muziki kama utanzu wa fasihi simulizi, bali ulitambua maumbo ya fasihi simulizi yanayopatikana katika vitabu teule vya Biblia wala si katika mashairi.

Miruka (2013) katika utafiti wake anachunguza maumbo ya fasihi simulizi katika mashairi andishi. Anaeleza kwamba utafiti wake umeegemezwa kwa dhana kuwa ushairi wa Kiswahili ni mwingiliano wa tanzu za fasihi simulizi. Anachunguza maumbo ya fasihi simulizi katika mashairi andishi ya Kiswahili ili kuthibitisha mchango wao katika kuyakuza. Amejadili tanzu mbalimbali za fasihi simulizi zinazopatikana katika mashairi andishi na kukuza dhana kuwa ushairi wa Kiswahili una mwingiliano wa tanzu za fasihi simulizi. Utafiti wake ulibainisha maumbo manne makuu ya fasihi simulizi yanayodhihirika katika mashairi andishi ya Kiswahili, yaani hadithi, maigizo, semi na ushairi simulizi. Alieleza kuwa maumbo ya fasihi simulizi husukwa kwa jinsi mbalimbali katika mashairi andishi hivyo kukuza tungo za kishairi huku zikisaidia kujenga ploti nzima ya mashairi andishi na fasihi kwa jumla. Utafiti huu kwa upande mwingine ulikuwa tofauti kwa sababu ulichunguza maumbo haya katika vitabu teule vya Biblia wala si katika mashairi andishi anavyofanya Miruka.

### 2.4 Mchango wa Biblia katika Fasihi Simulizi

Biblia sio kitabu kimoja tu, wala hakikuandikwa na mtu mmoja. Ni mkusanyiko wa kazi za fasihi za watu wengi.  Kwa mujibu wa Lee (1998), Biblia iliandikwa katika kipindi cha miaka 1500 hivi. Historia na unabii unaopatikana ndani yake unahusiana na serikali saba kuu za ulimwengu: Misri, Ashuru, Babiloni, Umedi na Uajemi, Ugiriki, Roma na Muungano wa Uigereza na Merikani. Ingawa ni kitabu kitakatifu, misingi yake mikuu ni tamaduni za wayahudi. Ni mkusanyiko wa vitabu vyenye maumbo kadha ya fasihi simulizi kama anavyoeleza Cross (1974). Mbali na kuwa mkusanyiko wa vitabu vyenye maumbo kadha ya fasihi simulizi, utafiti huu ulitarajia kutathmini jinsi Biblia inavyochangia katika ukuzaji wa fasihi simulizi kupitia maumbo haya.

Menlken (1946) anaeleza kwamba Biblia ni zaidi ya kazi ya fasihi. Inahusisha theolojia, historia na fasihi. Kulingana na Menlken, fasihi inayo maumbo yake. Masimulizi huwasilisha maana yake kupitia kwa wahusika na utendaji wao. Ili kuelewa hadithi, msomaji lazima azingatie umbo. Vilevile si rahisi kuelewa maana ya shairi kabla ya kuelewa umbo la shairi lenyewe. Ni haya maumbo ya fasihi simulizi ambayo utafiti huu uliyatambua katika matini teule za Biblia na pia ukatathmini jinsi Biblia inavyosaidia katika ukuzaji wa fasihi simulizi.

Plekanov (1957) amesema kwamba fasihi, ikiwemo fasihi andishi na fasihi simulizi, ni chombo mojawapo katika harakati dhidi ya mazingira. Mtazamo huu unaashiria kwamba sanaa haina budi kutumiwa kumsukasuka na kumzindua mwanajamii ili apambane na mazingira machafu. Ili fasihi simulizi iwe na manufaa katika jamii, ni lazima iwe na jukumu la kuieleza jamii, kuichambua, kuikosoa na kuiongoza katika lengo lake la kuupindua unyonge na uchafu uliosakini katika jamii. Fasihi simulizi hutekeleza haya kupitia maumbo yake. Utafiti huu kwa upande wake haukulenga kuonyesha jukumu la fasihi simulizi katika jamii, bali ulinuia kutathmini mchango wa Biblia katika kukuza na kuhifadhi fasihi simulizi.

Karama (1968) anazungumzia elimu ya fasihi linganishi kuhusu Yusufu mwana wa Yakobo katika Biblia. Anasema kwamba maudhui ya maisha yake yanapatikana katika fasihi ya dunia; kuanzia hekaya za kimisri miaka 1500 kabla ya kuzaliwa kwa Kristo, kuendelea katika Biblia kwa Wayahudi; kupitia tanzia ya Hippolytos ya Euripedes kwa wagiriki; tungo za Firdaus huko Uajemi. Mwandishi anaonyesha jinsi hadithi ya mzee Kibao katika utenzi wa nabii Yusufu ilivyoathiriwa na kisa cha Yusufu. Anazungumzia maudhui ya mapenzi na wivu jinsi baba alivyompendelea mwanawe mmoja akawafanya ndugu zake kumwonea kijicho na kumuuza katika nchi ya kigeni huko Misri. Hii inaonyesha jinsi Biblia inavyochangia katika udumishaji wa fasihi simulizi yaani mwingiliano matini.

Nelson (1995) anasema kwamba wakati wote wa enzi ya ukristo usomaji na ufasiri wa Biblia ulikuwa jukumu la weledi na ilifasiriwa kulingana na desturi na imani za kanisa. Uvumbuzi wa kisayansi katika karne ya kumi na saba ulionekana kupinga sehemu fulani za Biblia. Wakati huo huo Biblia ilikuwa ikisomwa na kuhakikiwa kama vitabu vingine vya kawaida ambapo ilikuwa tisho kwa wahifadhi wa misingi ya dini ya kikristo ambao baadaye walidai kwamba kila kitu kilichomo katika Biblia ni ukweli kwani zilikuwa takatifu. Ufasihi wa Biblia wakati huu unatokana na usanii na hujaribu kuelewa habari aliyotaka kupasha mwandishi na jinsi ambavyo ingeeleweka katika mkao wa asili wa kihistoria na kitamaduni. Hii inahusisha maarifa kuhusu muundo wa mwandishi, matumizi ya lugha, historia, utamaduni na mambo kuhusu wakati na mahali ilipoandikwa. Uelewa huu ulituwezesha kuelewa jinsi Biblia na fasihi simulizi vinavyochangiana, yaani mwingiliano taaluma. Aidha, ulituwezesha kutathmini mchango wa Biblia katika ukuzaji wa fasihi simulizi.

Jamii ya Biblia za Tanzania na Kenya (1997) inaeleza kuwa waandishi wa vitabu mbalimbali vya Biblia wametumia tanzu za fasihi simulizi ambazo zinapatikana katika fasihi simulizi za kiafrika; kuna matumizi ya hadithi katika vitabu vya Biblia, matumizi ya nyimbo, mbazi, methali na vitendawili. Ujumbe unaojitokeza katika Biblia ni ule wa kufunza, kuonya, kutahadharisha na kadhalika. Sifa za wahusika katika Biblia zinashabihiana na zile za wahusika katika fasihi simulizi ya jamii mbalimbali. Jamii ya Biblia za Tanzania na Kenya (1997) imeshughulikia historia ya shujaa Fumo Liyongo na shujaa Emanuel (Yesu), taswira ya kifo chao, kufanana na kutofautiana kwao, kuonyesha kwamba Yesu ni mmoja wa wahusika wakuu katika Biblia takatifu. Utafiti huu ulitupa msingi wa kuchunguza mwingiliano matini kwa kuzingatia uhusika katika ukuzaji wa fasihi simulizi.

Magesa (2011) anasema kwamba Mwalimu Julius Nyerere wa Tanzania aliandika ushairi na nyimbo za kiroho zilizotokana na Injili ya Matayo, Mariko, Luka, Yohana na Matendo ya Mitume, kama njia ya kuendeleza Kiswahili hasa fasihi simulizi ya Kiswahili. Vilevile, alitafsiri sehemu ya Biblia takatifu katika Agano Jipya katika mtindo wa kishairi, ili kuonyesha kwamba Kiswahili kama lugha inao uwezo wa kuelezea ujumbe wa aina yoyote. Mbali na mashairi ya kidini, aliandika mashairi yenye maudhui tofauti bila kuweka bayana maudhui ya mashairi hayo na mchango wake katika fasihi ya Kiswahili. Hivyo ni bayana kuwa matini za Biblia zinasaidia katika ukuzaji wa fasihi simulizi.

Third Millennium Ministries (2012) wanaelezea jinsi Waisraeli walivyothamini hadithi kuhusu mwanzo wao. Walizipitisha hizi hadithi kutoka kizazi hadi kizazi ili kujikumbusha matukio ya zamani na mafanikio makubwa ya mababu zao pamoja na mwelekeo waliopaswa kufuata. Mojawapo ya majukumu ya fasihi simuluzi ni kuhifadhi historia. Tunapoendelea kusoma Biblia, mbali na kuhifadhi historia ya Waisraeli, tunazidi kudumisha fasihi simulizi.

### 2.5 Mapitio kuhusu Nadharia

**N**adharia ya mwingiliano matini iliasisiwa na Julia Kristeva (1969) ambaye aliizua kutokana na nadharia ya usemezano ya Mikhail Bakhtin (1968). Dhana kuu katika nadharia hii ni kuwa hakuna matini yoyote ya kifasihi inayoweza kujitegemea bila kuhusiana na matini nyingine;

kwamba watunzi hawabuni matini kutokana na fikra zao wenyewe, bali hukusanya mawazo mbalimbali kutokana na matini kati ya kazi moja ya fasihi na nyingine.

Abrams (1981) anafafanua mwingiliano matini kama njia ya ubunifu ya kuonyesha jinsi matini yoyote ile ya fasihi inavyohusishwa na matini nyingine, iwe ni kwa njia ya masimulizi ya wazi ama kufikiria, ama kwa kumezwa kwa matini ya mwanzo na matini nyingine. Miruka (2013) akiyarejelea mawazo ya Abrams alizingatia mwingiliano tanzu ambapo alichunguza maumbo mbalimbali ya fasihi simulizi na jinsi yanavyoingiliana na jinsi mengine yanavyomezwa na utanzu changamano wa ushairi andishi wa Kiswahili.

Eagleton (1983) anasema kwamba kazi zote za fasihi kwa kiwango fulani zimeandikwa tena. Hakuna usomaji wa kazi ambayo si marudio ya maandishi. Mwingiliano matini inaweza kuchukuliwa kama upanuzi wa mawazo yaliyopo ama dhana mpya kuwasilisha dhana ya zamani ambayo imepitwa na wakati. Ingemark (2005) anaeleza kwamba tanzu mbalimbali huweza kuingiliana ambapo tanzu tata humeza tanzu sahili na kuzifanya sehemu ya tanzu hizo. Kwake ulimwengu wa mwingiliano matini ni utanzu changamano ambao humeza tanzu sahili na kuzifanya sehemu ya utanzu huo changamano. Hapa matini huchukua sifa na maumbo asilia ya kitamaduni ya tanzu zingine na kubadilishwa na tanzu hizo hivyo maumbo ya matini yakiingizwa katika matini nyingine. Nadharia ya mwingiliano matini kwa jumla ilifaa utafiti huu kutokana na dhana yake kuwa hakuna matini yoyote ya kifasihi inayoweza kujisimamia bila kuhusishwa na matini nyingine. Kwa sababu hii, vitabu teule vya Biblia vilihusishwa na fasihi simulizi ili kuonyesha jinsi vinavyotegemeana kimaumbo.

Note & Jordan (2011) walitumia nadharia ya mwingiliano matini kuchunguza njia ambazo matini za Biblia hasa kitabu cha Judith, katika Biblia ya dini ya Kikatoliki, zinavyoleta maana katika hali ya kuunda matini. Hoja yao ilikuwa kwamba itikadi za waandishi wa matini huunga mkono njia ambazo matini nyingine zinatumika. Kusudi la uchunguzi wao lilikuwa kuonyesha jinsi udokezaji wa mwingiliano matini katika kitabu cha Judith unavyotumika kuelezea Mungu kama Mungu wa vita ingawa angali Mungu. Utafiti huu kwa upande mwingine haukushughulikia udokezaji wa mwingiliano matini katika kitabu fulani cha Biblia, bali ulitathmini mwingiliano matini wa maumbo ya fasihi simulizi katika vitabu teule vya Biblia.

## SURA YA TATU

## NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulizingatia muundo wa kimaelezo ambao ni sehemu ya utafti stahilifu. Mundo huu huazimia kueleza hali jinsi ilivyo. Vitabu teule vya Biblia ya Tafsiri Jipya la Kimataifa vilisomwa na maumbo ya fasihi simulizi yakadondolewa kisha maelezo yakatolewe kwa kila umbo kulingana na linavyojitokeza katika Biblia. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), muundo wa kimaeezo huhusu ukusanyaji data, uainishaji, uchanganuzi, ulinganishi na ufasiri wa data. Data ilikusanywa maktabani kwa kudurusu na kuchanganua matini za Biblia ya Tafsiri Jipya la Kimataifa kisha ikaainishwa na kupangwa kitanzu, ikalinganishwa halafu ikafasiriwa kwa kuzingatia maumbo makuu manne ya fasihi simulizi; hadithi/ masimulizi, maigizo, mashairi/ ushairi simulizi na semi/ tanzu bainifu, pamoja na vipera vyao. Matokeo yaliwasilishwa kwa maelezo kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti yakiwemo; kuchanganua maumbo ya fasihi simulizi katika matini teule katika Biblia; kupambanua mwingiliano taaluma wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia; kutathmini mchango wa Biblia katika ukuzaji wa fasihi simulizi. Mihimili ya nadharia ilitumiwa katika kuwasilisha maelezo.

### 3.2 Eneo la Utafiti

Muktadha wa utafiti huu ulikuwa vitabu sitini na sita vya Biblia ya Tafsiri Jipya la Kimataifa. Vitabu hivi vyote vilisomwa kisha vitabu saba vikateuliwa kutoka Agano la kale na Agano Jipya. Utafiti huu ulichunguza vitabu teule vya Biblia kwa kuvihusisha na maumbo ya fasihi simulizi. Vitabu vilivyotumika vilikuwa kitabu cha Mwanzo, Wafalme wa kwanza na Wafalme wa pili, Zaburi, Mithali, Mathayo na Luka. Vitabu hivi vilichaguliwa kwa sababu ya utajiri wao wa maumbo ya fasihi simulizi. Mwingiliano wa tanzu za fasihi simulizi na matini teule ya Biblia ulichunguzwa huku maumbo ya fasihi simulizi yakitiliwa maana na jinsi yalivyojitokeza katika vitabu teule vya Biblia.

### 3.3 Kundi Tafitiwa

Utafiti ulifanywa kwa kusoma, kuchunguza na kuchanganua maandishi mbalimbali ya Biblia ya Tafsiri Jipya la Kimataifa yanayohusiana na swala la utafiti. Kuna tafsiri nyingi za Biblia

takatifu. Kwa mujibu wa Zondervan Corporation (1987), Biblia ya Tafsiri Jipya la Kimataifa iliidhinishwa na idadi kubwa ya viongozi kutoka madhehebu mbali mbali na uaminifu wake kwa lugha asilia ukachunguzwa kwa hivyo ubora wa maandishi yake unafaa umma na watu binafsi. Biblia takatifu inavyo vitabu sitini na sita ambavyo vimegawika katika Agano la Kale na Agano Jipya. Agano la Kale linavyo vitabu thelathini na tisa nalo Agano Jipya vitabu ishirini na saba. Baada ya kuvipitia vitabu hivi vyote, vile vilivyobainisha maumbo ya fasihi simulizi vilichaguliwa kufanyiwa utafiti. Hivi vilikuwa, kitabu cha Mwanzo, Wafalme wa kwanza, Wafalme wa pili, Zaburi, Mithali, Mathayo na Luka mtakatifu.

### 3.4 Sampuli na usampulishaji

Huu ni mchakato au mbinu ya kuchagua kundi dogo kutoka idadi ya watu kushiriki katika utafiti (Ogula 2005). Ili kupata sampuli faafu, usampulishaji dhamirifu ulitumiwa. Aina hii ya usampulishaji hutumika ili kuteua data kwa misingi ya lengo la utafiti. Mtafiti alitumia mbinu ya kimaksudi kwa kuwa malengo yalikusudia sampuli maalum. Sampuli kimaksudi ilitumiwa kuteua vitabu vya Biblia katika Agano la Kale na Agano Jipya. Sifa zilizoongoza uteuzi wa kazi zilizochanganuliwa ni pamoja na ujidhihirishaji wa tanzu za maumbo ya fasihi simulizi, yaani hadithi, mashairi, semi na mazungumzo. Katika agano la Kale, utafiti ulichunguza kitabu cha Mwanzo ambapo ulisampulisha maumbo kama vile visasili, visakale, hekaya na mighani. Katika kitabu cha Zaburi, utafiti ulisampulisha mazungumzo, mawaidha, tashhisi, nyimbo na maghani. Katika kitabu cha Mithali mtafiti alichunguza methali, nahau, tashhisi na vitendawili. Katika Agano Jipya aliangazia kitabu cha Luka ambapo alisampulisha mazungumzo, mbazi, mawaidha na nyimbo. Hakukuwa na idadi maalum ya maumbo yaliyochunguzwa katika kila kitabu, kwa sababu hakuna sheria za idadi katika usampulishaji kimaksudi (Patton, 2002). Kutokana na sampuli hii, vifungu tisini na tatu vya Biblia vilitumika kama vielelezo vya data.

### 3.5 Ukusanyaji Data

Data ilikusanywa kwa njia ya maktaba. Mtafiti alisoma vitabu teule vya Biblia na kudondoa maumbo ya fasihi simulizi yaliyoafiki madhumuni ya utafiti huu ili kuona uwiano uliokuwepo kati ya fasihi simulizi na Biblia. Orodha ya uchunzaji ilitumika katika ukusanyaji wa data. Tanzu za fasihi simulizi ziliteuliwa na kutumika kama data.Tanzu zenyewe ziliwekwa katika kategoria nne; Hadithi/ masimulizi, maigizo, semi/ tanzu bainifu na ushairi simulizi. Utukiaji wa tanzu

hizo nne katika vitabu vyote saba vya Biblia vilivyoteuliwa ulinukuliwa katika jedwali. Maelezo ya wataalam mbalimbali kuhusu maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia yalizingatiwa huku yakihusishwa na utafiti.

**3.6 Uaminifu na Uthabiti wa vifaa vya kukusanya data**

Uaminifu ni usahihi wa matokeo yanayopatikana kwa kutumia vifaa vya utafiti waala sio vifaa vyenyewe. Kwa mujibu wa mvumbi (2015), uaminifu wa vifaa vya utafiti kisifa humwangazia mtafiti kama kifaa chenyewe.Uaminifu na uthabiti wa vifaa vya kukusanya data huchukuliwa pamoja. Uaminifu wa mtafiti kwa hivyo huhusisha kusadikika ama kuaminika, kutegemewa, uhawilishi au uhamisho na ukubalifu. Uaminifu wa vifaa vya kukusanya data vilivyotumika katika utafiti huu ulibainishwa baada ya kupitia maandishi ya awali na kusoma Biblia kwa urefu na upana.

**3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji data**

Uchanganuzi unaoshirikishwa katika utafiti huu ni uchanganuzi kisifa ambao unalenga kubaini na kuainisha kikamilifu tanzu za fasihi simulizi na vipera vyake vinavyodhihirika katika data iliyoainishwa. Maumbo ya tanzu hizi pia yanaelezwa. Data iliyokusanywa ilipangwa kulingana na maumbo jinsi yanavyojitokeza katika Biblia na kisha ikachanganuliwa kwa njia ya kusimba (msimbo) ili kurahisisha uchambuzi. Vitabu vya Biblia vilivyoteuliwa vilichanganuliwa. Vipengele vya uchanganuzi vilikuwa tanzu nne kuu za fasihi simulizi zilizoteuliwa, yaani, hadithi/ simulizi, maigizo, mashairi/ ushairi simulizi na semi/ tanzu bainifu. Tanzu hizi zilipangwa na kuainishwa kwa kutumia mada zilizozotokana na maumbo yaliyochanganuliwa. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Nadharia ya mwingiliano matini ndiyo iliyotumika katika utafiti huu. Mihimili yake mitatu iliyotumiwa ilifungamanishwa na madhumuni na swala la utafiti.

Kulingana na madhumuni ya kwanza ambayo ni kutathmini maumbo ya fasihi simulizi katika vitabu teule vya Biblia, tanzu za fasihi simulizi zimeelezwa kwa kutumia mhimili wa kwanza, kazi ya kifasihi huingiliana na kuhusiana. Kulingana na mhimili huu, matini huchukua sifa na maumbo asilia ya kitamaduni ya tanzu zingine na kuingiliana vilivyo. Madhumuni ya pili ni, kupambanua mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule ya Biblia. Hayo

yalishughulikiwa kutumia mhimili wa pili unaosema kwamba matini hupeana umatini ambamo matini nyingine zinaweza kuundwa na kufasiriwa. Madhumuni ya tatu ni kutathmini mchango wa Biblia katika ukuzaji wa fasihi simulizi. Mhimili wa tatu unaosema fasihi hutokana na fasihi ulitumika. Muundo elezi ulizingatiwa katika kueleza jinsi matini za fasihi simulizi zilivyoingiliana na zile za Biblia.

### 3.8 Maadili ya Utafiti

Maadili katika utafiti yanahusu matumizi ya kanuni adilifu katika mada mbali mbali zinazohusiana na utafiti wa Kisayansi. Kwa mujibu wa Blaxter (2001), maswala ya maadili ni ya muhimu katika utafiti kwa sababu humwezesha mtafiti kuwa mwaminifu  na mwadilifu katika kazi yake. Katika utafiti huu, idhini yabaraza la uongozi wa wa taaluma, chuo kikuu cha Maseno iliombwa na aidha, itifaki za utafiti zilizoidhinishwa na baraza hilo zilizingatiwa. Ili taarifa hasi isifanywe, taarifa ya kutosha kuhusu madailitafutwa. Vilevile, utakatifu wa Biblia ulizingatiwa kwa kuhakikisha kwamba swala la dini halichafuliwai kwa kuhusishwa na fasihi simulizi.

### 3.9 Hitimisho

Ili kuafikia njia na mbinu za utafiti, utafiti ulishughulikia muundo wa utafiti, eneo la utafiti,kundi tafitiwa, sampili na usampulishaji, ukusanyaji data na uwasilishaji data. Uaminifu na uthabiti wa vifaa vya kukusanya data pamoja na maadili ya utafiti vilevile yalishughulikiwa.

## SURA YA NNE

## UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI DATA

### 4.1 Utangulizi.

Tanzu mbalimbali za fasihi simulizi zinazozipatikana katika vitabu teule vya Biblia zimeshughulikiwa katika sura hii. Vipengele vyenyewe vimejadiliwa kwa misingi ya masimulizi/ hadithi, maigizo, semi/ tanzu bainifu na mashairi/ ushairi simulizi. Sura hii inazingatia madhumuni yafuatayo: kuchanganua vipengee vya fasihi simulizi vinavyopatikana katika Biblia; kupambanua mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia; kutathmini mchango wa Biblia katika ukuzaji wa fasihi simulizi. Data iliyochanganuliwa ilitokana na maumbo ya fasihi simulizi yaliyopatikana katika vitabu vya Biblia vilivyoteuliwa.

### 4.2 Maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia.

Maumbo ya fasihi simulizi yanayopatikana katika Biblia yamejadiliwa katika sehemu hii. Hii imeongozwa na mhimili wa nadharia unaoonyesha kwamba matini huchukua sifa na maumbo asilia ya kitamaduni na tanzu zingine na kubadilishwa na tanzu hizo.Kama tulivyoeleza hapo awali, umbo ni utanzu, mgao au kundi la vipengele vya fasihi vilivyowekwa pamoja kwa sababu ya uwiano wake kimtindo, kiuwasilishaji, kimaudhui au kimuundo (Finnegan, 1970). Tanzu za fasihi simulizi zinazopatikana katika Biblia zimejadiliwa katika sehemu hii. Mifano ya tanzu hizo ni pamoja na hadithi, maigizo, semi/tanzu bainifu na ushairi simulizi, pamoja na vipera vyao. Ni vyema kuelewa kwamba tanzu ni istilahi inayotumiwa kuelezea au kurejelea aina ya kazi mbalimbali za kifasihi. Inawezekana utanzu mkuu kuwa na vitanzu/ vipera mbalimbali (Wamitila, 2003).

Hadithi/ Simulizi inayo vipera mbalimbali vikiwemo visasili, visakale/ hekaya, hurafa, mighani na mbazi. Maigizo yanayo vipera kama vile mazungumzo, mawaidha, miviga, michezo ya kuigiza na ngonjera. Semi/ tanzu bainifu zina vipera kama methali, vitendwaili, nahau tashhisi, tashbihi na takriri. Ushairi simulizi ni pamoja na nyimbo na maghani.

#### 4.2.1 Hadithi/ Simulizi

Baada ya data kukusanywa na kuchanganuliwa vilivyo, umbo la hadithi liliweza kubainika

waziwazi pamoja na vipera vyake. Wamitila (2003) anaeleza hadithi kama utungo wenye visa vya kubuni unaosimuliwa kwa lugha nathari kwa kusudi la kuburudisha, kukuza maadili na kuunganisha jamii. Naye Matei (2011) anafafanua hadithi kama masimulizi yanayowasilishwa kwa lugha ya nathari kuhusu watu, matukio na mahali mbali mbali. Baadhi ya vipera vya hadithi vilivyodhihirika katika utafiti huu ni pamoja na visasili, visakale/ hekaya, mighani na mbazi. Hurafa hazikudhihirika sana kama hivi vipera vingine.

**4.2.1.1 Visasili**

Kwa mujibu wa wamitila (2003), visasili hueleza asili au chanzo cha kitu. Huweza kueleza asili ya vitu mbalimbali katika jamii fulani. Huweza pia kueleza asili ya ulimwengu pamoja na mwenendo wake, msingi wa mtazamo na imani za jamii fulani, asili ya matendo au hali kama kifo, asili ya matukio fulani na wasifu fulani wa kimaumbile. Msambao wa kitamaduni unasabibisha baadhi ya sifa za visasili vya jamii fulani kuenea na kuingiliana na visasili vya jamii nyingine kiasi kwamba panakuwepo mfanano fulani katika muundo wa visasili vyenyewe. Kumeonekana mwingiliano wa visasili vya fasihi simulizi ya Kiafrika na vile vya Biblia.

Matteru (1987) anaeleza kwamba visasili ni hadithi ambazo pamoja na kuwa na wahusika wa aina tofauti hasa miungu na binadamu, husimulia matukio ya kiada kama jina la utanzu huu lilivyo, visasili ni visa vya mianzo. Hushughulikia mianzo ya matendo yaliyozowewa kama unyago, ndoa, kifo na imani mbalimbali. Hivi visasili vimejitokeza katika vitabu teule vya Biblia vilivyosomwa.

Miruka (2013) anaeleza sifa za visasili zikiwemo: hueleza chimbuko la jamii fulani; aghalabu huhusisha miungu, jamii fulani, mila, imani na matukio ya kiada kama vile kifo na tohara; matokeo yake hufanyika mwanzoni kama vile mwanzo wa dunia; huhifadhi historian a imani ya jamii huku zikiunganisha wanajamii. Kuna mifano mingi ya visasili katika Biblia ikiwemo;
Mwanzo 3:1-6, 17-19.
“Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote na mwitu aliowafanya BWANA Mungu, akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile matunda ya miti yote ya bust

**Kisasili kuhusu asili ya kifo ulimwenguni**

Mwanzo 3:6, 17- 19

"Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA Mungu, akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwananamke akamwambia nyoka, matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya, Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yale akala, akampa na mumewe, naye akala. Wakafumbuliwa macho wale wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo. Kisha wakamsikia Bwana Mungu akitembea bustanini wakati wa jua kupunga. Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone. Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, uko wapi? Akamwambia, nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi, nikajificha. Akasema, ni nani aliyekuambia kuwa u uchi? Je, umekula matunda niliyokuagiza usiyale? Adamu akasema, huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja name ndiye aliyenipa matunda ya mti huo nikala. Bwana Mungu akamwambia mwanamke, nini hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, nyoka alinidanganya nikala. Bwana Mungu akamwambia nyoka, kwa sababu umefanya hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko hayawani wote walioko mwituni. Kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako; name nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake, huo atakuponda kichwa, nawe utamponda kisigino. Akamwambia mwanamke, hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa uchungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo,naye atakutawala. Akamwambia Adamu, kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, usiyale: ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yako siku zote za maisha yako. Akamwambia Adamu, kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nilikuagiza usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako

utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi"

Hadithi hii inatueleza jinsi nyoka alivyomdanganya Hawa hata akala tunda kutoka kwa mti waliokuwa wamekatazwa na Mungu wasile. Baada ya kula alimpa Adamu mumewe pia akala, wakawa wamekiuka amri ya Mungu. Adamu ambaye alikuwa kichwa cha nyumba alikuwa ameelezewa na Mungu cha kufanya. Badala yake alimsikiza Hawa mkewe ambaye alikuwa amedanganywa na nyoka. Mungu alikasirika nao kisha akawaadhibu kila mmoja wao; akawaambia *mchangani mlitoka, na mchangani mtarudi*, na hivyo ndivyo kifo kilivyoingia duniani. Jinsi asemavyo Wamitila (2003), hadithi huwa na ufundi wa kisanaa ambao hujitokeza kwa lugha ya mvuto na iliyochanganya tamathali mbalimbali za usemi, tunaona mwingiliano tanzu wa fasihi simulizi ambapo mafumbo yanatumika katika hadithi, *mchangani mlitoka na mchangani mtarudi,* kuonyesha kwamba binadamu aliumbwa kutoka kwa mchanga na akifa, atazikwa mie mie mchangani. Wahusika katika kisasili hiki walikuwa binadamu pamoja na mnyama, yaani Adamu na Hawa, pamoja na nyoka, jinsi ilivyo kawaida katika fasihi simulizi (Wamitila, 2003). Aidha, ilivyo kawaida ya viishio katika hadithi, kisasili hiki kimeishia kwa kauli, na kutoka huko BWANA akawatawanya waende usoni pa nchi yote. Hii inadhihirisha mwingiliano wa tanzu za fasihi simulizi na zile za matini ya Biblia kwa mujibu wa Allen (2000), kwamba kazi za fasihi zimejengwa kutokana na mifumo, kanuni na taratibu zilizokubaliwa na jamii na tamaduni zilizojengwa na kazi za zamani za fasihi.

**Kisasili kuhusu asili ya lugha nyingi duniani**

Mwanzo 11:1-9.

> "Nchi yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja. Ikawa watu waliposafiri pande za mashariki waliona nchi tambarare katika nchi ya Shinari; wakakaa huko. Wakaambiana, Haya, na tufanye matofali tukayachome moto. Walikuwa na matofali badala yam awe, na lamii badala ya chokaa. Wakasema, Haya, na tujijengee mji, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni, tujifanyie jina; ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi yote. BWANA akashuka ili auone mji na mnara waliokuwa wakiujenga wanadamu. BWANA akasema, Tazama, watu hawa ni taifa moja, na lugha yao ni moja; naa haya ndiyo wanayoanza kuyafanya, wala sasa hawatazuiliwa neno wanalokusudia kulifanya. Haya, na tushuke

huko, tuwachafulie usemi wao ili wasikilizane maneno wao kwa wao. Basi BWANA akawatawanya kutoka huko waende usoni pa nchi yote; wakaacha kuujenga ule mji. Kwa sababu hiyo jina lake likaitwa Babeli; maana hapo ndipo BWANA alipoichafua lugha ya dunia yote; na kutoka huko BWANA akawatawanya waende usoni pa nchi yote."

Kisasili hiki kinatuonyesha jinsi lugha nyingi zilivyoingia duniani. Tamaa ya binadamu kutaka kumfikia Mungu na kutawanyika ulimwenguni kote kulimfanya Mungu akakasirika nao hata akawachafulia usemi wao kisha akawatawanya ulimwenguni kote. Hii tamaa ya kutaka kujifanyia jina ili wawe kama Mungu ndiyo iliyosababisha lugha nyingi duniani kwani walijikuta kila mmoja wao akisema lugha tofauti na wakakosa kuelewana. Ijulikane kwamba aina ya wahusika hudhihirisha umbo la kipengee husika. Katika visasili vya kidini, wahusika wakuu ni Mungu ama miungu, ambao wanajitokeza katika kisasili hiki.

Mulokozi (1989) anaeleza kwamba visasili ni hadithi za kale zenye kuwasilisha imani na mtazamo wa jamii inayohusika kuhusu asili ya ulimwengu na mwenendo wake, kuhusu asili yao wenyewe, na maana na shabaha ya maisha yao. Mara nyingi hadithi hizi huaminika kuwa ukweli mtupu na hutumika kuelezea au kuhalalisha baadhi ya mila na madhehebu ya jamii inayohusika. Ilivyo kawaida ya viishio katika hadithi, kisasili hiki kimeishia kwa kauli, *na kutoka huko……*

#### 4.2.1.2 Hekaya

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) hekaya ni ngano ambazo huhusisha mhusika mmoja ambaye anajifanya rafiki huku akiwa na dhamira ya kujinufaisha yeye mwenyewe. Ni ngano ambapo mhusika mmoja hutumia hila au ujanja kujinufaisha kutoka kwa mhusika mwingine anayedanganyika kwa wepesi, japo hastahili. Ipara na Waititu (2004) wanafafanua hekaya kama ngano fupi zinazosimulia matukio ya kustaajabisha na yanayoonyesha hila au ujanja wa mwanadamu. Hekaya huonya dhidi ya upumbavu na pia hutoa maadili kwa wanajamii ili waache kuwatendea wenzao ujanja. Kipera cha hekaya kimejitokeza mara nyingi katika vitabu tulivyovisoma. Baadhi yazo ni kama zifuatazo.

**Hekaya ya Yakobo kuchukua baraka za Esau**

Mwanzo 27:18-29.

> "Akaja kwa baba yake, akasema, Babangu. Akasema, mimi hapa, U nani wewe, mwanangu? Yakobo akamwambia babaye, Mimi ni Esau, mzaliwa wako wa kwanza, nimefanya kama ulivyoniambia. Ondoka, tafadhali, ukae kitako, ule mawindo yangu, ili roho yako inibariki. Isaka akamwuliza mwanawe, imekuwaje umepata upesi namna hii, mwanangu? Akasema, kwa sababu BWANA, Mungu wako, amenifanikisha. Isaka akamwambia Yakobo, karibu, tafadhali, ili nikupapase, mwanangu, nione kwamba wewe ndiwe mwanangu Esau, ama siyo. Basi Yakobo akamkaribia Isaka, babaye, naye akampapasa, akasema, sauti ni sauti ya Yakobo, lakini mikono ni mikono ya Esau. Wala hakumtambua, kwa maana mikono yake ilikuwa kama mikono ya Esau, ndugu yake, yenye malaika; basi akambariki. Akamwuliza, wewe ndiwe kweli mwanangu Esau? Akasema, ndimi. Akasema, Niletee karibu nami nipate kula mawindo ya mwanangu, ili roho yangu ikubariki. Akamsogezea karibu, naye akala; kisha akamletea mvinyo, akanywa. Isaka, baba yake, akamwambia, Njoo karibu sasa, ukanibusu, mwanangu. Akamkaribia akambusu. Naye akasikia harufu ya mavazi yake, akambariki akasema, tazama, harufu ya mwanangu ni kama harufu ya shamba alilolibariki Bwana. Mungu na akupe ya umande wa Mbingu, na ya manono ya nchi, na wingi wa nafaka na mvinyo. Mataifa na wakutumikie na makabila wakusujudie, uwe bwana wa ndugu zako, na wana wa mama yako na wakusujudie. Atakayekulaani alaaniwe, na atakayekubariki abarikiwe."

Hapa Yakobo ni mhusika ayari ambaye anamdanganya babake kisha baadaye anachukua baraka za nduguye kutoka kwake. Mamake alimsikia baba akipanga na Esau jinsi ambavyo angembariki na akapanga njama na Yakobo wakamhadaa baba yao hata akachukua baraka za nduguye. Babake anadanganyika kwa wepesi na kumpa Yakobo baraka zake zote ambapo anajuta mwanawe mkubwa anapofika na kupata hakuna baraka zozote kwake. Jambo hili linasababisha mzozano kati ya Esau na Yakobo na baadaye Yakobo analazimika kutoroka nyumbani. Kwa kudanganyika kwa wepesi, Isaka alisababisha mafarakano katika nyumba yake. Vilevile, Yakobo alipokea baraka za babake ingawa hakustahili. Mojawapo wa sifa za hekaya ni ngano ambapo mhusika mmoja hutumia hila au ujanja kujinufaisha kutoka kwa mhusika mwingine, alivyofanya

Yakobo. Nadharia ya mwingiliano matini inajitokeza hapa ambapo Kristeva (1978) anaeleza kwamba matini si kitu binafsi ila ni mkusanyiko wa matini za kitamaduni.

**Hekaya ya Yakobo kuoa Lea badala ya Raheli**

Mwanzo 29:16-27.

> " Labani alikuwa na binti wawili, jina la mkubwa ni Lea, na jina la mdogo ni Raheli. Naye Lea macho yake yalikuwa dhaifu, lakini Raheli alikuwa mzuri wa umbo, na mzuri uso. Yakobo akampenda Raheli akasema, nitakutumikia miaka saba kwa kumpata Raheli, binti yako mdogo. Labani akasema, afadhali nikupe wewe kuliko mtu mwingine; kaa kwangu. Yakobo akatumika miaka saba kwa kumpata Raheli. Ikawa machoni pake kama siku chache tu kwa vile alivyompenda. Yakobo akamwambia Labani, nipe mke wangu, maana siku zangu zimetimia; niingie kwake. Labani akakusanya watu wote wa mahali pale, akafanya karamu. Ikawa wakati wa jioni akamtwaa Lea, binti yake, akamletea Yakobo naye akaingia kwake. Labani akampa Lea mjakazi wake Zilpa, awe mjakazi wake. Ikawa, kulipokuwa asubuhi, kumbe! Ni Lea. Akamwambia Labani, nini hii uliyonitenda? Sikukutumikia kwa Raheli? Mbona umenidanganya? Labani akasema, havitendeki hivi kwetu, kumtoa mdogo kabla ya mkubwa, timiza siku zake saba, nasi tutakupa huyu naye kwa utumishi utakaonitumikia, miaka saba mingine."

Katika hekaya hii, Labani ni mhusika ayari kwani anamdanganya Yakobo amfanyie kazi kwa miaka saba kisha amwoze Raheli aliyempenda. Baada ya miaka saba, Yakobo anapewa Lea ambaye hakumpenda na vilevile alikuwa chongo. Labani alijua kwamba Lea alikuwa kifungua mimba wake na ili aweze kuolewa mbele ya dadake aliyekuwa mdogo wake, ilibidi atumie hila. Huu ni mfano mzuri wa hekaya kwani Labani anajinufaisha kutoka kwa Yakobo kwa kutumia hila.

**Hekaya yaYusufu kuuzwa na ndugu zake**

Mwanzo 37:13-36.

> "Israeli akamwambia Yusufu, Je! Ndugu zako hawachungi kondoo katika Shekemu? Njoo, nikutume kwao. Akamwambia, Mimi Hapa. Akamwambia, enenda, basi ukaone kama ndugu zako hawajambo, na kundi nalo li salama,

ukaniletee habari. Basi akampeleka kutoka bonde la Hebroni, akafika Shekemu. Mtu mmoja akamkuta, naye alikuwa anazunguka zunguka katika nyika; Yule mtu akamwuliza, akisema, unatafuta nini? Akasema, Nawatafuta ndugu zangu; tafadhali uniambie mahali wanakochunga. Yule mtu akasema, wametoka hapa, maana niliwasikia wakisema, twendeni Dothani. Basi Yusufu akawafuata ndugu zake akawakuta huko Dothani. Wakamwona toka mbali, na kabla hajawakaribia, wakafanya shauri juu yake ili wamwue. Wakasemezana wao kwa wao, tazama, yule bwana wa ndoto anakuja. Haya, twende, tukamwue na kumtupa katika birika mojawapo, nasi tutasema, mnyama mkali amemla; kisha tutaona zitakuwaje ndoto zake".

Rubeni akasikia akamwokoa katika mikono yao, akasema, tusimwue. Rubeni akawaambia, msimwage damu, mtupeni katika birika hii iliyopo nyikani, wala msimguse, ili apate kumwokoa katika mikono yao, akamrudishe kwa baba yake. Ikawa Yusufu alipofika kwa ndugu zake, wakamvua Yusufu kanzu yake, kanzu ile ndefu aliyoivaa, wakamtwaa wakamtupa katika birika hii iliyopo nyikani, wala msimguse, ili apate kumwokoa katika mikono yao akamrudishe kwa baba yake. Ikawa Yusufu alipofika kwa ndugu zake, wakamvua Yusufu kanzu yake, kanzu ile ndefu aliyoivaa, wakamtwaa wakamtupa katika birika, na hiyo birika ilikuwa tupu, hamna maji. Nao wakakaa kitako kula chakula, wakainua macho yao, wakona, msafara wa waishmaeli wanakuja wakitoka Gileadi na ngamia zao, wakichukua ubani na zeri na manemane, wakisafir kuvichukua mpaka Misri. Yuda akawaambia ndugu zake, kwafaa nini kumwua ndugu yetu, na kuificha damu yake haya na tumwuze kwa hawa waishmaeli, wala mikono yetu isimdhuru, maana yeye ni ndugu yetu, na damu yetu. Ndugu zake wakakubali. Wakapita wafanya biashara wamidiani basi wakamtoa Yusufu, wakampandisha kumtoa katika birika, wakamwuza Yusufu kwa Waishmaeli kwa vipande vya fedha ishirini; nao wakamchukua Yusufu mpaka Misri".

"Akarudi Rubeni birikani, kumbe! Yusufu hayumo katika birika, akararua nguo zake. Akarudi kwa ndugu zake, akasema, mtoto hayuko, nami niende

> wapi? Wakaitwaa kanzu ya Yusufu, wakchinja mwana-mbuzi, na kuichovya kanzu katika damu. Wakaenda nayo ile kanzu ndefu, wakamletea baba yao, wakasema, tumeona hii basi, utambue kama kanzu hii ni ya mwanao, ama siyo. Akaitambua, akasema, ndiyo kanzu ya mwanangu, mnyama mkali amemla bila shaka Yusufu ameraruliwa. Yakobo akararua mavazi yake, akajivika gunia viunoni, na kumlilia mwanawe siku nyingi. Wanawe wote, na binti zake wote, wakaodoka wamtulize, lakini akakataa kutulizwa. Akasema , la! Nitamshukia mwanagu, nikisikitika, hata kuzimu. Baba yake akamlilia. Nao wamidiani wakamwuza huko Misri, kwa Potifa, akida wa Farao, Mkuu wa askari".

Ndugu zake Yusufu walitumia ujanja kwa baba yao walipomuuza ndugu yao na kumdanganya baba yao kuwa ameliwa na mnyama mbaya. Baada ya kumuuza Yusufu walipelekea baba yao koti lililojaa damu ili kumhadaa kuwa Yusufu alikuwa ameliwa na mnyama wa mwitu. Wivu wao dhidi ya Yusufu kupendwa na baba yao uliwafanya wakapanga njama ya kumtendea mabaya kwa kumuuza, kasha wakachinja mwana mbuzi na kulichovya kanzu la Yusufu katika damu kasha wakampelekea baba yao huku wakimdanganya eti mwanawe mpendwa alikuwa ameaga dunia. Baba yao aliamini ujanja wao hata akararua mavazi yake, akajivika guniakiunoni na kumlilia mwanawe. Hii hekaya inathibitisha nadharia ya mwingiliano matini kama alivyosema Kristeva kwamba matini huchukua sifa na maumbo asilia ya kitamaduni. Utamaduni wa Kiyahudi unaonekana kushabihiana na utamaduni wa Kiafrika.

**Hekaya ya bibi wa Yereboam kutumia udanganyifu ili nabii Ahiya amponye mwanawe**

1Wafalme 14:1-5.

> "Siku zile akaugua Abiya, mwana wa Yeroboamu. Yeroboamu akamwambia mkewe, ondoka, tafadhali, ujibadilishe, wasikujue kuwa mkewe Yeroboamu; ukaenda Shilo; tazama, yuko huko Ahiya nabii, aliyeninena mimi ya kwamba nitakuwa mfalme juu ya watu hawa. Twaa mkononi mikate kumi, na kaki, na mtungi wa asali, ukamwendee, naye atakuambia kijana atakuwaje. Akafanya hivi mkewe Yeroboamu, akaondoka, akaenda Shilo, akaja nyumbani kwa Ahiya. Basi Ahiya hakuweza kuona, kwa kuwa macho yake yamepofuka kwa sababu ya uzee wake. Bwana akamwambia Ahiya, Angalia mkewe Yeroboamu anakuja akuulize mambo ya mwanawe, kwa hawezi, hivi na hivi umwambie, kwani itakuwa akiingia atajifanya kuwa mwanamke mwingine."

Bibi wa Yeroboam alijaribu kutumia udanganyifu kwa nabii Ahiya ili akamponye mwanawe. Kwa kuwa nabii Ahiya alikuwa amepofuka kutokana na uzee, Yeroboam alifikiri kwamba hangemtambua mkewe kwa hivyoangemponya tu mwanawe. Hila ziligunduliwa kwani Mungu mwenyewe alimfunulia nabii Ahiya hila zao na hivyo hawakufanikiwa katika ujanja wao. Hila hapa ni thibitisho la kisa chenyewe kuwa hekaya huku bibi wa Yeroboam akijitokeza kama mhusika ayari.

**Hekaya ya Elisha kuwahadaa washamu**

2 Wafalme 6:1-7.

> "Na walipomtelemkia Elisha akamwomba Bwana akasema, uwapige, nakusihi,
> watu hawa kwa upofu. Akawapiga na upofu sawasawa na neno la Elisha.
> Elisha akawaambia, njia hii siyo, na mji huu sio. Nifuateni mimi, nami nitawapeleka kwa mtu Yule mnayemtafuta. Akawapeleka Samaria. Hata walipokwisha ingia Samaria, Elisha akasema, Bwana, wafumbue macho watu hawa, wapate kuona. Bwana akawafumbua macho wakaona. Kumbe! Walikuwa katikati yaSamaria."

Hapa Elisha ni mhusika ayari ingawa yeye ni nabii. Aliwahadaa washamu ya kwamba anawaonyesha njia ya kwenda kwa mtu waliyekuwa wakimtafuta (yeye Elisha), kumbe alikuwa akiwapeleka Samaria katikati ya adui zao waisraeli. Walipofika huko wakafumbuliwa macho, walishtuka. Elisha aliwahadaa ili waweze kuona nguvu na uwezo wa mungu aliokuwa nao.

Kulingana na hizi hekaya, tunapata kwamba udanganyifu unazo athari mbalimbali zikiwemo; kuwaokoa wanaodhulumiwa kwa kutumia uwezo mkubwa wa kiakili wa mhusika, jinsi alivyofanya nabii Elisha ili kuwaokoa wana wa Israeli; katika ulimwengu uliojaa hila na shaka, silaha ya maisha ni maarifa, jinsi alivyotumia maarifa Labani hata akafaulu kumwoza mwanawe Lea kwa Yakobo, ambaye pengine hangepata mwanamme wa kumuoa; kutoa maadili kwa wanajamii ili waache kuwatendea wenzao ujanja, jinsi alivyofanya Yakobo- alimhadaa babake akazichukua baraka za nduguye Esau, naye baadaye akahadaiwa na mjombake kwa kupewa mwanamke asiyempenda. Ukimtendea mwenzako mabaya, nawe pia utatendewa vivyo hivyo. Aidha, hekaya huonya juu ya upumbavu. Bibi wa Yeroboamu alionekana mpumbavu alipotumia hila kwa nabii Ahiya ili amponye mwanawe. Ujanja wake ulitambuliwa wala hakusaidika jinsi alivyotarajia.

#### 4.2.1.3 Mighani/ Visakale

Mighani, kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999) ni aina ya hadithi ambazo huzunguka kwenye matendo ya mashujaa au majagina wa jamii fulani. Kimuundo, hadithi za aina hii huchanganya historia na chuku ya kifasihi kiasi kwamba ule ukweli wa kihistoria unaelekea kufunikwa na sifa za kifasihi. Si ajabu hadithi za aina hii kuwa na sifa za kifantasia, kuwako kwa matendo ya ukiamaumbile na miujiza ya ajabu. Ipara na Waititu (2004) wanafafanua mighani kuwa hadithi za mashujaa. Wanaendelea kusema kwamba mashujaa hawauliki kwa urahisi maana silaha za kawaida haziwadhuru. Aidha, hupigana na watu wengi na kuwashinda. Kulingana nao, majagina huwa na maumbile makubwa kuliko ya kawaida. Si kweli kusema hivyo kwani kunao majagina wengine jinsi tutakavyoona ambao maumbile yao ni ya kawaida ingawa wanatenda mambo ya kishujaa. Katika vitabu teule tulivyosoma, mighani imejitokeza mara nyingi.

**Mighani ya Yakobo kushindana na Mungu**

Mwanzo 32:24-29.

> “Yakobo akakaa peke yake, na mtu mmoja akashindana naye mweleka hata alfajiri. Naye alipoona ya kuwa hamshindi, alimgusa panapo uvungu wa paja lake, ukateguka uvungu wa paja la Yakobo alipokuwa akishindana naye. Akasema, niache, niende, maana kunapambazuka. Akasema, sikuachi, usiponibariki. Akamwuliza, jina lako ni nani? Akasema Yakobo. Akamwambia, jina lako hutaitwa tena Yakobo, ila Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu, nawe umeshinda. Yakobo akamwuliza, akasema, niambie, tafadhali, jina lako? Akasema, kwa nini waniuliza jina langu? Akambariki huko”.

Kwa kawaida tunajua kwamba Mungu si kiumbe aonekanaye kwa macho wala hashikiki kwa mikono kwani ni roho. Lakini hapa tunamwona Yakobo akishindana na Mungu kwa kupigana naye miereka mpaka akashinda. Tunafahamu kwamba Mungu ni mwenye nguvu zaidi ya viumbe wote duniani, na jinsi Yakobo alivyomshinda hata akaamua kumtegua paja lake haieleweki lakini ni kawaida ya mighani kuchanganya historia na chuku. Yakobo alijua ya kwamba alihitaji baraka za Mungu ili aweze kufanikiwa maishani hasa baada ya kumhadaa babake na kuchukua baraka za nduguye. Hiki ni kitendo kisicho cha kawaida na ni dhahiri kwamba ni kisakale.

**Mighani ya Eliya na manabii wa Baal**

1Wafalme 18:36-40.

> “Ikawa,wakati wa kutoa dhabihu ya jioni, Eliya nabii akakaribia, akasema, Ee BWANA, Mungu wa Ibrahimu, na wa Isaka, na wa Israeli, na ijulikane leo ya kuwa wewe ndiwe Mungu katika Israeli, na ya kuwa nimefanya mambo haya yote kwa neno lako. Unisikie, Ee BWANA, unisikie, ili watu hawa wajue ye kuwa wewe, BWANA, ndiwe Mungu, na ya kuwa wewe umewageuza moyo wakurudie. Ndipo moto wa BWANA ukashuka, ukaiteketeza sadaka ya kuteketezwa, na kuni, na mawe, na mavumbi, ukayaramba yale maji yailiyokuwamo katika mfereji na watu wote walipoona, wakaanguka kifudifudi, wakasema, BWANA ndiye Mungu, BWANA ndiye Mungu. Eliya akawaambia, wakamateni hao manabii wa Baali, asiokoke hata mmoja. Wakawakamata, na Eliya akawachukua mpaka kijito cha Kishoni, akawaua huko.”

Visakale huhusu mambo ya kiuwazaji ambayo labda hayawezekani kufanyika. Eliya mtu mmoja anapambana na manabii mia tano wa Baal. Baada ya wao kuomba Mungu wao na kukosa jibu kutoka kwake, Eliya anamwomba Mungu wake anayejibu kwa moto, kisha baadaye tunamwona Eliya mtu mmoja akiwaongoza mpaka kijito cha Kishoni na kuwaua manabii hao wote. Jambo kama hili haliwezekani katika maisha yetu ya kawaida, yaani Eliya kuwaua watu hawa wote pekee yake. Hapa Eliya amejitokeza kuwa jagina kwani anapigana na watu wengi na kuwashinda jinsi ilivyo mojawapo ya sifa za mighani. Aidha, aliwakomboa wana wa Israeli kutoka kuabudu miungu mingine ambayo walikuwa wamekatazwa na Mungu wao, hasa kuabudu Baal.

**Mighani ya Eliya kuchukuliwa mbinguni kwa upepo wa kisulisuli**

2Wafalme 2:1-18.

> “Ikawa hapo BWANA alipopenda kumpandisha Eliya mbinguni kwa upepo wa kisulisui, Eliya alitoka Gilgali pamoja na Elisha. Eliya akamwambia Elisha, Tafadhali, kaa hapa; maana BWANA amenituma niende mpaka Betheli. Elisha akasema, Kama BWANA aishivyo, na roho yako iishivyo, sitakuacha, Basi wakashuka mpaka Betheli. Hata ikawa, walipokwisha kuvuka, Eliya akamwambia Elisha, omba kwangu lolote utakalo nikutendee, kabla sijaondolewa kwako. Elisha akasema, Nakuomba, sehemu maradufu ya roho yako na iwe juu yangu. Akasema, umeomba neno gumu; lakini, ukiniona nitakapoondolewa kwako, utalipata; la hukuniona, hulipati. Ikawa, walipokuwa

> wakiendelea mbele na kuongea, tazama! Kukatokea gari la moto, na farasi wa moto, likawatenga wale wawili, naye Eliya akapanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli."

Kama anavyosema mulokozi (1989) visakale ni masimulizi ya kimapokeo juu ya wahenga na mashujaa wa kabila au taifa yenye kuchanganya chuku na historia. Kwa mujibu wa Biblia, ili yeyote aweze kwenda mbinguni, lazima afe kwanza. Kisakale hiki kinatufahamisha kwamba Eliya alienda mbinguni kwa kuchukuliwa na upepo wa kisulisuli, bila kuona kifo. Eliya hakufa kwa sababu ya kuwa mtiifu na mwaminifu kwa Mungu na kutenda kulingana na amri zake Mungu. Hapo Eliya anaonekana kuwa shujaa asiyefuata njia ya kawaida waipitiao watu wote ili kwenda mbinguni. Kama asemavyo Bediako (2001), maandishi matakatifu ni kumbukumbu ya ahadi ya Mungu na utamaduni; kwamba Biblia ingawa ni kitabu kitakatifu cha dini ya Kikristo, misingi yake mikuu ni tamaduni za Wayahudi kwa hivyo hii ni mojawapo ya visakale vya Kiyahudi.

**Mighani yaYona kukaa tumboni mwa samaki kwa siku tatu**

Mathayo 12:38-41.

> "Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako. Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara, ila ishara ya nabii Yona. Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi. Watu wa Nineve watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona."

Yona kumezwa na samaki na kukaa tumboni mwa samaki mwenyewe kwa siku tatu ni jambo la ajabu. Ajabu zaidi ni kwamba samaki alimpeleka hadi Nineve na kumtema huko bila kumwathiri kwa vyovyote vile. Mwishowe tunamwona Yona akienda kuhubiri Nineve ambako alikuwa ameogopa kwenda mwanzoni. Hatuwezi kumtoroka Mungu. Akiamua anataka tufanye jambo fulani, lazima tulitekeleze jinsi alivyomfanyia Yona hata akafika nineve bila kutarajia. Huu ni mfano mzuri wa kisakale katika Biblia kwani kisa chenyewe ni cha ajabu kwa sababu ya matendo yake kuwa ya ukiamaumbile na miujiza ya ajabu (Njogu na Chimera 1999).

**Mighani ya Yesu kuwalisha watu 5000 kwa samaki wawili na mikate mitano**

Luka 9:10-17.

> “ Basi wale mitume waliporudi walimweleza mambo yote waliyoyatenda; akawachukua, akaenda nao faraghani mpaka mji mmoja uitwao Bethsaida. Na makutano walipojua walimfuata; akawakaribisha, akawa akisema nao habari za ufalme wa Mungu, akawaponya wale wenye haja ya kuponywa. Na jua likaanza kushuka; wakamwendea wale Thenashara, wakamwambia, Uage mkutano, ili waende katika vijiji na mashamba ya kandokando wapate mahali pa kulala na vyakula, maana hapa tulipo ni nyika tupu. Akawaambia, Wapeni nyinyi chakula. Wakasema, Hatuna kitu zaidi ya mikate mitano na samaki wawili, tusipokwenda tukawanunulie watu hawa wote vyakula. Kwa kuwa wanaume waliokuwako walipata kama elfu tano. Akawaambia wanafunzi wake, Waketisheni watu kwa safu, kila safu watu hamsini. Wakafanya hivyo, wakawaketisha wote. Akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni akavibariki, akavimega, akawapa wanafunzi wake ili wawaandikie mkutano. Wakala, wakashiba wote; na katika vile vipande vilivyowabakia walikusanya vikapu kumi na viwili.”

Hii ni hadithi iliyoongezwa chuku kwa hali ya juu kwani mikate mitano na samaki wawili hawawezi kujaza hata zaidi ya vikapu viwili. Hapa tunaona wanaume elfu tano mbali na wanawake na watoto wakila na kushinda na hata kubakisha kiasi hicho. Yesu hapa ni shujaa anayetenda miujiza isiyo ya kawaida.

**Mighani ya Yesu kutuliza tufani**

**Luka 8:22-24.**

> **“**Ikawa siku zile mojawapo alipanda chomboni yeye na wanafunzi wake, akawaambia, Na tuvuke mpaka ng’ambo ya ziwa. Wakatweka matanga. Nao walipokuwa wakienda, alilala usingizi. Ikashuka tufani juu ya ziwa, chombo kikaanza kujaa maji, wakawa katika hatari. Wakamwendea, wakamwamsha, wakisema, Bwana mkubwa, Bwana mkubwa, tunaangamia. Akaamka,akaukemea upepo lakini akawakataza wasimwambie mtu lililotukia.”

Si kawaida kwa binadamu kutawala maumbile. Bila shaka Yesu amechorwa kama mhusika aliye na nguvu za ukiamaumbile ambapo anaweza kukemea hata tufani na inamsikiza na kumtii. Haya ni matendo ya ajabu kwani mojawapo ya sifa za majagina ni kupigania haki za wanyonge ambapo wao wenyewe hawauliki kwa urahisi kwani silaha za kawaida haziwadhuru; hata tufani juu ya ziwa haikuwa na mamlaka juu ya Yesu.

#### 4.2.1.4 Mbazi

Wamitila (2003) anafafanua mbazi kama aina ya hadithi za kimafumbo ambazo huwa na mafunzo kwa hadhira. Kimsingi hadithi za aina hii hutolewa kama kielelezo hasa wakati wa maongezi au mazungumzo na hukusudiwa kumkanya, kumwelekeza, kumuadhibu au hata kumfunza anayesikiliza. Mtambaji huwa anataka hadhira yake ijifunze kutokana na hali au masaibu yaliyowafika wahusika wa hadithi hiyo.

Mifano ya mbazi inayopatikana katika Biblia ni pamoja na mbazi ya mpanzi, mbazi ya magugu, mbazi ya juya, mbazi ya mkubwa katika ufalme wa Mbingu, kondoo aliyepotea, mtumwa asiye na msamaha, kijana tajiri, wafanyakazi katika shamba la mizabibu, wanawali kumi, talanta, msamaria mwema, tajiri mjinga, mtini, karamu kubwa, mfarisayo na mtoza ushuru, fedha mafungu kumi, mwana mpotevu na mbazi ya wakulima. Baadhi ya mbazi tulizoshughulikia hapa ni pamoja na

**Mbazi ya punje ya haradali.**

**Mathayo 13:31-32.**

> "Akawatolea mfano mwingine,akisema, Ufalme wa mbinguni unafanana na punje ya haradali, aliyoitwaa mtu akaipanda katika shamba lake; nayo ni ndogo kuliko mbegu zote; lakini ikiisha kumea, huwa kubwa kuliko mboga zote, ikawa mti, hata nyuni wa angani huja na kukaa katika matawi yake."

Kwa kawaida, punje ya haradali ni punje ndogo sana wala haiwezi kutambuliwa mahali punje nyingine kubwa ziko. La kushangaza ni kwamba punje hii ikishapandwa shambani, humea na kuwa mti mkubwa zaidi ambapo hata nyuni wa angani hukaa katika matawi yake. Mbazi hii ni

funzo kwetu ya kwamba tusimdharau yeyote hata ingawa anaonekana dhaifu kati yetu. Huyu anayekaa dhaifu huenda akawa wa msaada kwetu baadaye kwani ya kesho hatuyajui. Nyuni ambaye ni aina ya ndege mkubwa hukaa kwenye matawi ya mti wa haradali, mti uliotokana na punje ndogo zaidi ya yote. Hii inadhihirisha ilivyosemwa na jamii ya Biblia za Tanzania na Kenya kwamba, ujumbe unaojitokeza katika Biblia kama kitabu cha fasihi ni ule wa kufunza, kuonya na kutahadharisha.

**Mbazi ya mtumwa asiye na msamaha**

Mathayo 18:21-35.

> "Kisha Petro akamwendea akamwambia, Bwana, ndugu yangu anikosee mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba? Yesu akamwambia, sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini. Kwa sababu hii, ufalme wa mbinguni umefanana na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake. Alipoanza kuifanya, aliletewa mtu mmoja awiwaye talanta elfu kumi. Naye alipokosa cha kulipa, bwana wake akaamuru auzwe, yeye na mkewe na watoto wake, na vitu vyote alivyo navyo, ikalipwe ile deni. Basi Yule mtumwa akaanguka, akamsujudia akisema, Bwana, nivumilie, name nitakulipa yote pia. Bwana wa mtumwa yule akamhurumia, akamfungua, akamsamehe ile deni. Mtumwa yule akatoka, akamwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari mia; akamkamata, akamshika koo, akisema, nilipe uwiwacho. Basi mjoli wake akaanguka miguuni pake, akamsihi, akisema, nivumilie, nami nitakulipa yote pia. Lakini hakutaka, akaenda, akamtupa kifungoni, hata atakapoilipa ile deni. Basi wajoli wake walipoyaona yaliyotendeka, walisikitika sana, wakaenda wakamweleza bwana wao yote yaliyotendeka. Ndipo bwana wake akamwita, akamwambia, Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe deni ile yote, uliponisihi, nawe, je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama nilivyokurehemu wewe? Bwana wake akaghadhibika, akampeleka kwa watesaji, hata atakapoilipa deni ile yote. Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake."

Hii ni hadithi iliyo na mafunzo kwa hadhira. Mtambaji anataka hadhira ijifunze kutokana na hali au masaibu yaliyomfika mtumwa ambaye hangeweza kusamehe. Yeye mwenyewe alikuwa na deni kubwa la mkubwa wake, lakini alipomlilia na kuomba msamaha, yule bwana alimhurumia

akamsamehe hilo deni. Mtumwa, baada ya kusamehewa alikutana na mdeni wake wa shilingi mia moja pekee. Baada ya kudai, mdeni wake alimlilia huku akimwomba msamaha. Badala ya kumsamehe, alimkamata na kumshika koo na kumfunga jela. Tendo hili lilimkasirisha mkubwa wake aliyeamua kwamba mtumwa ashikwe na afungwe jela pamoja na familia yake yote. Funzo linalopatikana katika mbazi hii ni kwamba tutendee wengine jinsi ambavyo tungependa kutendewa. Mtumwa anataka kusamehewa lakini yeye hataki kumsamehe mwenzake. Kutosamehe ndiko kulikomfanya akafungwa jela.

**Mbazi ya msamaria mwema**

Luka 10:25-37.

> "Na tazama, mwana-sheria mmoja alisimama amjaribu; akisema, Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele? Akamwambia, imeandikwa nini katika torati? Wasomaje? Akajibu akasema, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako. Akamwambia, Umejibu vema; fanya hivi nawe utaishi. Naye akitaka kujidai haki, alimwuliza Yesu, Na jirani yangu ni nani? Yesu akajibu akasema, Mtu mmoja alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko, akaangukia kati ya wanyang'anyi; wakamvua nguo, wakamtia jeraha, wakaenda zao, wakimwacha karibu ya kufa. Kwa nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile; na alipomwona alipita kando. Na Mlawi vivyo hivyo, alipofika pale akamwona, akapita kando. Lakini, Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo; na alipomwona alimhurumia, akakaribia, akamfunga jeraha zake, akizitia mafuta na divai; akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba ya wageni, akamtunza. Hata siku ya pili akatoa dinari mbili, akampa mwenye nyumba ya wageni, akisema, Mtunze huyu, na chochote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa. Waonaje wewe, katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi? Akasema, ni huyo aliyemwonea huruma. Yesu akamwambia, Enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo."

Yesu amewapa wafuasi wake changamoto. Kuhani na mlawia mbao waliokuwa waisraeli pamoja na mtu aliyeumia walipita kando yake walipomwona ameumia, wala hawakumjali ndewe wala sikio. Msamaria aliyekuwa wa mbari tofauti na iliyokuwa ya wachache waliodharauliwa na

Israel ndiye aliyejitolea kumsaidia huyu mtu. Hapa Yesu alikuwa akiwafunza tofauti kati ya imani za dini na upendo wa kweli. Ya kwamba jirani yako si yule mnayekaa tu karibu naye bali ni yule anayeweza kukusaidia wakati wa shida. Wakati mwingine wale tunaowadharau wanaweza kuwa msaada wetu wa karibu kushinda wale tunaowatarajia.

**Mbazi ya maombi ya mfarisayo na mtoza ushuru**

> "Akawaambia mfano huu watu waliojikinai ya kuwa wao ni wenye haki, wakiwadharau wengine wote. Watu wawili walipanda kwenda hekaluni kusali, mmoja farisayo, wa pili mtoza ushuru. Yule farisayo akasimama akiomba hivi moyoni mwake; Ee Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, wanyang'anyi, wadhalimu, wazinzi, wala kama huyu mtoza ushuru. Mimi nafunga mara mbili kwa juma; hutoa zaka katika mapato yangu yote. Lakini Yule mtoza ushuru alisimama mbali, wala hakuthubutu hata kuinua macho yake mbinguni, bali alijipiga-piga kifua akisema, Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi. Nawaambia, huyu alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko Yule; kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa."

Hili ni onyo kwa wale wanaopenda kujiinua na kuwadharau watu wengine. Mfarisayo aliienda mbele za Mungu akishukuru kwamba yeye ni mwenye haki wala si mwenye dhambi kama wengine akiwemo mtoza ushuru. Kinyume naye, mtoza ushuru alijiona mwenye dhambi asiyefaa mbele za Mungu, akaomba tu radhi kwa Mungu. Unyenyekevu wake ulimfurahisha Mungu hata akamhesabia haki kuliko yule mfarisayo aliyekuwa akijiinua. Ni funzo kwa wale wanaojiona bora kushinda wengine na kufikiria kwamba ni wao tu walio na ujuzi wala bila wao chochote hakiwezi kutendeka. Yesu alitamatisha kwa kuwaambia kwamba ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa.

**Mbazi ya mwana mpotevu**

Luka 15:11-24.

> "Akasema, mtu mmoja alikuwa na wana wawili; Yule mdogo akamwambia babaye, baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia. Akawagawia vitu vyake. Hata baada ya

siku si nyingi, yule mdogo akakusanya vyote, akasafiri kwenda nchi ya mbali; akatapanya mali yake huko kwa maisha ya uasherati. Alipokuwa amekwisha tumia vyote, njaa kuu iliingia nchi ile, yeye naye akaanza kuhitaji. Akaenda akashikamana na mwenyeji mmoja wan chi ile; naye alimpeleka shambani mwake kulisha nguruwe. Akawa anatamani kujishibisha na maganda waliyobakisha nguruwe, wala hapana mtu aliyempa kitu. Alipozingatia moyoni mwake, alisema, Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa? Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena. Nifanye kama mmoja wa watumishi wako. Akaondoka, akaenda kwa babaye. Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana. Yule mwana akamwambia, baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele zako, sistahili kuitwa mwana wako tena. Lakini baba aliwaambia watumwa wake, Leteni upesi vazi lililo bora, mkamvike. Mtieni na pete kidoleni, na viatu miguuni; mleteni ndama Yule aliyenona mkamchinje; nasi tule na kufurahi, kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana. Wakaanza kushangilia."

Jinsi anavyoeleza Plekanov (1957) katika mapitio ya maandishi, mojawapo ya majukumu ya fasihi simulizi ni kuielekeza jamii, kuichambua, kuikosoa na kuiongoza katika lengo lake la kuupindua unyonge na uchafu uliosakini katika jamii. Mbazi ya mwana mpotevu inalenga kuwaelekeza wanajamii, kuwakanya, kuwaadhibu na hata kuwafunza wanaosikiliza. Mtambaji anawataka wasikilizaji wajifunze kutokana na masaibu yaliyompata mwana mpotevu, ya kwamba nyumbani ni nyumbani na hata ukijaribu kutoroka, mwishowe utarudi jinsi alivyofanya mwana mpotevu. Aidha, mali huisha kwa hivyo tusikimbilie anasa za dunia tunapopata mali. Mwana mpotevu aliingilia anasa za dunia lakini mwishowe, mali yake yote iliisha hata ikabidi arudi kule alikotoka akiwa hana mbele wala nyuma. Mwisho, mbazi hii inatufunza umuhimu wa msamaha. Baba alimsamehe mwanawe aliporudi nyumbani hata akasahau jinsi alivyomtendea mabaya kwa kutumia mali yake yote katika anasa za dunia.

### 4.2.2 Maigizo

Maigizo kwa mujibu wa Wamitila (2008) ni mpangilio wa maneno ambayo huambatana na utendaji wa wahusika ambao huiga mambo yanayopatikana na jinsi yanavyoonekana katika jamii. Katika sehemu hii, tulijadili mazugumzo, mawaidha, miviga na michezo ya kuigizakama vipera vya maigizo. Maigizo huwa na sifa mbalimbali zikiwemo kuwepo kwa hadhira, maelekezo ya jukwaani na matumizi ya maleba.

#### 4.2.2.1 Mazungumzo

Mazungumzo ni upitishaji wa ujumbe au habari fulani zenye maana inayojadiliwa na watu au kikundi cha watu kwa lengo fulani ( M'Ngaruti 2008). Katika vitabu vya Biblia tulivyovisoma, kulidhihirika kipera hiki cha mazungumzo kwa njia mbalimbali.

**Mazungumzo kati ya Esau na Yakobo**

Mwanzo 25:29-34.

> "Yakobo akapika chakula cha dengu. Esau akaja kutoka nyikani, naye alikuwa amechoka sana. Esau akamwambia Yakobo, Tafadhali, unipe hicho chakula chekundu nile, kwa kuwa ninazimia mimi. Kwa hiyo walimwita jina lake Edomu. Yakobo akamwambia, kwanza niuzie leo haki yako ya mzaliwa wa kwanza. Esau akasema, Tazama, mimi ni karibu kufa, itanifaa nini haki hii ya uzazi? Yakobo akamwambia, Uniapie kwanza. Naye akamwapia, akamwuzia Yakobo haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Yakobo akampa Esau mkate na chakula cha dengu, naye akala, akanywa, kisha akaondoka, akaenda zake. Hivyo Esau akaidharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza."

Jinsi M'Ngaruthi asemavyo, mazungumzo kati ya Esau na Yakobo yalihusu jambo la kujadiliwa, chakula. Esau alikuwa na njaa sana iliyompelekea kukubali kuuza haki yake ya kuzaliwa kwa Yakobo ili apate chakula. Kupitia kwa mazungumzo waliyokuwa nayo kati yao, waliweza kuelewana hivi kwamba Yakobo alimpa Esau chakula naye Esau akamuuzia haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Jinsi ujumbe ulivyowasilishwa katika mazungumzo haya kati ya Esau ya Yakobo ndiyo yanayoyafanya kuwa mazungumzo.

**Mazungumzo kati yaYesu na ibilisi**

Mathayo 4:1-11.

> “Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na ibilisi. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Kisha ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia, Ukiwa wewe ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini, kwa maana imeandikwa, Atakuagizia malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua; Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe. Yesu akamwambia, Tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako. Kisha ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za Ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake. Kisha ibilisi akamwacha; na tazama, wakaja malaika wakamtumikia.”

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), kigezo kikuu kinachofanya mazumgumzo yawe ya kifasihi ni kuwapo kwa usanii na ufundi katika muundo wake na jinsi yanavyouwasilisha ujumbe wake. Hoja kuu ya ibilisi katika mazungumzo haya ilikuwa kumshawishi Yesu atende dhambi. Anatumia ufundi wa hali ya juu anapomjia yesu huku akielewa kwamba kwa siku arobanini Yesu alikuwa hajala chochote. Tunaona Yesu aidha akikabiliana naye katika mazungumzo yao hadi mwishowe ibilisi akamwacha. Ni mazungumzo kwani mojawapo wa sifa za mazungumzo ni kuwa na mada au wazo kuu lililojitokeza katika jamii. Ibilisi alitaka kumjaribu Yesu kwa kutaka kujua ikiwa kweli alikuwa mwana wa Mungu. Yesu pia kwa kumuonyesha alifahamu hiyo mada barabara, alizidi kumfahamisha ya kwamba imeandikwa kwa kukariri neno la Mungu. Alielewa hiyo mada kwa sababu yeye alikuwa mwana wa Mungu.

**Mazungumzo kati ta Yesu na wafarisayo**

Mathayo 19:3-11.

> “Basi Mafarisayo wakamwendea, wakamjaribu wakimwambia, Je! Ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu? Akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, akasema, Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili

watakuwa mwili mmoja? Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe. Wakamwambia, jinsi gani basi Musa aliamuru kumpa hati ya talaka, na kumwacha? Akawaambia, Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu; lakini tangu mwanzo haikuwa hivi. Nami nawaambia nyinyi, Kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa ni kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini; naye amwoaye Yule aliyeachwa azini. Wanafunzi wake wakamwambia, Mambo ya mtu na mkewe yakiwa hivyo, haifai kuoa. Lakini yeye akawaambia, Si wote wawezao kuipokea neno hili, ila wale waliojaliwa."

Kwa mujibu wa Ipara na Waititu (2004), mojawapo wa sifa za mazungumzo ni kuwa na mada au wazo kuu lililolijtokeza katika Jamii. Wafarisayo walikuwa na jambo lililokuwa likiwasumbua katika jamii, yaani talaka. Walitaka kujua kutoka kwa Yesu ikiwa ni halali mtu kumwacha mkewe ima fa ima. Kupitia mazungumzo waligundua kwamba mtu hafai kumwacha mkewe na kwamba Musa aliwaruhusu kupeana talaka kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao wala sio kwamba ilikuwa halali.

#### 4.2.2.2 Mawaidha

Kipera cha mawaidha kilijidhirisha katika vitabu vya Biblia vilivyosomwa. Mawaidha ni kipera kinachohusisha mazungumzo maalumu yanayolenga kuonya, kushauri, kuelekeza, kutahadharisha, kuelimisha na kuadilisha. Aghalabu mawaidha hutolewa na watu maalum katika jamii; wenye hekima, waadilifu na walioheshimika. Mulokozi (1996) anafafanua mawaidha kama maneno ya maonyo au mafunzo aghalabu yenye mwongozo. Baadhi ya mawaidha yaliyojitokeza ni pamoja na:

**Mawaidha ya Daudi kwa Sulemani.**

1Wafalme 2:1-9.

"Basi siku ya kufa kwake Daudi ikakaribia, akamwusia Sulemani mwanawe, akasema, Mimi naenda njia ya ulimwengu wote; basi uwe hodari, ujionyeshe kuwa mwanamume; uyashike mausia ya BWANA, Mungu wako, uende katika njia zake, uzishike sheria zake, na amri zake, na hukumu zake, na shuhuda zake, sawasawa na ilivyoandikwa katika torati

ya Musa, upate kufanikiwa katika kila ufanyalo, na kila utazamako; ili BWANA afanye imara neno lake alilonena kwa habari yangu, akisema, Ikiwa watoto wako wataiangalia njia yao, wakienda mbele zangu kwa kweli, kwa moyo wao wote, na kwa roho yao yote, (akasema), hutakosa mtu katika kiti cha enzi cha Israeli. Na zaidi ya hayo,umejua alivyonitenda Yoabu, mwana wa Seruya, yaani, alivyowatenda majemadari wawili wa majeshi ya Israeli, Abneri mwana wa Neri, na Amasa, mwana wa Yetheri, ambao aliwaua, na kuimwaga damu ya vita wakati wa amani, akautia damu ya vita mshipi uliokuwa viunoni mwake, na viatu vilivyokuwa miguuni mwake. Kwa hiyo ufanye kama ilivyo hekima yako, wala usimwachie mvi zake kushukia Ahera kwa amani. Lakini uwafanyie mema wana wa Barzilai, Mgileadi, wawe miongoni mwao walao mezani pako; kwa jinsi walivyonijilia nilipokuwa nimekimbia mbele ya Absalomu, ndugu yako. Hata, angalia, yuko pamoja nawe Shimei, mwana wa Gera, Mbenyamini, wa Bahurimu, ndiye aliyenilaani kwa laana kuu siku ile nilipokwenda Mahanaimu; lakini akashuka kunilaki kule Yordani, name nikamwapia kwa BWANA, nikamwambia, mimi sitakuua kwa upanga. Basi kwa hiyo usimwachilie, kwa kuwa wewe u mtu wa akili; nawe utajua ikupasayo umtendee, na mvi zake utazishusha Ahera pamoja na damu.”

Tumesema kwamba mawaidha hulenga kuonya, kushauri, kuelekeza na kadhalika. wakati mfalme Daudi alipojua kwamba anakaribia kifo chake, alimwita mwanawe Sulemani ambaye alikuwa amemuachia kiti cha uongozi, akampa ushauri na kumwelekeza jinsi ambavyo angefaulu katika uongozi wake; akamkumbusha haja ya kuzishika sheria za Mungu ili akaweze kufanikiwa katika kila jambo ambalo angelifanya. Daudi alikuwa mwadilifu na kiongozi au mfalme aliyemwogopa Mungu; ndiposa Mungu akamwita, rafiki yake. Kwa hivyo mawaidha haya yalitolewa na mtu mwadilifu ambaye alikuwa kielelezo, ilivyokuwa kuhusu mtoa mawaidha yeyote katika fasihi simulizi.

**Mawaidha ya Sulemani kwa mwanawe.**

**Mithali 1:8-19.**

**“**Mwanangu, yasikilize mafundisho ya baba yako, wala usiiache sheria ya mama yako, kwa maana hayo yatakuwa kilemba cha neema kichwani pako, na mikufu shingoni mwako. Mwanangu, wenye dhambi wakikushawishi, wewe usikubali! Wakisema, Haya!

> Njoo pamoja nasi, na tuvizie ili kumwaga damu; tumwotee asiye na hatia, bila sababu; tuwameze hai kama kuzimu, na wazima, kama wao washukao shimoni. Tutapata mali yote ya thamani, tutazijaza nyumba zetu mateka. Wewe utashirikiana nasi; tutakuwa na vitu vyote shirika. Mwanangu, usiende njiani pamoja nao; Uzuie mguu wako usiende katika mapita yao. Maana miguu yao huenda mbio maovuni, Nao hufanya haraka ili kumwaga damu. Kwa kuwa mtego hutegwa bure, mbele ya macho ya ndege yeyote. Na hao hujiotea damu yao wenyewe, hujinyemelea nafsi zao wenyewe. Ndivyo zilivyo njia za kila mwenye tama ya mali; huuondoa uhai wao walio nayo."

Mojawapo wa sifa za mawaidha ni kuimarisha maadili, adabu njema na kuwaelekeza wanajamii kuandama mwelekeo ufaao. Sulemani anamuasia mwanawe asiiache sheria ya mama yake wala asiandamane na wenye dhambi. Anamwelekeza kwa njia ifaayo ili aisije akaondoa uhai wake bure bali aweze kuishi maisha mazuri. Hapa, maadili na adabu njema inaimarishwa kama ilivyo mojawpo wa sifa za mawaidha.

**Mawaidha ya Yakobo kwa wanawe**

**Mwanzo 49:1-33.**

> "Yakobo akawaita wanawe, akasema, kusanyikeni, ili niwaambie yatakayowapata siku za mwisho. Kusanyikeni, msikie enyi wana wa Yakobo, Msikilizeni Israeli, baba yenu. Reubeni, u mzaliwa wangu wa kwanza, nguvu zangu, na malimbuko ya uwezo wangu. Umewapita wengine kwa ukuu na kwa nguvu. Umeruka mpaka kama maji, basi usiwe na ukuu, kwa sababu ulikipanda kitanda cha baba yako, ukakitia unajisi; alikipandia kitanda change. Benyamini ni mbwa-mwitu mwenye kurarua-rarua. Asubuhi atakula mawindo, na jioni atagawanya mateka. Hizo zote ndizo kabila za Israeli kumi na mbili. Na hayo ndiyo aliyowaambia baba yao, na kuwabariki; mmoja mmoja kwa mbaraka wake aliwabariki. Akawaamuru, akasema, mimi ninakwenda kukusanywa pamoja na watu wangu; mnizike pamoja na baba zangu, katika pango iliyomo shambani mwa Efroni, Mhiti, katika ile pango iliyomo shambani mwa Makpela, iliyo mbele ya Mamre katika nchi ya Kanaani, aliyoinunua Ibrahimu pamoja na shamba kwa Efroni Mhiti, pawe milki yake ya kuzika. Humo walimzika Ibrahimu, na Sara mkewe, humo wakamzika Isaka, na Rebeka mkewe; name humo nikamzika Lea; shamba na pango iliyomo lililonunuliwa

> kwa wazawa wa Hethi. Basi Yakobo alipokwisha kuwaagiza wanawe, akakunja miguu yake kitandani, akafa, akakusanywa pamoja na watu wake."

Kabla ya Yakobo kuaga dunia, aliwaita wanawe wote kwa ajili ya kuwapa mawaidha. Alianza na Rubeni aliyekuwa mzaliwa wa kwanza, hadi kwa Benyamini kitinda mimba. Aliwapa wote wosia wake wa mwisho ili akienda kwa babu zake, awaache baada ya kuwaelekeza, jinsi ilivyo kawaida ya mawaidha, yaani mafunzo aghalabu ya kidini na yenye mwongozo. Hakutaka wanawe wapotoke baada yake kuaga dunia. Aidha, alimtaka kila mmoja apate nafasi yake katika familia. Vilevile, alitaka azikwe mahali maalum, hivyo ilibidi awaelekeze. Haya mawaidha waliopewa wanawe Yakobo ni yala yale wazazi waliokuwa wakiwapa wanao katika tamaduni za Kiafrika, hivyo mwaingiliano matini unajitokeza.

**Mawaidha ya Yesu Kwa wanafunzi wake**

Luka 6: 20-26.

> "Akainua macho yake akawatazama wanafunzi wake, akasema, heri ninyi mlio maskini, kwa sababu ufalme wa Mungu ni wenu. Heri ninyi mlio na njaa sasa, kwa sababu mtashiba. Heri ninyi mliao sasa, kwa sababu mtacheka. Heri nyinyi watu watakapowachukia, na kuwatenga, na kuwashutumu, na kulitupa nje jina lenu kama neno ovu, kwa ajili ya mwana wa Adamu. Furahini siku ile na kuruka-ruka, kwa kuwa, tazama, thawabu yenu ni kubwa mbinguni, maana, baba zao waliwatenda manabii vivyo hivyo. Lakini, ole wenu ninyi mlio na mali, kwa kuwa faraja yenu mmekwisha kuipata. Ole wenu ninyi ambao mmeshiba sasa, kwa kuwa mtaona njaa. Ole wenu ninyi mnacheka sasa, kwa kuwa mtaomboleza na kulia. Ole wenu ninyi watu wote watakapowasifu, kwa kuwa baba zao waliwatenda manabii wa uongo mambo kama hayo."

Yesu aliwapa wanafunzi wake mawaidha kuhusu jinsi wanavyofaa kuishi. Akawakumbusha umuhimu wa kupenda adui zao na kuwatendea mema; kuwa na huruma, kutolaumu yeyote na kupeana vitu kwa walio na mahitaji. Kwa mujibu wa Ipara na waititu (2004), aghalabu, mawaidha hutolewa zaidi kwenye sherehe za dini au ibada, ama mahali popote wakati wowote. Yesu alikuwa mahali tambarare pamoja na wafuasi wake wengi, na makutano makubwa ya watu

waliotoka sehemu mbalimbali alipoamua kuwapa haya mawaidha. Kwa kawaida mawaidha ni njia moja ya kutoa elimu ya jamii na kuwapa wanajamii maadili, amali na turathi.

#### 4.2.2.3. Sanaa ya maonyesho

Katika sanaa ya maonyesho huwa kuna mpangilio wa mazungumzo baina ya watu pamoja na matendo yao. Mazungumzo hayo hujenga kisa ambacho kinaonyesha mgogoro fulani (wamitila 2003). Katika utafiti huu baadhi ya sanaa za maonyesho zilijidhihirisha zikiwemo:

**Maonyesho ya Sulemani na makahaba wawili**

1Wafalme 3: 6-28.

> "Ndipo wanawake wawili, makahaba, walimwendea mfalme, wakasimama mbele yake. Na mwanamke mmoja akasema, Ee bwana wangu, mimi na mwanamke huyu tunakaa katika nyumba moja; nami nalizaa nilipokuwa pamoja naye nyumbani. Kisha, siku ya tatu baada ya kuzaa kwangu, ikawa mwanamke huyu naye akazaa; na sisi tulikuwa pamoja; hapakuwa na mtu mwingine pamoja nasi nyumbani, isipokuwa sisi wawili tu. Na mtoto wa mwanamke huyu akafa usiku, maana alimlalia. Akaondoka kati ya usiku, akamwondoa mtoto wangu ubavuni pangu, mimi mjakazi wako nilipokuwa usingizini, akamweka kifuani pake, na mtoto wake mwenyewe, aliyekuwa amekufa, akamweka kifuani pangu. Nilipoondoka asubuhi nimnyonyeshe mtoto wangu, kumbe! Amekufa. Hata asubuhi nilipomtazama sana, kumbe! Siye mtoto wangu niliyemzaa. Ndipo Yule mwanamke wa pili akasema, sivyo hivyo, bali mtoto wangu ndiye aliye hai, na mtoto wako ndiye aliyekufa. Na mwenzake akasema, sivyo hivyo; bali mtoto wako ndiye aliyekufa, na mtoto wangu ndiye aliye hai. Ndivyo walivyosema mbele ya mfalme. Ndipo mfalme akasema, huyu anasema, mtoto wangu yu hai, na mtoto wako amekufa. Na huyu anasema, sivyo hivyo; bali mtoto aliyekufa ni wako, na mtoto aliye hai ni wangu. Mfalme akasema, nileteeni upanga. Wakaleta upanga mbele ya mfalme. Mfalme akasema, mkate mtoto aliye hai vipande viwili, kampe huyu nusu, na huyu nusu. Ndipo mwanamke Yule, ambaye mtoto aliye hai ni wake, akamwambia mfalme, kwa maana moyoni mwake alimwonea mtoto wake huruma, akasema, Ee bwana wangu, mpe huyu mtoto aliye hai, wala usimwue kamwe. Lakini Yule mwingine akasema, asiwe wangu wala wako; na akatwe. Ndipo mfalme akajibu, akasema, mpe huyu wa kwanza

mtoto aliye hai, maana yeye ndiye mama yake. Na Israeli wote wakapata habari za hukumu ile aliyoihukumu mfalme wakamwogopa mfalme; maana waliona ya kuwa hekima ya Mungu ilikuwa ndani yake, ili afanye hukumu”.

Katika maonyesho haya, tunashuhudia mgogoro kati ya makahaba wawili wote ambao walidai mtoto aliyekuwa hai alikuwa wao. Sulemani kwa kutumia hekima yake akaagiza upanga, lengo lake likiwa kumkata huyo Mtoto aliyekuwa hai vipande viwili ili kila kahaba apewe nusu nusu. Mwanamke aliyekuwa mama halali wa mtoto akamwonea mtoto wake huruma na akapendekeza apewe yule mwenzake badala ya kuuawa. Yule mwingine naye akashikilia auawe kila mmoja apewe nusu, ndiposa Sulemani akapeana mtoto kwa mzazi halali. Baadhi ya vifaa vilivyotumika katika maonyesho haya ni pamoja na upanga. Maonyesho yenyewe yalikuwa mbele ya hadhira kwani tunamwona mfalme akiitisha upanga kutoka kwa hiyo hadhira. Vilevile hawa wanawake wanaonekana wakijibizana kule jukwaani, wote wakidai mtoto aliyekuwa hai ni wao; kisha mama halisi wa mtoto anakataa mtoto asiuawe kuonyesha hali halisi ya mgogoro.

**Maonyesho ya Elisha na mwanamke mjane**

2Wafalme 4:1-6.

> “Basi, mwanamke mmoja miongoni mwa wake za wana wa manabii alimlilia Elisha, akasema, Mtumishi wako mume wangu amekufa; nawe unajua ya kuwa mtumishi wako alikuwa mcha BWANA; na aliyemwia amekuja ili ajitwalie wana wangu wawili kuwa watumwa. Elisha akamwambia, Nikufanyie nini? Niambie, una kitu gani nyumbani? Akasema, mimi mjakazi wako sina kitu nyumbani, ila chupa ya mafuta. Akasema, Nenda, ukatake vyombo vile vyote; navyo vilivyojaa ukavitenge. Basi akamwacha, akajifungia mlango yeye na wanawe hao wakamletea vile vyombo, na yeye akamimina. Ikawa, vilipokwisha kujaa vile vyombo, akamwambia mwanawe, Niletee tena chombo. Akamwambia, Hakuna tena chombo. Mafuta yakakoma. Ndipo akaja akamwambia Yule mtu wa Mungu. Naye akasema, enenda ukayauze mafuta haya, uilipe deni yako; nayo yaliyosalia uyatumie wewe na watoto wako.”

Huyu mwanamke, baada ya kumpoteza bwanake hakuwa na chochote. Akamwendea nabii Elisha akiomba usaidizi kwani mdeni wake alikuwa amekuja kumdai. Elisha alimwagiza atafute vyombo vitupu vingi iwezekanavyo kisha aingie ndani ajifungie pamoja na mwanawe

avimiminie vyombo mafuta. Baada ya vyombo vyote kujaa mafuta yakakoma. Elisha akamwambia auze hayo mafuta alipe deni na yaliyobaki ayatumie na mtoto wake. Hapa tunaona maigizo kamili na vifaa kama chupa, mafuta na vyombo vimetumika katika ile hali ya kuzua mazingira maalum. Wahusika nao ni mama, mtoto, mdeni na mtu wa Mungu.

**Maonyesho ya kuuawa kwa Yohana mbatizaji**

Matayo 14:6-12.

> “Hata ilipofika sikukuu ya kuzaliwa kwake Herode, binti Herodia alicheza mbele ya watu, akampendeza Herode. Hata akaahidi kwa kiapo ya kwamba atampa lo lote atakaloliomba. Naye, huku akichochewa na mamaye, akasema, Nipe hapa katika kombe kichwa cha Yohana mbatizaji. Naye mfalme akasikitika; lakini kwa ajili ya viapo vyake, na kwa ajili ya wale walioketi chakulani pamoja naye, akaamuru apewe, akatuma mtu, akamkata kichwa Yohana mle gerezani. Kichwa chake kikaletwa katika kombe, akapewa yule kijana; akakichukua kwa mamaye. Wanafunzi wake wakaenda, wakachukua yule maiti, wakamzika; kisha wakaenda wakampasha Yesu habari.”

Mchezo wa kuigiza hujumuisha vitendo vinavyofanywa kwa ufundi na huandamana na matendo au mambo ya ziada kama nyimbo na ngoma. Vilevile hutegemea vifaa, maleba na mapambo (Ipara na Waititu 2004). Katika mchezo huu tunaona bintiye Herode akicheza mbele ya watu mpaka akampendeza Herode ambaye aliahidi kwamba angempa chochote ambacho angeomba. Kwa kuchochewa na mamaye, binti huyu aliomba kichwa cha Yohana mbatizaji ambacho aliletewa katika kombe. Hapa tunamwona Herode akiapa ambapo inabidi ampe bintiye kichwa cha Yohana ingawa kwa masikitiko. Aidha tunaona vifaa kama chakula, kombe, na kichwa, kudhihirisha kwamba huu ni mchezo wa kuigiza kwa sababu matumizi ya vifaa ni baadhi ya sifa za mchezo wa kuigiza. Ni dhahiri kuwa maonyesho ya sanaa kama umbo la fasihi simulizi yamedhihirika katika kisa hiki.

**Maonyesho ya kusulubiwa kwa Yesu**

Luka 22:47-62.

> “Baadaye kitambo mtu mwingine alimwona akasema, Wewe nawe u mmoja wao. Petro akasema, Ee mtu, si mimi. Halafu yapata saa moja, mtu mwingine alikaza kusema, Hakika na huyu alikuwa pamoja naye, kwa kuwa yeye piya ni Mgalilaya. Petro akasema,

> Ee mtu, sijui usemalo. Na papo hapo alipokuwa katika kusema, jogoo aliwika. Bwana akageuka akamtazama Petro. Petro akalikumbuka lile neno la Bwana jinsi alivyomwambia, Leo kabla hajawika jogoo utanikana mara tatu. Akatoka nje akalia kwa majonzi."

Mambo mengi yanabainika kuonyesha kwamba huu ni mchezo wa kuigiza. Lugha imetumiwa kwa ufundi wa hali ya juu na matendo yameonyeshwa. Kwa mfano, kuna usemi wa moja kwa moja kama vile ; "Ee mtu, si mimi" na " papo hapo". Aidha, kuna semi kama vile, "Yesu alijitenga na wanafunzi wake kama kiasi cha kutupa jiwe, akapiga magoti akaomba, hari yake ikawa kama matone ya damu yakidondoka nchi'. Aidha, Yuda anamkaribia Yesu ili kumbusu. Wafuasi wa Yesu wakauliza, 'Bwana, tuwapige kwa upanga?' mmoja akamkata kuhani mkuu sikio la kuume, naye Yesu akamgusa sikio lenyewe akamponya. Pia tunaona Yesu akiwauliza wakuu wa makuhani, maakida wa hekalu na wazee waliokuja juu yake, 'Je, mmekuja na mapanga na marungu kama kukamata mnyang'anyi?'Mapanga na marungu ni baadhi ya vifaa vilivyotumika katika mchezo huu. Aidha, tunaona watu wakiota moto, Petero mfuasi wa Yesu akiwa mmoja "Basi alipokuwa katika kusema, tazama, mkutano wa watu, na Yule aitwaye Yuda, ambaye ni mmoja wa wale thenashara, amewatangulia. Akamkaribia Yesu ili kumbusu. Yesu akamwambia, Yuda, wamsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu? Na wale waliokuwa karibu naye walipoona yatakayotukia, walisema, Bwana, tuwapige kwa upanga? Mmoja wao akammpiga mtumwa wa kuhani Mkuu, akamkata sikio la kuume. Yesu akajibu akasema, Muwe radhi kwa hili. Akamgusa sikio, akamponya. Yesu akawaambia wakuu wa makuhani, na maakida wa hekalu, na wazee, waliokuja juu yake, Je! Mmekuja wenye panga na marungu kama kukamata mnyang'anyi? Kila siku nilipokuwa pamoja nanyi hekaluni hamkuninyoshea mikono, lakini hii ndiyo saa yenu, na mamlaka ya giza. Wakamkamata, wakamchukua, wakaenda naye nyumbani kwa Kuhani Mkuu. Na Petro alimfuata kwa mbali. Na walipokwisha washa moto katikati ya kiwanja, waliketi pamoja, naye Petro akaketi kati yao. Ndipo mjakazi mmoja akamwona ameketi mwangani, akamkazia macho akasema, Na huyu alikuwa pamoja naye. Akakana, akisema, Ee mwanamke, simjui huyo".

Anapoulizwa ikiwa alikuwa pamoja na Yesu anakana. Baadaye jogoo anapowika, anakumbuka yale Yesu aliyomwambia kwamba 'kabla jogoo awike utanikana mara tatu', mwishowe Yesu

akatwikwa msalaba kisha baadaye akasulubiwa. Wakachukua mavazi yake wakagawana. Mavazi hapa ni mfano mzuri wa maleba. Pia vitu kama taji la miiba alilovalishwa kichwani ni maleba. Mkuki uliotumiwa kumchoma, siki aliyopewa anywe, misumari iliyochomelewa miguuni na mikononi mwake; vyote ni vifaa vilivyotumika katika mchezo huu kama sifa za maonyesho ya sanaa, kwa hivyo huu ni mfano mzuri wa sanaa ya maonyesho katika Biblia.

#### 4.2.2.4 Miviga

Mulokozi (1989) anaeleza miviga kama sherehe au shughuli mbalimbali za kitamaduni zinazofanywa kufuatana na desturi au kaida fulani kwa sababu maalum. Miviga hujumuisha vitendo maalumu kama kuimba, kuomba na kucheza ngoma. Wahusika hutoa sadaka na huweka ahadi za kutenda mema. Wamitila (2003) anafafanua miviga kama neno linalotumiwa kuelezea sherehe za kitamaduni na huweza kuhusisha matambiko. Ni matendo madhubuti ambayo hubainisha maigizo. Leo na Tonny (2006) wanasema kwamba miviga hutumika kurejelea sherehe za jamii ya watu kama vile ndoa, tohara, kuzaliwa, jando na unyago, matambiko na matanga. Baadhi ya sifa za miviga ni pamoja na; huwa na kipindi maalum cha kutendeka; Huwa na sababu maalum ya kufanyika sherehe; Sherehe huhusishwa na sheria maalum; Ni watu maalum wanaoendesha sherehe hizi kama vile wazee. Katika utafiti huu kuna visa mbalimbali vilivyojitokeza kama miviga. Baadhi yao ni pamoja na:

**Miviga ya Isaka kutolewa kama sadaka ya kuteketezwa**

Mwanzo 22: 1-14.

> “Ikawa baada ya mambo hayo Mungu alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ee Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa. Akasema, Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia. Ibrahimu akaondoka alfajiri, akatandika punda wake, akachukua vijana wawili pamoja naye, na Isaka mwanawe, akachanja kuni kwa ajili ya hiyo sadaka ya kuteketezwa, akaondoka, akaenda mpaka mahali alipoambiwa na Mungu. Siku ya tatu Ibrahimu akainua macho yake, akapaona mahali pakali mbali. Ibrahimu akawaambia vijana wake, Kaeni nyinyi hapa pamoja na punda, na mimi na kijana tutakwenda kule, tukaabudu, na kuwarudia tena. Basi Ibrahimu akazitwaa kuni za hiyo sadaka, akamtwika Isaka mwanawe, akatwaa moto na kisu

> mkononi mwake, wakaenda wote wawili pamoja. Isaka akasema na Ibrahimu babake, akinena, Babangu! Naye akasema, Mimi hapa mwanangu. Akasema, Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yupo wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa? Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili pamoja. Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu, Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni, kisha akamfunga Isaka mwanawe, akamweka juu ya madhahabu, juu ya zile kuni. Ibrahimu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe. Ndipo malaika wa BWANA akamwita kutoka mbinguni, akasema, Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa. Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, ikiwa hukuniulizia mwanao, mwanao wa pekee. Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe. Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-Yire, kama watu wasemavyo hata leo, katika mlima wa BWANA itapatikana."

Ibrahimu, baada ya kukaa kwa miaka mingi sana bila mtoto, mwishowe alifanikiwa kupata mtoto kwa jina Isaka, akiwa miaka mia moja, (Mwanzo 17:17). Alipoulizwa na Mungu akamtoe mwanawe kama sadaka ya kuteketezwa, Ibrahimu hakusita kama ilivyo kawaida ya miviga, Alichukua mwanawe Isaka kama sadaka kwa Mungu, akajenga madhabahu, akatayarisha kuni kisha akamfunga Isaka, akamweka juu ya madhabahu juu ya zile kuni. Ibrahimu alikuwa akitimiza mila na desturi za kwao za kumtolea Mungu sadaka. Ingawa hakumchinja Isaka, Mungu alimpa kondoo akamtoa Sadaka ya kuteketezwa badala ya Isaka. Katika miviga, kuna matumizi ya vifaa, mavazi na mapambo maalum. Ibrahimu alikuwa na kuni, kisu na moto. Aidha kulikuwa na madhabahu ambapo sadaka ilifaa iteketezewe, kama sifa mojawapo ya miviga.

**Miviga ya sanduku la agano kupelekwa hekaluni**

1Wafalme 8:1-5.

> “Ndipo Sulemani alipowakusanya wazee wa Israel, na wakuu wote wa kabila, wakuu wa mbari za mababa wa wana wa Israeli, wamwendee mfalme Sulemani huko Yerusalemu,

> ili walipandishe sanduku la agano la BWANA kutoka mji wa Daudi, yaani, Sayuni. Wakakutana mbele ya mfalme Sulemani watu wote wa Israeli wakati wa sikukuu, katika mwezi wa Ethanimu, ndio mwezi wa saba. Wazee wote wa Israeli wakaja, nao makuhani wakajitwika sanduku. Wakalipandisha sanduku la BWANA, na ile hema ya kukutania, na vyombo vitakatifu vyote vilivyokuwa katika ile Hema; vitu hivyo makuhani wa Walawi wakavipandisha. Mfalme Sulemani, na makutano wote wa Israeli waliokutanika kwake walikuwako pamoja naye mbele ya sanduku, wakichinja sadaka kondoo na ng'ombe, wasioweza kuhesabiwa wala kufahamiwa idadi yao kwa kuwa wengi."

Hapa kulikuwa na sherehe wakati ambapo sanduku la agano lilikuwa likipelekwa hekaluni kutoka mji wa Daudi, yaani Sayuni. Sulemani pamoja na wana wa Israeli walisherehekea kwa furaha kuu. Kondoo na ng'ombe wasioweza kuhesabiwa walichinjwa na kutolewa kama sadaka kwa Mungu. Kulikuwa na nyimbo za kusifu pamoja na maombi ya kumshukuru Mungu kwa uaminifu wake. Aidha kukatolewa sadaka ya unga na mafuta kama sadaka za amani, kukawa na sikikuu kwa siku kumi na nne kisha baadaye watu wakaagana kwa furaha kuu. Kama asemavyo Ipara na Waitutu (2004), miviga huwa na sababu fulani zikiwemo kutakasa na kuomba baraka, pamoja na kujenga uhusiano mwema na miungu au mababu. Tunaona haya yote yakijitokeza katika miviga hii. Sulemani aliomba baraka kwa Mungu kwa niaba ya wana wa Israeli, na katika ile hali ya kuomba na kutoa sadaka kwa Mungu, walikuwa wakijenga uhusiano mwema kati yao na Mungu.

**Miviga ya kutahiriwa na kutakaswa kwa Yesu**

Luka 2:21-24.

> "Hata ziliotumia siku nane za kumtahiri, aliitwa jina lake Yesu, kama alivyoitwa na malaika kabla hajachukuliwa mimba. Kisha, zilipotimia siku za kutakasika kwao kama ilivyo torati ya Musa walikwenda naye hata Yerusalemu, wamweke kwa Bwana, (kama ilivyoandikwa katika sheria ya Bwana, kila Mtoto mwanamume aliye kufungua mimba

> ya mamaye na aitwe mtakatifu kwa Bwana), wakatoe na sadaka, kama ilivyonenwa katika sheria ya Bwana; Hura wawili au makinda ya njiwa wawili."

Yesu alitahiriwa siku ya nane na pia kutakaswa kama ilivyokuwa torati ya Musa. Wazazi wake walitoa sadaka ya huria wawili na makinda ya njiwa wawili kama ilivyokuwa desturi yao. Miviga kwa mujibu wa wamitila (2003) huelezea sherehe za kitamaduni. Hapa tunaona sherehe ya kutahiriwa na kutakaswa kwa Yesu ikifanywa kulingana na desturi na tamaduni za Wayahudi. Kutakaswa kulitendeka hekaluni ili kumweka kwa Bwana, kama ilivyokuwa sheria yao kwamba kila mtoto mwanamume aliye kifungua mimba wa mamaye aitwe mtakatifu wa Bwana. Wazazi wa Yesu walifanya yote waliyotakikana kufanya kulingana na tamaduni zao.

#### 4.2.3 Semi

Semi ni fungu la tungo za kisanaa ambazo ni fupi fupi zenye kutumia picha, tamathali na ishara. Semi hizi hubeba maana na mafunzo muhimu kijamii (Mwansoko, 1988). Wamitila (2003) naye anafafanua semi kama tungo za fasihi simulizi ambazo ni fupifupi na zina matumizi ya taswira, tamathali na ishara kwa mapana. Ujumbe wake huwasilishwa kwa njia ya mkato yenye mkokotezo na hukumbukika haraka. Baadhi ya semi zilizojidhihirisha katika utafiti huu ni pamoja na methali, vitendawili, nahau, tashhisi, tashbihi na takriri. Kila kipera kilichunguzwa kama ifuatavyo.

##### 4.2.3.1 Methali

Mulokozi (1989) anaeleza methali kama semi fupifupi ya kueleza kwa muhtasari fikira au mafunzo mazito yaliyotokana na uzoefu wa kijamii. Mara nyingi maelezo haya huelezwa kwa kutumia tamathali za usemi hasa sitiari na mafumbo. Mtesigwa (1989) anatoa baadhi ya sifa za methali kuwa; methali huwa usemi mfupi na wenye urari wa maneno ijapokuwa maneno hayo si mepesi na ya kawaida. Usemi huo ukubalike na watumiaji wa lugha husika kwa sababu unatokana na maadili au vitendo vya kila siku vinavyochipuka kutoka katika jamiii ya lugha ile.
Utafiti huu uligundua kwamba kunazo methali nyingi sana zinazopatikana katika Biblia, hasa katika vitabu vya zaburi na mithali. Baadhi ya methali hizo ni pamoja na;

Mithali 10:1

"Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye, bali mwana mpumbavu ni mzigo wa mamaye".

Mithali 10: 12

"Kuchukiana huondokesha fitina, bali kupendana husitiri fitina".

Mithali 11:2

"Kijapo kiburi ndipo ijapo aibu, bali hekima hukaa na wanyenyekevu"

Mithali 13: 24

"Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe, bali yeye ampendaye humrudi mapema".

Mithali 15:1

"Jawabu la upole hugeuza hasira, bali neno liumizalo huchochea ghadhabu".

Mithali 17:17

"Rafiki hupenda siku zote; na ndugu, amezaliwa kwa siku ya taabu".

Mithali 21:17

"Mtu apendaye anasa, atakufa maskini".

Mithali 25:15

"Ulimi laini, huvunja mfupa".

Mithali 27:12

"Mwenye busara huona mabaya na kujificha, bali wajinga huendelea mbele wakaumia".

Mithali 29:11

"Aonywaye mara nyingi akishupaza shingo, atavunjika ghafla, wala hapati dawa".

Zaburi 126:5.

"Wapandao kwa machozi, watavuna kwa kelele za furaha".

Hizo zote ambazo zimetajwa ni methali. Aidha, Nkwera (1978) anasema kuwa methali ni kauli zenye busara na mafunzo kuhusu maisha na mahusiano ya watu. Wingi wa methali huwa na muundo wenye sehemu mbili, sehemu ya kwanza ambayo huanzisha wazo na ya pili ambayo hukanushua kulikamilisha hilo wazo; kwa mfano;

Adhabu kali ina aiachaye njia, naye achukiaye kukemewa atakufa (methali 15:10),

Zizi ni safi ambapo hapana ng'ombe, bali nguvu za ng'ombe zaleta faida (methali 14:4).

Hata hivyo kuna methali chache ambazo hazifuati mpangilio huu. Zingine zina sehemu ya pili ndefu kushinda sehemu ya kwanza, ama sehemu zote huwa sawa. Mfano :

Kiburi, hutangulia uangamivu (Mithali 16: 18)
Asiye na akili, humdharau mwenziwe (Mithali 11:12).

Mlacha (1985) anatueleza kuwa methali zimejaa maadili ambayo husaidia mwanadamu kwa kumwongoza kwenye misingi bora ya maisha. Kuna zile za kuonya, kuusia, kushauri na kufunza. Kuna vilevile zile za kukaripia na hata kukemea. Zote zilizotajwa hapo juu zinatimiza malengo hayo.

**4.2.3.2. Vitendawili**.

Ipara na Waititu (2006) wanafafanua vitendawili kama kauli fupi za kisanaa na kimafumbo ambazo hutolewa kwa watu ili wazifumbue. Hutumia lugha kisanaa na kwa kusudi maalum. Maana na majibu ya vitendawili hutegemea mazingira ya jamii inayohusika. Wamitila (2008) anaeleza vitendawili kama semi ambazo huwa zimefumbwa na hutolewa kwa mtu ili azifumbue. Kwake, kitendawili kinaweza kuwa sentensi fupi ama maelezo marefu. Vitendawili huwa na swali ambalo hujibiwa kwa kuteguliwa.

Utafiti huu umetambua vitendawili mbalimbali katika vitabu vya Biblia vilivyoteuliwa, hasa katika zaburi, mithali, Mathayo na Luka. Baadhi ya vitendawili vilivyojidhihirisha ni pamoja na Mithali 7: 16.

> "Nimetandika kitanda changu magodoro mazuri, kwa matandiko ya kimisri yenye msitari".

Jibu: Mwanamke anayemshawishi mwanamume wakafanye mapenzi.

Hapa mwandishi ametumia lugha ya mafumbo. Anayezungumziwa ni kahaba ambaye anataka kumteka huyu mwanamme. Ametumia mazingira ya kawaida ambayo ni magodoro mazuri na matandiko ya Kimisri yenye mistari, yaani matandiko ya kifahari. Kwa hivyo kutegua kitendawili hiki, ni mwanamke anayemshawishi mwanamume wakafanye naye mapenzi.

Mithali 9: 7

> "Maji yaliyoibiwa ni matamu, na mkate ulioliwa kwa siri hupendeza".

Jibu: Mapenzi ya siri.

Hiki ni kitendawili ambacho jawabu lake ni mapenzi ya siri. Huyu ni mwanamke anayetambuliwa na Biblia kama mpumbavu ambaye hukaa mlangoni mwa nyumba yake akiwaita wapita njia ili waweze kufanya mapenzi naye.

Mithali 13: 7

> "Kuna mtu mwenye kujitajirisha lakini hana kitu, kuna ajifanyaye kuwa maskini lakini ana mali nyingi".

Jawabu la hiki kitendawili ni, mwenye kujiinua na mnyenyekevu.

Mwenye kujitajirisha (anayejiinua) huenda mwishowe akakosa kila kitu ilhali yule ajifanyaye kuwa maskini, yaani anayejinyenyekeza huenda akafanikiwa maishani na akawa na zaidi ya walivyotarajia watu. Ni vyema kunyenyekea mbele ya wenzetu.

Mithali 24:33.

> "Bado kulala kidogo, kusinzia kidogo, bado kukunja mikono upate usingizi! Hivyo umaskini wako huja kama mnyanganyi na uhitaji wako kama mtu mwenye silaha".

Jawabu ni uzembe/ uvivu.

Mtu mvivu anaogopa kazi. Badala ya kuamka asubuhi aanze kazi anaamua asinzie kidogo, akunje mikono apate usingizi. Katika hiyo hali ya usingizi anashindwa kufanya kazi zake na mwishowe anajikuta katika hali ya umaskini. Wakati wa mavuno hana chochote kwani hakutayarisha shamba lake.

Mathayo 8: 22.

> "Waache wafu wazike wafu wao".

Jibu: Mungu awekwe mbele ya kila kitu.

Katika kitendawili hiki, vitu visivyo na uhai vimepewa sifa za binadamu. Wafu hawana uhai. Yesu anapowaambia waache wafu wazike wafu wao, anatumia lugha fiche kwani inaonekana kwamba katika jamii husika jambo la mazishi ni la kawaida na kwamba watu wamependa sana mambo ya kuzika wafu. Kwa hivyo anajaribu kuwaeleza kwamba ukitaka kuwa mfuasi wake, lazima uweke mambo ya Mungu mbele wala sio yako binafsi.

Mithali 12:33.

> "Mti mwema hutoa matunda mazuri, na mti mbaya matunda mabaya".

Jibu: mtu mwema hutenda mazuri, naye mbaya hutenda mabaya.

Mulokozi (1989) anaeleza kwamba vitendawili hufuatana na mazingira maalum ya watu pamoja na Silka, tamaduni na itikadi zao. Ni rahisi kupata maana ya kitendawili ukiwa na ujuzi wa mazingira yaliyozaa kitendawail hicho.Kitendawili hiki kimezuka katika jamii ya kiukulima ambapo watu wanaelewa aina ya miti na matunda yanayotokana na miti hiyo. Yesu alitumia kitendawili hiki akizingatia mazingira yanayofahamika.

Luka 7: 41 – 42.

> "Mtu mmoja mkopeshaji alikuwa na wadeni wawili; mmoja amwia dinari mia tano, na wa pili hamsini. Nao walipokuwa hawana cha kumlipa, aliwasamehe hawana cha kumlipa, aliwasamehe wote wawili katika hao wawili ni yupi atakayempenda zaidi"?

Jibu:Aliyekopeshwa dinari mia tano.

Huu ni mfano wa kitendawili chenye sentensi ndefu kama asemavyo Wamitila (2008). Yesu alitumia kitendawili hiki wakati alipoalikwa kwa nyumba ya mfarisayo kwa chakula kisha mwanamke mwenye dhambi akaja hapo na kuanza kumdondoshea machozi yake na kuipanguza kwa nywele ya kichwa chake huku akiipaka ile miguu ya Yesu marhamu mfarisayo aliyemwalika alighadhabishwa na kitendo hicho kwani mwanamke huyo alikuwa mwenye dhambi naye Yesu ni mtakatifu. Yesu alitaka wajifunze kutokana na kitendawili hicho kwani mwenye dhambi nyingi anaposamehewa hupenda zaidi ya Yule asiye na dhambi nyingi. Aliyesamehewa dinari mia tano bila shaka alipenda kuliko aliyesamehewa dinari tano.

#### 4.2.3.3. Misemo/ nahau

Ipara na Waititu (2004) wanaeleza misemo kama tungo fupi ambazo hutumia mbinu za picha, ishara au tamathali za usemi ili kutoa wazo au maana kuhusu jambo, kitu au mtu. Maana ya misemo hutegemea mazingira, muktadha na utamaduni wa watu. Kuna aina mbili za misemo: misemo inayotumia kitenzi na nomino, yaani nahau, na misemo ambayo hutumia aina nyingine za maneno isipokuwa kitenzi.

Wamitila (2003) anaeleza nahau kama kauli zilizoundwa kwa lugha ya kawaida lakini zenye maana iliyofichika. Ni kama vikolezo vya kutia utamu katika lugha inayohusika. Ipara na Waititu (2004) wanasema kwamba nahau ni misemo inayotumia kitenzi na nomino. Baadhi ya misemo/ nahau iliyojitokeza katika utafiti huu ni pamoja na;

Zaburi 91:1

Msemo; "Kaa katika uvuli wake mwenyezi".

Zaburi 45:1

Msemo: "Furika kwa neno jema".

Zaburi 64:3

Nahau: "Kutunywesha mvinyo wa kutuyumbisha".

Zaburi 85:7

Nahau: "Tuonyeshe rehema zako".

Mithali 1: 9.

Nahau: "Kuvaa kilemba cha neema kichwani".

Zaburi 104:9

Nahau: "Umeweka mpaka wasipite".

Zaburi 119:58

Nahau: "Nimekuomba radhi".

Zaburi 140:3

Nahau: "Wamenoa ndimi zao".

Mithali 6:14

Nahau: “Hupenda mbegu za magomvi”.

Mithali 6: 21

Nahau: “Jivike maagizo shingoni mwako”.

Mithali 9:8

Nahau: “Alishika njia”.

Mithali 7:18

Nahau: “Tushibe pendo”.

Mithali 3:3

Nahau: “Zifunge sheria shingoni mwake”.

Mithali 5:15

Nahau: “Unywe maji ya birika lako mwenyewe”.

Mithali 31:9

Nahau: “Tambua kinywa chako”.

Mithali 31:20

Nahau “Huwakunjulia maskini mikono yake”.

**Mifano ya matumizi**.

Zaburi 91:1.

“Kukaa katika uvuli wa mwenyezi”.

Hapa haimaanishi Mungu atasimama hapo na unakaa chini ya kivuli chake, bali inamaanisha kuwa na amani ya Mungu. Yaani ikiwa watatafuta uso wa Mungu kwa kutembea katika njia zake na kutenda mapenzi yake, basi wataishi kwa amani. Mungu atawapa amani wala hawatahangaika maishani mwao.

Zaburi 45 :1

“Furika kwa neno jema”.

Moyo kufurika kwa neno jema inamaanisha kuwa na roho safi. Maneno yanayotoka kwako ni mazuri/ mema wala siyo ya kusababisha maafa au dhiki, wala siyo ya kuudhi watu.

Zaburi 140:3.

“Wamenoa ndimi zao”.

Tunajua ya kwamba kitu chenye makali ndicho hunolewa. Ulimi hauwezi ukanolewa. Hii nahau inamaanisha watu walio tayari kugombana ama kutumia midomo yao kwa vita. Kunoa ndimi hapa inamaanisha kuwa tayari kwa vita vya midomo/ kuongea zaidi ya ipasavyo kwa minajili ya kuwaumiza wenzako.

Mithali 6:21.

“Jivike maagizo shingoni mwako”.

Sulemani alikuwa akitoa ushauri kwa mwanawe. Kumwambia ajivike maagizo shingoni mwake anamaanisha kwamba ayafuate/ ayatii maagizo wala asiyaache Ukivaa kitu shingoni, unatembea nacho kila uendapo, kwa hivyo kutii magizo inamaanisha kwamba kila alipo akumbuke hayo maagizo wala asiyaache.

Mithali 31: 20.

“Kuwakunjulia maskini mikono”.

Sulemani alikuwa akiongea kuhusu mke mwema alipoitaja hii nahau. Anasema kwamba mke mwema hufanya kazi kwa bidii na nyumba yake hujaa kila aina ya mahitaji nayo familia yake haikosi chochote. Huwakunjulia maskini mikono yake, kumaanisha kuwa huwasaidia walio na mahitaji.

**4.2.4 Ushairi simulizi**

Kwa mujibu wa Wamitila (2006), ushairi simulizi ni utanzu wa fasihi simulizi unaohusisha kuwasilishwa kwa njia ya mdomo kwa kuimba, kughani au kukariri. Matei (2011) anaeleza kwamba ushairi simulizi una vipera vitatu ambavyo ni nyimbo, ngonjera na maghani. Miruka (2013) anasema kwamba ushairi simulizi katika jamii nyingi hulingana au kuingiliana na nyimbo. Katika utafiti wake, alibainisha ushairi simulizi kama mojawapo ya maumbo makuu ya ya fasihi simulizi. Utafiti uliofanywa katika vitabu teule vya Biblia ulionyesha kwamba nyimbo na maghani zinajidhihirisha kwa wingi na ndivyo vipera tulivyovijadili.

#### 4.2.4.1 Maghani

Maghani ni aina ya tungo za ushairi zinazotolewa kwa maneno au kalima bila kuimbwa, (Wamitila 2005). Kulingana na Matei (2011), maghani ni hadithi ambayo husimulia sifa za mtu, kitu, mnyama, historia au tukio fulani. Aina za maghani ambazo ni tungo za kusifu huitwa sifo. Katika utafiti huu, maghani mbalimbali yalijitokeza yakiwemo pamoja na:

**Maghani ya kumsifu Mungu kwa utukufu wake.**

Zaburi 97:1-13.

> "BWANA ametamalaki, nchi na ishangilie,visiwa vingi na vifurahi. Mawingu na giza vyamzunguka, haki na hukumu ndio msingi wa kiti chake
> Moto hutangulia mbele zake, nao huwateketeza watesi wake pande zote.
> Umeme wake huangaza ulimwengu, nchi ikaona ikatetemeka.
> Milima iliyeyuka nta mbele za Bwana, mbele za Bwana wa dunia yote.
> Mbingu zimetangaza haki yake, na watu wote wameuona utukufu wake.
> Na waaibishwe wote waabuduo sanamu, wajivunao kwa vitu visivyofaa.
> Enyi Miungu yote, msujuduni yeye.
> Sayuni imesikia na kufurahi, binti za Yuda walishangilia,
> kwa sababu ya hukumu zako ee Bwana.
> Maana wewe, BWANA, ndiwe uliye juu, juu sana kuliko nchi yote;
> Umetukuka sana juu ya miungu yote. Enyi mpendao Bwana, uchukieni uovu;
> Huwalinda nafsi zao watauwa wake, Na kuwaokoa na mkono wa wasio haki.
> Nuru imemzukia mwenye haki, Na furaha wanyofu wa moyo.
> Enyi wenye haki, mfurahieni BWANA, Na kulishukuru jina lake takatifu."

Katika Zaburi hii, Daudi anamsifu Mungu kwa utukufu wake na maajabu yake. Anaendelea kusema kuwa Mungu ni mkuu na wa kuhofiwa kuliko Miungu yote. Ndiye aliyezifanya mbingu. Ni mwenye heshima, nguvu na uzuri na anastahili kusifiwa na kupewa utukufu na pia kuabudiwa kwa uzuri wa utakatifu wake. Hata ingawa haonekani, vitu ambavyo ameviumba vinaonekana wazi huku vikidhihirisha uwepo na uwezo wake.

Zaburi 117: 1 – 2

> "Haleluya, Enyi mataifa yote, msifuni BWANA,
> Enyi watu wote, mhimidini.

Maana fadhili zake kwetu sisi ni kuu,
Na uaminifu wa BWANA ni wa milele."

Hapa Daudi anawaita mataifa na watu wote kumsifu Bwana kwa sababu fadhili zake kwao ni kuu, na uaminifu wake ni wa milele. Kwa hivyo Mungu anasifiwa kwa kuwa mwenye fadhili na pia uaminifu.

Zaburi 89 : 6 – 13

"Maana ni nani katika mbingu awezaye kulinganishwa na BWANA?
Ni nani afananaye na BWANA miongoni mwa malaika?
Mungu huogopwa sana barazani pa watakatifu,
Ni wa kuhofiwa kuliko wote wanaomzunguka.
BWANA, Mungu wa majeshi, Ni nani aliye hodari kama Wewe, Ee YAHU?
Na uaminifu wako unakuzunguka.
Wewe ndiwe ukitawalaye kiburi cha bahari.
Mawimbi yake yainukapo, wayatuliza wewe.
Ndiwe uliyemseta Rahabu akawa kama aliyeuawa,
Kwa mkono hodari umewatawanya wakuchukiao.
Mbingu ni mali yako, nchi nayo ni mali yako,
Ulimwengu na vyote viujazavyo ndiwe uliyeupiga msingi wake.
Kaskazini na kusini ndiwe uliyeziumba, Tabori na Hermoni hulifurahia jina lako.
Mkono wako ni mkono wenye uweza, mkono wako una nguvu,
Mkono wako wa kuume umetukuka."

Mungu hawezi kulinganishwa na chochote, hata malaika hawawezi kufananishwa naye. Ni wa kuhofiwa na anaogopwa katika baraza la watakatifu. Anaendelea kueleza kwamba Mungu wa majeshi ni hodari na anazugukwa na uaminifu wake. Anatawala kiburi cha bahari kwa kutuliza mawimbi yanapoinuka. Kila kitu ni mali ya Mungu ikiwemo mbingu, nchi na vyote viujazao ulimwengu. Anakamilisha kwa kusema kwamba mkono wa Mungu una nguvu, unaweza yote na umetukuka. Huu ni mfano wa tungo za sifo kwani matteni (1989) anaeleza sifo kama tungo za kusifu.

**Maghani ya kumsifu Mungu kwa uumbaji wake.**

Zaburi 8:1-9

> "Wewe, MUNGU, Bwana wetu,
> jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote!
> Wewe umeuweka utukufu wako mbinguni;
> Vinywani mwa watoto wachanga na wanyonyao
> Umeiweka misingi ya nguvu;
> Kwa sababu yao wanaoshindana nawe,
> Uwakomeshe adui na mijilipiza kisasi.
> Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako,
> mwezi na nyota ulizoziratibisha.
> Mtu ni kitu gani hata umkumbuke,
> na binadamu hata umwangalie?
> Umemfanya mdogo punde kuliko Mungu
> Umemvika taji ya utukufu na heshima;
> umemtwaza juu ya kazi za mikono yako;
> Umevitia vitu vyote chini ya miguu yake.
> Kondoo na ng'ombe wote pia;
> Naam, na wanyama wa kondeni;
> Ndege wa angani, na samaki wa baharini,
> Na kila kipatacho njia za baharini.
> Wewe MUNGU, Bwana wetu,
> jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote!"

Mungu anasifiwa kwa utukufu wa Jina lake, amewakomesha wote wanaoshindana naye. Mwandishi anatazama mbingu na vyote vilivyoumbwa na Mungu na anashangaa ni kwa nini Mungu anamjali binadamu ilhali binadamu ni kazi ya mikono ya Mungu. Ni Mungu ndiye aliyetia vitu vyote chini ya utawala wa binadamu – ngombe, kondoo, ndege wa angani, samaki wa baharini na kila kilicho hai. Kweli Mungu ni Mkuu.

Haya ni maghani kwani baadhi ya sifa za maghani ni, hueleza matukio katika mpangilio fulani, huwa na wahusika, hutumia lugha kimaelezo na huwa na maudhui ya kweli au ya kubuni na yenye funzo fulani (Ndungo na Wafula, 1993). Hizi sifa zote zinajidhihirisha katika maghani haya, kwa mfano kuna mpangilio wa uumbaji wa nyota na mwezi na jinsi Mungu alivyoviweka vitu vyote chini ya ulinzi wa binadamu. Lugha ya kimaelezo imetumika hasa mwandishi anapoelezea jinsi Mungu alivyo mkuu na vile vile alivyoviweka vitu vyote alivyoviumba chini ya ulinzi wa binadamu.

Dhima ya maghani katika jamii ni pamoja na kudumisha utu wa wahusika; kutoa sifa nzuri ili ziigwe au zitumiwe kukosoa; kuchochea ari ya kutaka kuwa shujaa, na kudhihirisha uhodari wa kutenda Ipara na Waititu (2004). Katika maghani tiliyoshughulikia, tumeona jinsi Mungu anavyosifiwa na kudumishwa na kila kiumbe kama muumba wa vyote na wala hakuna anyeweza kulinganishwa naye. Aidha, jinsi anavyosifiwa Mungu inachochea watu kuiga sifa zake, ama kukosolewa kama anavyowaambia, wampendao Bwana wauchukie uovu, wamfurahie Bwana na kulishukuru jina lake takatifu. Mungu vilevile, amedhihirishwa kama hodari wa kutenda maana matendo yake yote ni makuu.

#### 4.2.4.2 Nyimbo

Nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi (Wamitila, 2003). Nyimbo huwa na mawazo mazito na hupaniwa kuonyesha uhusiano wa kijamii, mgogoro, kukejeli, kuliwaza, kuongoa na kuburudisha. Baadhi ya sifa za nyimbo ni pamoja na maneno yanayoimbwa au matini yenye mpangilio maalum; muktadha unaofungamana na wimbo, kwa mfano sherehe, ibada, kilio na kadhalika, pamoja na hadhira inayoimbiwa (Wamitila, 2003). Matteru (1987) anafafanua kwamba tanzu kama nyimbo na maghani ni tungo za fasihi simulizi zinazotumia mapigo kwa utaratibu maalum.

Peter (2012) katika utafiti wake ameweza kuonyesha jinsi nyimbo zilivyo baadhi ya vipera vya tanzu za fasihi simulizi. Alitambua aina nyingi za nyimbo zikiwemo bembezi, mbolezi, nyimbo za kisiasa, nyimbo za mapenzi, hodiya, tendi, nyiso, nyimbo za dini, harusi, tumbuizo na nyimbo

za kizazi kipya. Katika utafiti huu aina ya nyimbo zilizojidhihirisha sana ni zile za dini, hasa za kumsifu Mungu.

Zaburi 33: 1 – 9

> “Mpigieni BWANA vigelegele, enyi wenye haki,
> kusifu kunawapasa wanyofu wa moyo
> Mshukuruni BWANA kwa kinubi,
> Kwa kinanda cha nyuzi kumi mwimbieni sifa.
> Mwimbieni wimbo mpya,
> Pigeni kwa ustadi kwa sauti ya shangwe.
> Kwa kuwa neno la BWANA lina adili,
> Na kazi yake yote huitenda kwa uaminifu.
> Huzipenda haki na ukumu,
> Nchi imejaa fadhili za BWANA.
> Kwa neno la BWANA mbingu zilifanyika,
> Na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake.
> Hukusanya maji ya Bahari chungu chungu;
> Huviweka vilindi katika ghala.
> Nchi yote na imwogope BWANA,
> wote wakaao duniani na wamche.
> Maana Yeye alisema, ikawa; Na Yeye aliamuru, ikasimama.”

Huu ni wimbo wa kumsifu Mungu. Baadhi ya sifa za nyimbo zimejitokeza hapa kama vile kupiga vigelegele ambapo wenye haki wanahimizwa kumpigia Mungu vigelegele; kumsifu bwana kwa ala za muziki kama vile vinubi na vinanda vya nyuzi kumi. Hizi ni baadhi ya ala za muziki zinazotumika katika nyimbo. Vilevile tunaona watu wakihimizwa wamwimbie Bwana kwa kupiga hizo ala kwa ustadi na kwa sauti ya shangwe. Kwa ufupi, huu ni wimbo wa kumsifu Mungu na wanaomsifu wanahimizwa kufanya hivyo kwa shangwe na vigelegele. Mojawapo wa dhima ya nyimbo katika jamii ni kuburudisha. Kwa hivyo tunapoimba kwa shangwe na vigelegele huku tukicheza vinubi na vinanda, tunaburudisha na kutumbuiza wale wanaosikiliza.

Zaburi 136 : 1-15  Mshukuruni Mungu kwa maana fadhili zake ni za milele.

> “Mshukuruni BWANA kwa kuwa ni mwema;
> Kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Mshukuruni Mungu wa miungu;
> kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Mshukuruni Bwana wa mabwana,
> kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Yeye peke yake afanya maajabu makuu,
> kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Yeye aliyefanya mbingu kwa fahamu zake;
> kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Yeye aliyeitandaza nchi juu ya maji;
> kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Yeye aliyefanya mianga mikubwa;
> kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Jua litawale mchana;
> kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Mwezi na nyota zitawale usiku;
> kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Yeye aliyeigawa bahari bahari ya Shamu,
> kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Akawavusha Israeli katikati yake;
> kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Akamwangusha farao na jeshi lake katika bahari ya Shamu;
> kwa maana fadhili zake ni za milele”.

Huu ni mfano mzuri wa nyimbo. Ndungo na Wafula (1993) wanaeleza tendi kama utungo mrefu wenye kusimulia matukio ya kishujaa yenye uzito wa kijamii au kitaifa.  Matukio haya yanaweza kuwa ya kihistoria lakini tendi nyingi huchanganya historia na visakale au visasili.

Katika utafiti huu, Zaburi 136 ni mfano mzuri wa tendi. Unasimulia kisasili cha kuumbwa kwa ulimwengu, jinsi Mungu alivyofanya maajabu makuu kwa kuumba mbingu kwa fahamu zake na

kuweka kila kitu mahala pake bila kukosea popote. Anaendelea na historia ya wana wa Israeli jinsi walivyotolewa Misri, wakavuka bahari ya Shamu huku farao na jeshi lake likiangamia katika bahari hiyo; Jinsi alivyowaongoza wana a Israeli jangwani hata wakafika nchi aliyowaahidi kwa kuwapiga wafalme wakuu na kuwaondoa katika nchi zao ili ziwe urithi wa wana wa Israeli.

Mulokozi (1989) anaeleza utendi kama ushairi wa matendo ambao husimulia visa kwa kutumia mapigo ya kimziki, na visaidizi vinavyojenga milio ya aina. Baada ya kila mshororo katika wimbo huu tunapata kisaidizi,"kwa maana fadhili zake ni za milele", hadi mwisho wa wimbo wenyewe.

Zaburi 96:1-8

> "Mwimbieni bwana wimbo mpya, mwimbieni Bwana, nchi yote.
> Mwimbieni Bwana, libarikini jina lake lake,
> tangazeni wokovu wake siku kwa siku,
> wahubirini mataifa habari za utukufu wake,
> Na watu wote habari za maajabu yake,
> kwa kuwa Bwana ni mkuu mwenye kusifiwa sana,
> Na wa kuhofiwa kuliko miungu yote.
> Maana miungu yote ya watu si kitu,
> Lakini Bwana ndiye aliyezifanya mbingu.
> Heshima na adhama ziko mbele zake,
> nguvu na uzuri zimo katika patakatifu pake.
> Mpeni Bwana utukufu na nguvu.
> Mpeni wa jina lake, leteni sadaka mkaziingie nyua zake".

Wimbo huu unawahimiza watu wamwimbie Bwana wimbo mpya kwa kutangaza habari za maajabu yake na kumpa utukufu anaostahili. Ipara na Waititu (2004) wanaeleza muundo wa nyimbo kuwa; mistari huwa na silabi zenye mapigo ya kimziki na kwamba mafungu au mistari yaweza kurudiwa rudiwa. Katika wimbo huu, mistari kama mwimbieni Bwana na mpeni Bwna imerudiwa rudiwa. Aidha wanaeleza kwamba uimbaji unaweza kuwa na hadhira inayoonekana

au isiyoonekana. Ni dhahiri kwamba katika wimbo huu kuna hadhira kwani kiongozi wa wimbo anaihimiza hadhira kumwimbia bwana – ‘Mwimbieni Bwana, tangazeni wokovu wake siku kwa siku’.

Zaburi 118: 1 – 4

> “Haleluya. Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema,
> kwa maana fadhili zake ni za milele.
> Israeli na aseme sasa,
> ya kwamba fadhili zake ni za milele.
> Wamchao Bwana na waseme,
> Fadhili zake ni za milele.”

Wimbo huu ni wa kumshukuru Bwana kwa wema na fadhili zake za milele. Katika wimbo huu, kuna kiongozi na waimbaji ambapo unaimbwa kwa kupokezana. Kiongozi anaimba sehemu ya kwanza nao waimbaji wanajibu, ya kwamba fadhili zake ni za milele.

Zaburi 150 :

Wimbo wa kumsifu Mungu kwa vyombo vya muziki.

> “ Haleluya. Msifuni Mungu katika patakatifu pake;
> Msifuni katika anga la uweza wake.
> Msifuni kwa matendo yake makuu;
> Msifuni kwa kadiri ya wingi wa ukuu wake.
> Msifuni kwa mvumo wa baragumu;
> Msifuni kwa kinanda na kinubi.
> Msifuni kwa matari na kucheza;
> Msifuni kwa zeze na filimbi.
> Msifuni kwa matoazi yaliayo;
> Msifuni kwa matoazi yaliayo sana.
> Kila mwenye pumzi na amsifu Bwana. Haleluya!

Ipara na Waititu (2004) wanaeleza baadhi ya sifa za nyimbo kama kucheza ala za muziki. Hapa tunaona ala mbalimbali za muziki zikichezwa na aidha tunawaona waimbaji wakisifu kwa matari na kucheza. Wamitila (2003) anaeleza kwamba nyimbo zinapoambatana na ala za muziki, aina hizo huwa msingi mkuu wa kugawa aina mbalimbali ya ngoma au nyimbo za wahusika; aidha hutambulisha jamii fulani. Inaonekana kwamba jamii ya Waisraeli ilikuwa ikitumia sana vyombo kama vile baragumu, vinubi, matari, zeze, filimbi na matoazi.

**4.3. Mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia**.

Mwingiliano matini kwa mujibu wa Senkoro (2011) ni ule uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya fasihi. Kuingiliana kwa matini katika kazi za fasihi kunamaanisha kazi moja ya kifasihi kuwa na sifa za tanzu nyingine ndani mwake. Mulokozi (1989) anasema kwamba mojawapo ya sifa kuu za fasihi simulizi ni vipera vyake kuingiliana katika utendaji; hivyo swala la mwingiliano matini ni mojawapo ya mitindo ya kifasihi.

Wamitila (2003) anaeleza kwamba tanzu za fasihi simulizi huingiliana kwa kiasi kikubwa sana. Kwa mfano, methali inaweza kuwa kitendawili na kitendawili kuwa methali. Inawezekana kitendawili kikaundwa kutokana na methali na kwa njia hii kuwa kama njia ya kufundishia methali yenyewe. Aidha, katika utambaji wa hadithi, nyimbo hutumiwa kwa kiasi kikubwa ili kuonyesha na kusisitiza kiini au wazo kuu katika hadithi au simulizi inayohusika. Pia nyimbo huingizwa katika hadithi kuongeza uhai wa usimulizi kwa kushirikisha hadhira hasa ikiwa ni hadhira tendi. Vilevile, hadithi huwa na ufundi wa kisanaa ambao hujitokeza kwa matumizi ya lugha yenye mvuto na iliyochanganya matumizi ya tamathali mbalimbali za semi kama vile tashbihi, methali, takriri na istiara.

Kwa kuchunguza mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia, utafiti huu ulichunguza jinsi maumbo ya fasihi simulizi yanavyojitokeza katika Biblia na uhusiano unaojitokeza katika maumbo haya kati ya matini za fasihi simulizi na matini za Biblia. Maumbo haya yalijitokeza kama hadithi/ masimulizi, maigizo, ushairi simulizi na semi/ tanzu bainifu, baada ya kusoma jumla ya vitabu saba vya Biblia na kukusanya data na kuipanga kulingana na maumbo. Baadaye uchunguzi ulibaini kuwa kuna mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini za Biblia.

#### 4.3.1 Mwingiliano matini kwa kuzingatia mtindo.

Ujenzi wa vitabu katika Biblia ulitokana na masimulizi/ mitindo tofauti ya maelezo yanayochukua maumbo ya kimasimulizi; kwa mfano, hadithi, nyimbo na tamathali za usemi. Escarpit (1973) anasema kwamba fasihi lazima ichukuliwe kama ilivyo na uhusiano usiotatanika na maisha ya jamii. Fasihi ni taasisi ya kijamii inayotumia lugha kama mtambo wake. Isitoshe, fasihi huwasilisha maisha. Hivi ndivyo matini za Biblia zilivyo. Hutumia lugha kuwasilisha maisha ya binadamu. Kwa mfano, utungo wa kwanza katika Biblia unasimulia mwanzo wa dunia, ukitumia umbo la hadithi. Mojawapo wa sifa za kimtindo za hadithi ni kuwa na muundo maalum. Wamitila (2003) anaeleza kwamba katika muundo, tunaangalia jinsi matukio ya hadithi yalivyopangwa kuanzia mwanzo kwenye kitangulizi, kisha mvutano wa hadithi unaoendeleza mgogoro kati ya wahusika walioko, hadi kwenye kilele cha hadithi au upeo na hatimaye mwisho wake.

Katika kitabu cha *Mwanzo 1:1-31-2:4*, tunasoma kisa/ hadithi ya kuumbwa kwa dunia. Mwandishi kama ilivyo kawaida katika fasihi simulizi anaanza kwa kitangulizi 'hapo mwanzo' kuonyesha kwamba hadithi yake imeanza. Tunamwona akiendeleza hadithi yake kuhusu Mungu kuumba nuru na giza, Mbingu, nchi na majani, mianga,viumbe wenye uhai wakiwemo wanyama, kisha kukawa na kilele cha hadithi ambapo binadamu aliumbwa kwa mfano wake Mungu, Mwanzo 1:26, Mungu akasema, *"Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; Wakatawale samaki wa baharini na ndege wa angani, na wanyama na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba. Mwanaume na mwanamke aliwaumba".* Baada ya kilele cha hii hadithi, yaani kuumbwa kwa binadamu, tunaona mwisho wa hadithi katika Mwanzo 2:4 – "Hivyo ndivyo vizazi vya mbingu na nchi vilivyoumbwa"

Vilevile, katika *Mwanzo 27:27-29*, tunaona matumizi ya ushairi simulizi katika hadithi. Uhusiano kati ya matini za Biblia na fasihi simulizi unajitokeza wazi kwani tunapochunguza matini haya ya Biblia katika hicho kitabu tulichotaja, tunaona hadithi ya jinsi Yakobo alivyomhadaa babake hata akachukua Baraka za nduguye Esau. Katika hiyo hadithi, Isaka

babake Yakobo anatumia ushairi simulizi kumbariki Yakobo; "Akakaribia akambusu. Naye akasikia harufu ya mavazi yake, akambariki akasema,

Tazama, harufu ya mwanangu
Ni kama harufu ya shamba alilolibariki Bwana.
Mungu na akupe ya umande wa mbingu,
Na manono ya nchi
Na wingi wa nafaka na mvinyo, mataifa na wakutumikie
Na makabila wakushujudie
Uwe Bwana wa ndugu zako,
Na wana wa mama yako na,
Wakusujudie.
Atakayekulaani alaaniwe,
Na atakayekubariki abarikiwe.

Katika kitabu cha Luka 3:1-21, tunamwona Yohana mbatizaji akitoa mawaidha kwa wale waliokuja kubatizwa naye. Katika mawaidha yake, anatumia masimulizi pamoja na wimbo ndani yake. Luke 3: 4 – 6;

Sauti ya mtu aliaye nyikani,
Itengezeni njia ya Bwana
Yanyosheni mapito yake.
Kila bonde litajazwa
Na kila mlima na kilima
Kitashushwa
Palipopotoka patakuwa
Pamenyoka
Na palipoparuza patatainshwa
Na wote wenye mwili watavuna
Wokovu wa Mungu

Katika huo wimbo aidha kuna mafumbo. Hili fumbo linawahimiza watu kupitia *"Sauti iliayo nyikani*" yaani Yohana mbatizaji. Watengeneze njia zao.Waache maovu kwani wasipofanya hivyo hawatauona wokovu wa Mungu.

Sifa nyingine ya mtindo katika fasihi simulizi ni urudiaji/ takriri. Takriri kwa mujibu wa Wamitila (2003) inaweza kuwa na vipengele vya muundo kama, virai maneno, sentensi, vifungu fulani na kadhalika. Takriri katika fasihi simulizi hufanya mambo yanayozungumziwa kukumbukika, na pia, ni njia moja ya kusisitiza jambo fulani. Kwa mfano, katika kitabu cha

Zaburi 103:1-2 mwandishi anarudia rudia kifungu ‘Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA’. Hapa anajaribu kusisitiza kile ambacho kinafaa kumhimidi Bwana, yaani ‘nafsi yake.’Aidha, katika Zaburi 89:13,

> Mkono wako ni mkono wenye uweza
> Mkono wako una nguvu
> Mkono wako wa kiume
> Umetukuka.

Maneno ‘mkono wako’ yamerudiwa katika msitari ili kusisitiza uwezo au nguvu zake Mwenyezi Mungu.

Vilevile, katika fasihi simulizi mojawapo wa sifa za kimtindo ni kuwa na wahusika ambao wanaweza kuwa binadamu au wanyama. Katika usimulizi wa hadithi, binadamu wanaweza kuingiliana, kujadiliana, kuzungumza na kuhusiana kwa jumla na wanyama.
Katika mwanzo 2:1-5, tunashuhudia mazungumzo kati ya binadamu na nyoka.

> “Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwanamke akamwambia nyoka, matunda ya miti ya bustanini tunaweza kula; Lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, msiyale wala msiyaguze, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu,mkijua mema na mabaya”

Hapa tunashuhudia mwingiliano wa ajabu kati ya mwanamke na nyoka. Hakuna mpaka wowote kati ya mwanamke huyu na nyoka. Nyoka amesawiriwa kama mnyama kwani anamdanganya mwanamke naye anakubaliana naye kama kwamba anaongea na binadamu mwenzake.

Sifa nyingine ya kimtindo katika fasihi simulizi ni matumizi ya tamathali za usemi au mbinu bainifu. Haya ni matumizi ya lugha yenye mvuto iliyochanganya semi kama vile tashbihi, sitiari, methali, vitendawili, tashhisi na nahau. Hizi semi zimetumiwa mara nyingi sana katika vitabu teule vya Biblia vilivyochanganuliwa, hasa katika vitabu vya Zaburi na methali, Mathayo na

Luka. Baadhi ya semi zilizojitokeza na zinazoonyesha mwingiliano taaluma ni pamoja na tashhisi.

Zaburi 97: 1.

"Nchi na ishangilie, visiwa vingi na vifurahi".

Zaburi 98:7-8.

"Bahari ivume: mito ipige makofi; milima iimbe pamoja kwa furaha".

Mithali 6:22.

"Maagizo yatakulinde ulalapo, uamkapo yatazungumza nawe".

Mithali 7:4.

"Mwambie hekima wewe ndiwe umbu langu, Mwite ufahamu jamaa yako mwanamke".

Hizo ni baadhi ya tashhisi zinazoonyesha mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia. Aidha, katika fasihi simulizi methali zilitumika sana kama tamathali za semi na pia kama kipera cha fasihi simulizi. Muundo wa methali unaweza kutumia mbinu maalum za lugha au kishairi. Methali za jamii mbalimbali aidha hufanana. Ndiposa tunapata methali mbalimbali katika Biblia zinazofanana na zile methali za jamii mbalimbali za kiafrika hasa Methali za Kiswahili. Hii inadhihirisha jinsi matini za fasihi simulizi zinavyoingiliana na matini za vitabu teule za Biblia. Baadhi ya mifano ni pamoja na:

Mithali 14: 4.

"Zizi ni safi ambapo hapana ng'ombe, bali nguvu za ng'ombe zaleta faida nyingi

Mithali 16:18.

"Kiburi hutangulia angamivu".

Mithali 21:17.

"Mtu apendaye anasa atakuwa maskini"

Mithali 27:10.

"Afadhali jirani aliye karibu kuliko ndugu aliye mbali".

Mithali 17:17.

"Rafiki hupenda siku zote, na ndugu amezaliwa kwa siku ya taabu".

#### 4.3.1.1 Mtindo wa ishara na taswira.

Ishara ni matumizi ya vitu fulani kusimamia vingine, yaani kuashiria vitu vingine tofauti. Taswira kwa upande mwingine ni kule kuitumia lugha ambayo inamfanya msikilizaji au hadhira iweze kuunda picha akilini. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) Picha zinazopatikana huweza kulenga hisia tofauti tofauti. Kuna picha zinazochochea kutazama, kunusa, kuonja na hata kusikia. Kutokana na msingi huu, tunapata aina mbalimbali za taswira, kama vile; taswira za uoni ambapo picha inayojengwa inalenga mtazamo wa macho; taswira ya mnuso/ harufu inayolenga viungo vya harufu; taswira ya usikivu inayolenga hisia za kusikia kwa kujenga picha inayohusiana na sauti, pamoja na taswira zingine. Katika kitabu cha 2 Wafalme, kuna hadithi ya jinsi njaa ilivyokuwa katika nchi ya Samaria ambapo watu walikuwa wanawakula hata watoto wao.

2Wafalme 6:26 – 30.

> "Ikawa mfalme wa Israeli alipokuwa akipita ukutani mwanamke mmoja akamwita akisema, unisaidie, Bwana wangu mfalme. Mfalme akamwambia, una nini? Akamjibu, mwanamke huyu aliniambia, mtoe mtoto wako, tumle leo, na mtoto wako tutamla kesho. Basi tukamtosa mtoto wangu, tukamla; Nikamwambia siku ya pili, mtoe mtoto wako tumle; naye amemficha mtoto wake. Ikawa mfalme alipoyasikia maneno ya huyo mwanamke, aliyararua mavazi yake, na watu wakaona, na tazama, alikuwa amevaa magunia ndani mwilini mwake".

Hapa taswira ya hicho kisa inajitokeza waziwazi. Tunaona picha ya hawa wanawake wawili wakielewana, kisha wanamchinja mtoto wa mwanamke wa kwanza na kumla. Baadaye picha ya huyu mwanamke wa pili inajitokeza akiwa amemficha mwanawe na huyu mwingine analalama hadi kumwendea nabii ambaye naye anararua nguo zake. Kwa jumla tumeona jinsi matini za fasihi simulizi zinavyoingiliana na matini za vitabu teule vya Biblia kimtindo.

### 4.3.2. Mwingiliano matini kwa kuzingatia sifa za fasihi simulizi katika Biblia

Kwa mujibu wa Tuki (2004), fasihi simulizi ni kazi ya fasihi inayohifadhiwa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo kama vile hadithi, ngano na vitendawili. Mojawapo ya sifa za fasihi simulizi ni kwamba hutumia mazungumzo ikihusisha

utendaji na njia nyingine za mawasiliano ili kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Aidha, fasihi simulizi huwasilishwa kwa hadhira iliyo hai. Harper (1988) naye anaeleza kwamba waandishi wa kiyahudi waliaminika kupitisha ujumbe kupitia kwa mafunzo simulizi. Haya mafunzo yalipitishwa kwa njia ya mdomo. Hata neno la Mungu lilipitishwa kwa njia ya mdomo kwa karne kadha kabla ya kuwekwa katika maandishi. Katika utafiti huu, ilibainika wazi kuwa baadhi ya kazi zilizomo katika Biblia ziliwasilishwa kwa njia ya mdomo na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Katika kitabu cha Mwanzo 24:1-9, lbrahimu anamwambia mtumishi wake aende amtwalie mwanawe Isaka bibi kutoka kwa nchi yake na watu wake aliowaacha akienda katika nchi ya Kanani aliposhauriwa na Mungu. Ibrahimu akamwambia mtumishi wake, mzee wa nyumba yake, *"…………tafadhali uutie mkono wako chini ya paja langu***,** *nami nitakuapisha kwa Bwana Mungu, kwamba hutamtwalia mwanangu mke katika binti za wakanani ambao nakaa kati yao, bali enenda hata nchi yangu, na kwa jamaa zangu, ukamtwalie mwanangu Isaka mke."* Kwa jinsi alivyowajua wakanaani, Ibrahim, hata ingawa alikuwa akiishi kati yao, alielewa mila, desturi na itikadi zao zilikuwa tofauti na zao ndiposa asingependelea mwanawe aoe kutoka kwa hao watu. Hiyo mila na desturi imerithishwa Isaka ambapo anapozeeka, anamwita Yakobo mwanawe na kumfanya kuoa mke kutoka kanani.

Mwanzo 28 :1-3

> "Basi Isaka akamwita Yakobo akambariki, akamwagiza akamwambia, usitwae mke wa binti za Kanani. Ondoka uende padan – aramu, mpaka nyumba ya Bethueli, baba ya mama yako. Na mungu Mwenyezi akubariki, akuzidishe, na kukuongesha, ili uwe mkutano wa makabila".

Isaka alimwagiza Yakobo aende aoe kutoka kwa nyumba ya mama yake wala sio kwa wakanani. Yeye Yakobo alipokaribia kufa akiwa kafika nchi ya Misiri, aliwaiita wanawe na baada ya kuwabariki akawaamuru kwamba baada ya kifo chake waende wamzike pamoja na baba zake katika shamba alilonunua Ibrahim.

Mwanzo 49:29 –31.

> "Akawaamuru akasema, mimi ninakwenda kukusanywa pamoja na watu wangu. Mnizike pamoja na watu wangu, mnizike pamoja na baba zangu, katika pango iliyomo shambani mwa Efroni aliyoinunua Ibrahim pawe milki yake ya kuzikia. Humo walimzika Ibrahim na Sara mkewe; Isaka na Rebeka mkewe; nami humo nikamzika Lea".

Vilevile Yusufu alipokaribia kufa aliwaambia nduguze katika kitabu cha Mwanzo;

Mwanzo 50:24,

> "Mimi nakuja, lakini Mungu atawajia ninyi bila shaka, atawapandisha toka nchi hii. Mpaka nchi aliyowaapia Ibrahim, na Isaka na Yakobo.Yusufu akawaapisha wana wa Israeli akasema, Bila shaka Mungu atawajia ninyi, nanyi mtaipandisha mifupa yangu. Basi Yusufu akafa".

Hapa tumeona jinsi fasihi simulizi inavyoingiliana na Biblia. Kuna kule kurithishwa kwa mila na desturi kutoka kizazi hadi kizazi, ambapo imeanzia kwa Ibrahim ambaye amerithisha kwa Isaka, Yakobo na hatimaye Yusufu. Na wote tunaona wakiwasilisha ujumbe wao kwa njia ya mdomo. Hivyo ndivyo ilivyo katika fasihi simulizi kwani lilikuwa jukumu la wazee kurithisha fasihi yao kutoka kizazi hadi kingine. Vilevile, hadhira inayozungumziwa katika beti hizi zote ni ile iliyo hai, ambayo ni moja wapo wa sifa za fasihi simulizi.

#### 4.3.3 Mwingiliano matini kwa kuzingatia dhima ya fasihi simulizi katika jamii.

Fasihi simulizi ni sanaa ya lugha inayoshughulikia maswali yanayomhusu binadamu, matatizo yake, matumaini yake, migogoro yake, na jinsi anavyoingiliana na mazingira yake. Fasihi ilianza kama njia ya kujifahamu kwa binadamu. Katika kutekeleza hili, fasihi hiyo ilimburudisha binadamu na kumpa elimu, ujitambuaji na ujijuaji, ujamiishaji na ujijuaji,ujamiishaji na ukuzaji wa stadi za lugha (Wamitila, 2003). Katika uchunguzi huu, hayo majukumu ama dhima ya fasihi katika jamii yamejitokeza wazi kupitia kwa maumbo ya fasihi simulizi yaliyodhirika katika Vitabu vilivyosomwa.

##### 4.3.3.1 Kuburudisha

Mojawapo wa dhima ya fasihi simulizi katika jamii ni kuburudisha. Tanzu kama hadithi, Ushairi, Semi na maigizo huweza kutumiwa kuburudisha wanaohusika. Mfano;

Zaburi 33:1-3

“Mpigieni Bwana vigelegele,
Enyi wenye haki
Kumsifu kunawapasa
wanyofu wa moyo
Mshukuruni Bwana kwa kinubi,
kwa kinanda cha nyuzi kumi mwimbieni sifa.
Mwimbieni wimbo mpya,
Pigeni kwa ustadi kwa
Sauti ya shangwe.”

Huu wimbo bila shaka ni wa burudani. Kwa kawaida wimbo unapoimbwa kwa vigelegele na kucheza ala za muziki huwa unatumbuiza.Tunaona kinubi, kinanda cha nyuzi kumi vikichezwa kwa ustadi kwa sauti ya shangwe. Wote wanaosikiza bila shaka wanaburudika, na hiyo ni mojawapo ya dhima ya fasihi simulizi. Kwa hivyo fasihi simulizi na matini za Biblia zinaingiliana kwa kuzingatia dhima ya kuburudisha.

Robert (1981) katika usuli uk. 5 anaeleza kwamba Biblia inazo hadithi za kuvutia na lugha yenye mvuto, kumaanisha ya kwamba inayo dhima ya kuburudisha. Katka Luka 16:19 – 31, Biblia inasema, *“Palikuwa na mtu mmoja tajiri, aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na kitani safi, na kula siku zote kwa anasa. Na maskini mmoja, jina lake Lazaro, huwekwa mlangoni pake, ana vidonda vingi, naye alikuwa akitamani kushibishwa kwa makombo yaliyoanguka kwa meza ya yule tajiri, hata mbwa wakaja wakamramba vidonda vyake. Ikawa Yule maskini alikufa akachukuliwa na malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa akazikwa. Basi kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Ibrahimu kwa mbali, na Lazaro kifuani mwake. Akalia akasema, Ee baba Ibrahimu, nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, auburudishe ulimi wangu, kwa sababu ninateswa katika moto huu. Ibrahimu akasema, mwanangu, kumbuka ya kwamba wewe uliyapokea mambo yako mema katika maisha yako, na Lazaro vivyo alipata mabaya; na sasa yeye yupo hapa anafarijiwa na*

*wewe unaumizwa. Na zaidi ya hayo kati yetu sisi na nyinyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze, wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu. Akasema, basi baba, nakuomba, umtume nyumbani kwa baba yangu, kwa kuwa ninao ndugu watano, ili awashuhudie, wasije wao pia wakafika mahali hapa pa mateso. Ibrahimu akasema, wanao Musa na manabii; na wawasikilize wao. Akasema, la baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu, watatubu. Akamwambia, wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu.''*

> Hii ni hadithi ya tajiri na Lazaro. Tukitazama mwanzo, ameanza jinsi ilivyo kawaida ya hadithi, kudhihirisha usanii wake. ''Palikuwa na mtu mmoja tajiri aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na kitani safi, na kula siku zote kwa anasa. Na maskini mmoja, jina lake Lazaro, huwekwa mlangoni pake; ana vidonda vingi, naye alikuwa akitamani kushibishwa kwa makombo yaliyoanguka katika meza ya yule tajiri, hata mbwa wakaja wakamramba vodonda vyake…..

Msanii ameiteka hadhira kutoka mwanzo wa hadithi yake ambayo ni ishara ya burudani. Mojawapo ya sifa za mtambaji ni kuwa na uwezo wa kujenga taharuki. Tunaona yule tajiri jinsi alivyojivaa vizuri na kuishi maisha ya anasa. Aidha, kinyume naye tunamwona maskini hohehahe aliyejaa vidonda mwilini. Pengine swali la balagha linalojitokeza hapa ni; Ni vipi tajiri akamruhusu maskini mchafu hivi mlangoni pake? Hii inaonyesha jinsi tayari mwandishi ameiteka hadhira ambayo itabidi ifuatilie hadithi yake ilivyo kawaida ya burudani. Mwishoni mwa hadithi tumeachwa katika hali ya taharuki:

> **"**Basi nakuomba umtume nyumbani kwa baba yangu, kwa kuwa ninao ndugu watano, ili awashuhudie, wasije wao pia wakafika mahali hapa pa mateso. Ibrahimu akasema, wanao musa na manabii, na wawasikilize wao. Akasema, La, baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu, watatubu. Akamwambia, wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishiwa hata mtu akifufuka katika wafu".

Hatujui mambo yaliendelea vipi? Ikiwa mwishowe Ibrahimu alikubali kumtuma maskini ama alimuacha tu tajiri ateseke milele. Hii inadhihirisha jinsi hadithi hii ilivyo ya kuburudisha. Mwandishi ameiburudisha hadhira yake kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi.

#### 4.3.3.2. Kuelimisha

Wamitila (2003) anaeleza kuwa katika jamii ambapo mfumo wa kimaandishi haujashika sana, fasihi simulizi inakuwa njia kuu ya kuelimishana. Wanajamii hupitisha thamani za kijamii, historia yao, utamaduni na mtazamo wao kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Msokile (1993) ilivyoelezwa katka usuli uk. 6 anasema kwamba mhakiki wa fasihi simulizi husaidia katika ujenzi wa jamii kwa kuzingatia maadili, ujumbe, falsafa na jumla ya kazi inayohusika. Dhima yake ni ile ya kufunza, kuonya, kutahadharisha na kuadilisha. Katika kitabu cha 1 Wafalme 2:1-4, Daudi anamshauri mwanawe sulemani:

> "Basi siku ya kufa kwake Daudi ikakaribia, akamwusha Sulemani mwanawe, akasema, mimi naenda njia ya ulimwengu wote; basi uwe hodari ujionyeshe kuwa mwanamume. Uyashike mausia ya Bwana Mungu wako, uende katika njia zake uzishike sheria zake, amri zake, hukumu zake na shuhuda zake sawasawa na ilivyoandikwa katika torati ya Musa, upate kufanikiwa katika kila ufanyalo, na kila utazamako, ili Bwana afanye imara neno lake alilonena kwa habari yangu, akisema, ikiwa watoto wako wataiangalia njia yao wakienda mbele zangu kwa kweli, kwa moyo wao wote, na kwa roho yao yote, hutakosa mtu katika kiti cha enzi cha Israeli".

Hapa Sulemani anaelimishwa kuhusu uongozi wake na umuhimu wa kushika sheria za Mungu. Anapewa mwelekeo na Daudi babaye jinsi alivyoelelezwa kupitia kwa torati ya Musa ambayo ilifunzwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Ni bayana kuwa fasihi simulizi na matini za Biblia zinaingiliana kupitia dhima hii ya kuelimisha.

#### 4.3.3.3 Kuhifadhi historia.

Fasihi simulizi ni nyenzo kuu ya kuhifadhi amali muhimu za jamii. Aidha wanajamii wanaweza kuijua historia yao, wao ni nani na wanatoka wapi, kutokana na fasihi simulizi. Maarifa haya ni muhimu kwa kuwa yanamsaidia mwanajamii sio tu kujielewa, bali pia kujitambua. Kristeva (1986) katika misingi ya nadharia anasema kwamba matini ni sehemu muhimu ya historia; kwamba matini hujengwa upya, hutilia mkazo na ni mangwi wa matini za awali hivyo hujenga historia ya kuchangia mabadiliko mengi katika matini huku zikitaazamia kujenga matini za baadaye.

1Wafalme 8:1-3, 12-21. Historia ya ujenzi wa nyumba ya Bwana.

> "Ndipo Sulemani alipowakusanya wazee wa Israeli, na wakuu wote wa kabila, wakuu wa mbari za mababa wa wana wa Israeli, wamwendee mfalme Sulemani huko Yerusalemu, ili walipandishe sanduku la agano la BWANA kutoka mji wa Daudi, yaani Sayuni. Wakakutana mbele ya mfalme Sulemani watu wote wa Israeli wakati wa siku kuu, katika mwezi wa Ethanimu, ndio mwezi wa saba. Wazee wote wa Israeli wakaja, nao makuhani wakajitwika sanduku. Wakalipandisha sanduku la BWANA, na ile hema ya kukutania, na vyombo vitakatifu vyote vilivyokuwa katika ile hema; vitu hivyo makuhani na Walawi wakavipandisha. Ndipo Sulemani akanena, BWANA na alisema ya kwamba atakaa katika giza nene. Hakika nimekujengea nyumba ya kukaa, iwe mahali pa makao yako milele. Mfalme akageuza uso wake akawabariki mkutano wote wa Israeli; na mkutano wote wa Israeli wakasimama. Akasema, BWANA, Mungu wa Israeli, ahimidiwe aliyenena na Daudi baba yangu kwa kinywa chake akalitimiza kwa mkono wake, akasema, Tokea siku ile nilipowatoa watu wangu Israeli katika Misri, sikuchagua mji wowote katika kabila zote za Israeli ili kujenga nyumba, jina langu liwe hapo; lakini nalimchagua Daudi awe juu ya watu wangu Israeli. Basi ilikuwa moyoni mwa Daudi, baba yangu, kujenga nyumba kwa jina la BWANA, Mungu wa Israeli. Lakini BWANA akamwambia Daudi baba yangu, kwa kuwa ilikuwa moyoni mwako kujenga nyumba kwa jina langu, ulifanya vizuri kuwaza hivi moyoni mwako. Lakini wewe hutanijengea nyumba hiyo; ila mwanao atakayetoka katika viuno vyako, yeye ndiye atakayeijenga nyumba kwa jina langu. Basi BWANA amelitimiza neno lile alilolinena, nami nimesimama mahali pa Daudi baba yangu, na kuketi katika kiti cha enzi cha Isrraeli, kama BWANA na alivyoahidi, nami nimejenga nyumba kwa jina la BWANA, Mungu wa Israeli. Na humo sanduku hili nimelifanyizia mahali, ambalo ndani yake mna maagano ya BWANA, aliyoyafanya na baba zetu, hapo alipowatoa katika nchi ya Misri."

Hapa tunaona Biblia kama historia simulizi. Sulemani anawafahamisha wana wa Israeli jinsi baba yake Daudi alivyopanga moyoni mwake kumjengea Mungu nyumba lakini Mungu mwenyewe akaamua kwamba ijengwe na Sulemani. Sulemani anawakumbusha historia yao; jinsi Mungu alivyowatoa katika nchi ya Misri na maagano aliyoyafanya na baba zao alipowatoa

huko Misri. Ni sawa na anavyosema Mulokozi (1996) kwamba fasihi simulizi huhifadhiwa kwa kichwa na kusambazwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo kupitia maumbo tofauti tofauti.

Zaburi 105:4- 45. Historia ya wana wa Israeli.

“Mtakeni BWANA na nguvu zake,
utafuteni uso wake siku zote.
Zikumbukeni ajabu zake alizozifanya,
Miujiza yake na hukumu yake na hukumu za kinywa chake.
Enyi wazao wa Ibrahimu, mtumishi wake;
Enyi wana wa Yakobo,wateule wake.
Yeye, BWANA, ndiye Mungu wetu;
Duniani mwote mna hukumu zake.
Analikumbuka agano lake milele;
Neno lile aliloviamuru vizazi elfu.
Agano alilofanya na Ibrahimu,
Na uapo wake kwa Isaka.
Alilomthibitishia Yakobo liwe amri,
Na Israeli liwe agano la milele.
Akisema, Nitakupa wewe nchi ya Kanaani,
Iwe urithi wenu mliopimiwa.
Walipokuwa watu wawezao kuhesabiwa,
Naam, watu wachache na wageni ndani yake;
Wakatanga-tanga toka taifa hata taifa,
Toka ufalme mmoja hata kwa watu wengine.
Hakumwacha mtu awaonee,
Hata wafalme aliwakemea kwa ajili yao.
Akisema, Msiwaguse masahii wangu,
Wala msiwadhuru nabii zangu.
Akaiita njaa iijilie nchi,
Akakiharibu chakula chote walichokitegemea.
Alimpeleka mtu mbele yao,Yusufu aliuzwa utumwani.

Walimwumiza miguu yake kwa pingu,
Akatiwa katika minyororo ya chuma.
Hata wakati wa kuwadia neno lake,
Ahadi ya BWANA ilimjaribu.
Mfalme alituma watu akamfungua,
Mkuu wa watu akamwachia.
Akamweka kuwa bwana wa nyumba yake,
Na mwenye amri juu ya mali zake zote.
Awafunge masheki wake kama apendavyo,
Na kuwafundisha wazee wake hekima.
Israeli naye akaingia Misri,
Yakobo akawa mgeni katika nchi Hamu.
Akawajalia watu wake wazae sana,
Akawafanya kuwa hodari kuliko watesi wao.
Akawageuza moyo wawachukie watu wake,
Wakawatendea hila watumishi wake.
Akamtuma Musa, mtumishi wake,
Na Haruni ambaye amemchagua.
Akaweka mambo ya ishara zake kati yao,
Na miujiza katika nchi ya Hamu.
Alituma giza, kukafunga giza, wala hawakuyaasi maneno yake.
Aliyageuza maji yao yakawa damu,
Akawafisha samaki wao.
Nchi yao ilijaa vyura,
Vyumbani mwa wafalme wao.
Alisema, kukaja makundi ya mainzi,
Na chawa mipakani mwao mwote.
Badala ya mvua aliwapa mvua ya mawe,
Na moto wa miali katika nchi yao.
Akaipiga mizabibu yao na mitini yao,
Akaivunja miti ya mipaka yao.

Alisema,kukaja nzige,
Na tunutu wasiohesabika;
Wakaila miche yote ya nchi yao,
Wakayala matunda ya ardhi yao.
Akawapiga wazaliwa wa kwanza katika nchi,
Malimbuko ya nguvu zao.
Akawatoa hali wana fedha na dhahabu,
Katika kabila zao asiwepo mwenye kukwaa.
Misri ilifurahi walipoondoka,
Maana, kwa ajili yao hofu imewaangukia.
Alitandaza wingu liwe funiko,
Na moto utoe nuru usiku.
Walipotaka akaleta kware,
Akawashibisha chakula cha mbinguni.
Akaufunua mwamba, kukabubujika maji,
Yakapita pakavuni kama mto.
Maana alilikumbuka neno lake takatifu,
Na Ibrahimu, mtumishi wake.
Akawatoa watu wake kwa shangwe,
Na wateule wake kwa nyimbo za furaha.
Akawapa nchi za mataifa,wakairithi kazi ya watu;
Ili wazishike amri zake, na kuzitii sheria zake.
Haleluya."

Daudi katika huu wimbo, anasimulia historia ya wana wa Israeli. Ameanzia agano la Mungu kwa Ibrahimu kwamba kupitia uzao wake Ibrahimu, nchi ingejaa watu wasiohesabika; kwamba angewapa nchi ya Kanani iwe urithi wao. Anakumbuka jinsi wana wa Israeli walivyokuwa kule Misri na vile Mungu alivyowaokoa wana wake kutoka katika mikono ya farao na wamisri kwa jumla, na hatimaye wakafika nchi ya Kanani. Mbali na kuwa historia simulizi, wimbo huu pia ni usimulizi ambapo mwingiliano matini unajidhihirisha waziwazi; hadithi inasimuliwa kwa njia ya

ushairi simulizi, huku historia ya wana wa Israeli ikizidi kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kama ilivyo desturi ya fasihi simulizi.

**4.3.3.4 Kuhifadhi utamaduni.**

Kama anavyosema Mrikaria (2007) katika usuli uk. 2, fasihi simulizi imejengwa kwa mfumo uliozoeleka wa kufikisha ujumbe kwa hadhira, na ulilenga zaidi katika kurithishana mila, desturi na tamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Fasihi hii ilirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia nyimbo, hadithi, miviga na hata majigambo. Wamitila (2003) anasema kuwa fasihi simulizi ina nafasi kubwa katika tamaduni simulizi, na hutumiwa kuirithisha jamii elimu, thamani na amali muhimu toka kizazi kimoja hadi kingine. Tanzu za fasihi simulizi huwa nyenzo kuu ya kurithishana elimu ya jadi katika jamii inayohusika.

**Miviga ya kutahiriwa kwa Yesu**

Luka 2:21-24

> "Hata zilipotimia siku nane za kutahiri, aliitwa jina lake Yesu; kama alivyoitwa na malaika kabla hajachukuliwa mimba. Kisha zilipotimia siku za kutakasika kwao, kama ilivyo torati ya Musa, walikwenda naye hata Yerusalemu wamweke kwa Bwana, (kama ilivyoandikwa katika sheria ya Bwana, kila mtoto mwanamume aliye kifungua mimba ya mamaye na aitwe mtakatifu wa Bwana),  wakatoe na sadaka kama ilivyonenwa katika sheria ya Bwana, hua wawili au makinda ya njuwa wawili".

Hapa tunaona jinsi wazazi wa yesu walivyojitahidi kuhifadhi utamaduni wao. Ilikuwa kwamba mtoto mwamamume atahiriwe afikishapo siku nane na pia apewe jina. Pia siku za kutakasika zifikapo, mtoto alifaa apelekwe hekaluni na sadaka itolewe kwa Mungu. Haya yote yalitendeka kwani baada ya kutahiriwa, kwa mujibu wa mila na tamaduni zao, alipewa jina Yesu. Vilevile, alipopelekwa hekaluni kutakaswa, wazazi walitoa sadaka kama ilivyokuwa sheria ya Bwana. Matini za Biblia zimesaidia sana katika kuhifadhi tamaduni husika kama ilivyo mojawapo ya dhima za fasihi simulizi.

Mithali 4:1-27

Ni mawaidha ya baba kwa wanawe.

5-8:

"Jipatie hekima, jipatie ufahamu
Usiusahau
Wala usiyakatae maneno
Ya kinywa changu.
Usimwache, naye atakuhifadhi
Umpende, naye atakulinda
Bora hekima, basi jipatie hekima
Naam, kwa mapato yako yote
Jipatie ufahamu.
Umtukuze,naye atakutukuza
Atakupatia heshima
Ukimkumbatia
Atakupa neema kuwa kilemba
Kichwani
Na kukukirimia taji ya uzuri."

Hayo ni mawaidha ambayo yamepeanwa kwa njia ya ushairi simulizi. Mnenaji amechagua kutumia lugha ya mkato badala ya lugha ya nathari. Katika usimulizi wake ametumia semi kama tashhisi ambayo ni ishara ya mwingiliano tanzu. Inaonyesha jinsi tanzu mbalimbali zinavyoingiliana asemavyo Miruka (2013). Anavipa hekima na ufahamu uhai kwa kuwaambia wanawe, 'usimwache hekima, naye atakuhifadhi. Umpende ufahamu, naye atakulinda.' Anachukulia hekima na ufahamu kama viumbe vyenye uhai anapowaambia wanawe wawakumbatie. Huu ni ufasihi. Vilevile anatumia nahau anaposema 'kuvaa kilemba kichwani'. Hii ni ishara ya mwingiliano wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia.

### 4.4 Mchango wa Biblia katika udumishaji wa fasihi simulizi

Madhumuni ya tatu ya utafiti huu yalikuwa kutathmini mchango wa Biblia katika ukuzaji wa fasihi simulizi. Baada ya kudurusu vitabu teule vya Biblia na kuchanganua maumbo ya fasihi simulizi yaliyobainika katika vitabu hivyo, na aidha, kupambanua mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia, utafiti huu uliweza kubaini kuwa Biblia takatifu inachangia

pakubwa katika ukuzaji wa fasihi simulizi kama asemavyo Kristeva (1969) katika sehemu ya nadharia. Hakuna sehemu yoyote ya fasihi inayoweza kujitegemea bila kuhusiana na matini nyingine. Baadhi ya michango iliyobainika wazi ni pamoja na :

### 4.4.1 Usanii wa watunzi wa Biblia

Usanii ni hali ya ubunifu wa mtunzi. Mbinu ya sanaa kwa kawaida hutokana na ubunifu wa mtunzi. Maumbo ya fasihi simulizi yanafaa yabuniwe ili kuwasilisha maudhui na dhamira ya mtunzi wa kazi ya fasihi katika muktadha wa kimuundo na kimtindo wa utanzu husika (Lemon na Marion, 1965). Kuna tofauti kati ya lugha ya sanaa na lugha ya kawaida. Wamitila (2006) anaeleza sanaa kama ufundi wa hali ya juu wa kuwasilisha mawazo aliyo nayo mtu kwa njia inayoweza kumwathiri anayeiona sanaa hiyo. Maumbo ya fasihi simulizi ni mfano wa usanii unaojitokeza katika vitabu vya Biblia vilivyosomwa.

Plekanov (1957) anaeleza kwamba sanaa haina budi kutumiwa kumsukasuka na kumzindua mwanajamii ili apambane na mazingira machafu. Ili fasihi simulizi iwe na manufaa katika jamii, ni lazima iwe na jukumu la kuieleza jamii, kuichambua, kuikosoa na kuiongoza katika lengo lake la kuupindua unyonge na uchafu uliosakini katika jamii. Fasihi simulizi hutekeleza haya kupitia kwa maumbo yake. Baadhi ya maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia yaliyodhihirisha usanii huu ni pamoja na :

Zaburi 106.

Hii ni hadithi iliyo na usanii wa hali ya juu. Mwandishi ameamua kusimulia hadithi kuhusu jinsi wana wa Israeli walivyomuasi Mungu tangu mwanzo alipowatoa katika nchi ya Misri, hata ikawafanya waishi jangwani kwa miaka arobaini kwa sababu ya uasi wao. Hadithi hii imesimuliwa kishairi, yaani kwa njia ya mkato. Kwa mfano, ili kuonyesha ushairi wa usimulizi huu, kwenye sura ya 7, anasema.

> “Baba zetu katika Misri
> hawakufikiri matendo yako ya ajabu
> hawakukumbuka wingi wa fadhili zako
> Wakaasi penye bahari,
> Bahari ya shamu”

Ingekuwa lugha ya nathari, hangerudia rudia neno "bahari" kama alivyofanya katika hilo shairi. Lakini anarudia neno 'bahari' ili kuonyesha sifa ya takriri kwa kugawa sentensi yenyewe katika mishororo miwili. Hii ni ishara ya ubunifu wa msanii na usanii huu katika Biblia unasaidia katika kukuza fasihi simulizi.

Aidha, usanii hudhihirika katika hadithi hii ambapo mwandishi anatumia usimulizi hakiki/ tunduizi. Mtambaji anatoa maoni yake kuihusu hadithi anayoisimulia.

Sura 23:

"Akasema ya kuwa atawaangamiza.
Kama Musa, mteule wake, asingalisimama,
Mbele zake kama mahali palipobomoka,
Ili aigeuze hasira yake asije akawaharibu".

Haya maoni ya mtambaji wa hii hadithi kuhusu sababu iliyomfanya Mungu akose kuwaangamiza Waisraeli, kwamba Musa alimwomba Mungu aigeuze hasira yake ili asiwaangamize. Matumizi ya tunduizi katika utambaji wa hadithi ni ishara ya usanii na inaonyesha jinsi Biblia inavyochangia katika ukuzaji wa fasihi simulizi mwishoni mwa usimulizi huu mtambaji anamalizia kwa wimbo. Nyimbo hutumiwa kwa kiasi kikubwa katika simulizi au hadithi, penginge kushirikisha hadhira katika hadithi inayosimuliwa ama kama kiliwazo, hasa katika hadithi hii.

Sura 47 – 48

"Ee Bwana Mungu wetu, utuokoe
Utukusanye kwa kututoa katika mataifa
Tulishukuru jina lako takatifu
Tuzifanyie shangwe sifa zako
na ahimidiwe Bwana, Mungu wa Israeli
Tangu milele hata milele
Watu wote na waseme,
Amina, Haleluya."

Usanii vilevile unajidhihirisha katika shairi hili.

Zaburi 118:10-12

"Mataifa yote walinizunguka
Kwa jina la Bwana
Naliwakatilia mbali.
Walinizunguka, naam,
Walinizunguka
Kwa jina la Bwana
Nalizunguka kama nyuki
Walizimika kama moto wa miibani".

Kwa kawaida mashairi huwasilishwa kwa lugha ya mkato, yenye mdundo wa kishairi. Aghalabu ushairi hutumia lugha ya mafumbo ili kuifinyanga lugha pia (Meyer, 2005). Mwandishi wa shairi hili anasimulia kisa ambapo alikuwa hatarini kwa kuzungukwa na mataifa kama nyuki. Anapotaja nyuki anaonyesha hatari iliyomkabidhi. Anaepuka lugha ya nathari na badala yake kuhifadhi mdundo wa kishairi. Ametumia hata kibwagizo katika shairi lake, "kwa jina la Bwana, naliwakatilia mbali." Hii ni ishara ya mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia kwani usanii wa waandishi wa haya matini unajidhihirisha wazi. Vilevile, katika hili shairi, mwandishi ametumia tamathali za usemi. Anaposema "walinizunguka kama nyuki." Kama, ni matumizi ya tashbihi katika fasihi simulizi kwa hivyo tunaona jinsi hayo matumizi yanavyojitokeza katika Biblia.

Mithali 4:1-27 Ni mawaidha ya baba kwa wanawe.

5-8:

"Jipatie hekima, jipatie ufahamu
Usiusahau
Wala usiyakatae maneno
Ya kinywa changu.
Usimwache, naye atakuhifadhi

Umpende, naye atakulinda
Bora hekima, basi jipatie hekima
Naam, kwa mapato yako yote
Jipatie ufahamu.
Umtukuze,naye atakutukuza
Atakupatia heshima
Ukimkumbatia
Atakupa neema kuwa kilemba
Kichwani
Na kukukirimia taji ya uzuri."

Hayo ni mawaidha ambayo yamepeanwa kwa njia ya ushairi simulizi. Mnenaji amechagua kutumia lugha ya mkato badala ya lugha ya nathari. Katika usimulizi wake ametumia semi kama tashhisi ambayo ni ishara ya mwingiliano tanzu. Inaonyesha jinsi tanzu mbalimbali zinavyoingiliana asemavyo Miruka (2013). Anavipa hekima na ufahamu uhai kwa kuwaambia wanawe, 'usimwache hekima, naye atakuhifadhi. Umpende ufahamu, naye atakulinda.' Anachukulia hekima na ufahamu kama viumbe vyenye uhai anapowaambia wanawe wawakumbatie. Huu ni ufasihi. Vilevile anatumia nahau anaposema 'kuvaa kilemba kichwani'. Hii ni ishara ya mwingiliano wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia.

### 4.4.2. Ufasihi wa Biblia

Allen (2000) kama alivyorejelewa katika misingi ya nadharia anaeleza kwamba kazi za fasihi zimejengwa kutokana na mifumo, kanuni na taratibu zilizokubaliwa na jamii na tamaduni zilizojengwa na kazi za zamani za fasihi. Tendo la kusoma humtosa msomaji katika mfumo wa uhusiano wa matini unaohusiana na matini zingine.

Ngure (2003) kama tulivyosema hapo awali anaeleza fasihi simulizi kama sanaa itumiayo maudhui yake kwa lugha ya maneno na kwamba fasihi ni namna ya utoaji maudhui kisanaa na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo. M'Ngaruti (2008) anaeleza kuwa fasihi simulizi huhusisha tamathali za usemi, ambazo hujumuisha tanzu kama vile methali, vitendawili, mafumbo, misimu, lakabu ambayo ni majina yanayobandikwa watu kutokana na sifa zao, maumbile, hulka au

mambo yanayowahusu, na kauli tauria. Katika uchunguzi huu, imebainika kwamba Biblia, kama ilivyo fasihi simulizi, inahusisha tanzu bainifu mbalimbali.. Tanzu hizo zimejitokeza kama methali, vitendawili, mafumbo na nahau.

Katika kitabu cha Mathayo 15:10 – 14, Yesu ametumia fumbo kuwafunza wanafunzi wake. Msitari wa kumi na nne unasema; *"Waacheni hao ni viongozi vipofu wa vipofu. Na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili*."

Hapa yesu alikuwa akiongea kuhusu mafarisayo waliokuwa viongozi wa hekalu ilhali wao wenyewe hawakuweza kuelewa neno la Mungu vilivyo. Yesu akawaita vipofu kwa kutofahamu au kutozingatia yale waliyokuwa wakifunza. Vilevile, wale waliokuwa wakifunzwa hawakufahamu chochote, ikawa kwamba kipofu anamwongoza kipofu mwenzake. Aidha katika Mathayo 26:31, Yesu alitumia mfano mwingine wa fumbo.

"Ndipo Yesu akawaambia, nyinyi nyote mtachukizwa kwa ajili yangu usiku huu kwa kuwa imeandikwa, nitampiga mchungaji wa kondoo, na kondoo wa kundi watatwanyika."

Yesu alikuwa akiongea na wanafunzi wake kuhusu kusulubiwa kwake. Mchungaji ni yeye, kondoo ni wanafunzi wake. Baada ya kuteswa na kusulubiwa kwake, wanafunzi wake wangetawanyika kwani hawangekuwa na mchungaji/ kiongozi ambaye angewaongoza kwa wakati huo. Methali pia zimetumika kwa wingi katika Biblia. Katika kitabu cha Mithali, wingi wa mafunzo umefanywa kwa kutumia Methali. Mifano ni kama ifuatayo"

Mithali 9:7

"Amkaripiaye mtu mbaya hujipatia aibu."

Mithali 10:1

"Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye, bali mwana mpumbavu, ni mzigo wa mamaye."

Mithali 10:17

" Akubaliye kurudiwa huwa katika njia ya uzima, bali yeye aachaye maonyo hukosa."

Mithali 10:19

“ Katika wingi wa maneno hapakosi kuwa na maovu, bali yeye azuiaye midomo yake hufanya akili.”

Mithali 10:31

“ Kinywa cha mwenye haki hutoa hekima, bali ulimi wa ukaidi utakatiliwa mbali.”

Mithali 11: 2

“Kijapo kiburi ndipo ijapo aibu, bali hekima hukaa na wanyenyekevu.”

Mithali 12:24

“Mkono wa mwenye bidii utatawala bali mvivu atalipishwa kodi”

Mithali 14:25

“Shahidi wa kweli huponya nafsi za watu, bali atoaye uongo hudanganya.”

Mithali 15: 1

“Jawabu la upole hugeuza hasira, bali neno liumizalo huchochea ghadhabu.”

Mithali 17:13

“Arudishaye mabaya badala ya mema, mabaya hayataondoka nyumbani mwake.”

Hizi ni baadhi tu ya methali zilizopatikana katika kitabu cha Mithali.

Aidha, vitendawili vimetumika kwa wingi. Baadhi yavyo ni pamoja na:-

Mithali 13:7

“Kuna mtu mwenye kujitajirisha lakini hana kitu, kuna ajifanyaye kuwa maskini lakini ana mali nyingi.”

Jibu: Mtu anayejiinua na mwenye kunyenyekea.

Hiki kitendawili kinahusu watu wanaopenda kujiinua kwa kuongea kana kwamba ni tajiri ilhali ukweli ni kwamba hana chochote cha maana cha kuonyesha kwamba ni tajiri. Wenye mali mara nyingi hawajionyeshi. Ukimtazama utafikiri ni maskini kwa sababu ya unyenyekevu wake, kumbe anayo mali nyingi. Kitendawili hiki kinatumiwa kuwaonya watu dhidi ya kiburi.

Luka 8: 18

> "Jiangalieni basi jinsi msikiavyo; kwa kuwa mwenye kitu atapewa, na Yule asiye na kitu atanyng'anywa hata kile ambacho anadhaniwa kuwa nacho."

Jibu: Kukubali hali yako.

Hiki kitendawaili kinawahimiza watu watumie chochote walicho nacho bila kulalamika wala kunung'unika. Ukitumia ulicho nacho kwa hekima, bila shaka utaongezewa. Ikiwa wewe kazi yako ni kulalamika na kudharau kidogo chako, basi hata hicho kidogo kitachukuliwa na ubaki bila. Kitendawili hiki kinawahimiza watu wafurahie walivyo au kile walicho nacho kwani padogo pako si pakubwa pa mwenzio.

Kuna baadhi ya nahau zilizotumika katika vitabu vilivyochunguzwa zikiwemo

Zaburi 45:1

> "Ulimi wangu ni kalamu ya mwandishi stadi"

Zaburi 44:25

> "Tumbo letu limegandamana na nchi."

Mithali 1:32

> "Kurudi nyuma kwao wajinga kutawaua."

Mithali 7: 27

> " Nyumba yake ni njia ya kwenda kuzimu."

Mithali 1:9

> " Amevaa kilemba cha neema kichwani."

Hizi ni baadhi ya nahau zilizotumika katika vitabu tulivyovisoma kudhihirisha usanaa wa Biblia kama kitabu cha fasihi. Baadhi ya sababu za matumizi ya mitindo hii ni kudhihirisha ufasihi na dhima yake katika jamii kama ilivyojadiliwa hapo awali. Kama asemavyo Nelson (1995), ufasihi wa Biblia unatokana na usanii na hujaribu kuelewa habari aliyotaka kupasha mwandishi na jinsi ambavyo ingeeleweka katika mkao wa asili ya kihistoria na kitamaduni. Hii inahusisha maarifa kuhusu muundo wa mwandishi, matumizi ya lugha, historian a utamaduni.

**4.4.3 Uhalisia na uhai wa Biblia**

Uhalisia ni neno ambalo lina maana mahususi kwake, ya kuzingatia kuwa mwandishi ni mbunifu wa jambo ambalo linaelekea kuwa kweli kwa sababu linayumkinika tu, yaani lipo katika jamii ingawa sio lazima liwe la kweli.

Tukimrejelea Plekanov (1957) fasihi ni chombo mojawapo katika harakati dhidi ya mazingira. Sanaa hutumiwa kumsukasuka na kumzindua mwanajamii ili apambane na mazingira machafu. Ili fasihi simulizi iwe na manufaa katika jamii, ni lazima iwe na jukumu la kuieleza jamii, kuichambua, kuikosoa na kuiongoza katika lengo lake la kuupindua unyonge na uchafu uliosakini katika jamii. Kwa mujibu wa Jamii ya Biblia za Tanzania na Kenya (1997) ujumbe unaojitokeza katika Biblia kama kitabu cha fasihi ni ule wa kufunza, kuonya na kutahadharisha. Kwa hivyo, jinsi wasemavyo Njogu na chimera (2008), fasihi hutokana na hali halisi ya jamii katika viwango vya siasa, uchumi na utamaduni. Ili uhalisia huu udhihirike katika kazi za fasihi, lazima mtunzi atumie maumbo yanayowasilisha maneno, vitendo na taswira halisi ya wahusika. Hali hii huwezekana katika matumizi ya maumbo ya fasihi simulizi kama vile maigizo, mazungumzo, maghani, mighani na mengineyo. Haya yote yaliweza kubainika katika utafiti huu.

Mfano, katika kitabu cha Mathayo 26: 47 – 52, kuna mfano wa maigizo.

> "Basi alipokuwa katika kusema, tazama, Yuda, mmoja wa wale thenashara akaja, na pamoja naye kundi kubwa wenye panga na marungu, wametoka kwa wakuu wa makuhani ni wazee wa watu. Na Yule mwenye kumsaliti alikuwa amewapa ishara, akisema, nitakayembusu, hivyo ndiye, mkamateni. Mara akamwendea Yesu, akasema, salama, Rabi, akambusu. Yesu akamwambia, Rafiki, fanya ulilolijia. Wakaenda, wakanyoosha mikono yao wakamkamata Yesu. Na tazama, mmoja wao waliokuwa na Yesu akanyosha mkono wake, akaufuta upanga wake, akampiga mtumwa wa kuhani mkuu, akamkata sikio. Ndipo Yesu akamwambia, rudisha upanga wako mahali pale, maana wote waushikao upanga wataangamia kwa upanga."

Kama ilivyo kawaida ya maigizo, huongeza uhalisia katika kazi ya wahusika kwa kutumia maneno halisi yaliyotajwa na wahusika. Hapa tunaona maneno ya Yuda kwa wakuhani na wazee wa watu kwamba, 'nitakayembusu, huyo ndiye'. Aidha, anamwambia Yesu, salamu, Rabi. Vilevile, Yesu pia anaongea kwa kumwambia Yuda afanye lililompeleka kwake. Pia

anamwambia aliyemkata mwenzake sikio arudishe upanga wake. Haya yote yanadhihirisha uhalisia katika kazi ya wahusika. Pia kuna matumizi ya maelekezo jukwaani yanayoonyesha mandhari, maleba na vitendo vya wahusika. Kwa mfano tunamwona Yuda akija na kundi kubwa. Kundi lenyewe limebeba mapanga na marungu. Mmoja wa wafuasi wa Yesu anachukua upanga wake na kumkata mwenziwe sikio. Yesu anamwamuru aurudishe upanga wake. Huu bila shaka ni uhalisia wa yale yanayotendeka katika jamii ya kawaida kwani ni kawaida adui akimshambulia mwenzako ama rafiki yako mkiwa pamoja, bila shaka utajaribu kumtetea ama kwa kulipiza kisasi au kwa kumkinga.

Katika kitabu cha 1Wafalme 12:28 – 30, kuna mfano wa miviga ambapo Yeroboamu mfalme wa Yuda anafanya kwa ajili ya woga wa ufalme kuirudia nyumba ya Daudi

> "Kwa hivyo mfalme akafanya shauri, akafanyiza ngo'mbe wawili wa dhahabu, akawaambia watu, ni vigumu kwenu kupanda kwenda Yerusalemu. Tazama, hii ndiyo Miungu yenu, enyi, Israeli, iliyowapandisha kutoka nchi ya Misri. Akamweka mmoja katika Betheli, na wa pili akamweka katika Dani. Jambo hili likawa dhambi maana watu walikwenda kuabudu mbele ya kila mmoja, hata huko Dani ….. akatoa dhabihu juu ya ile madhabahu aliyoifanya katika Betheli na Dani."

Katika maisha yetu ya kawaida, viongozi mara nyingi huwa na hofu ya uongozi wao kuchukuliwa na kiongozi mwingine. Hii huwapelekea kufanya mambo yasiyostahili ili kuhifadhi uongozi wao. Mathayo 2 katika Biblia inatuonyesha jinsi Herode mfalme wa Uyahudi alivyobabaika aliposikia kwamba Yesu alikuwa amezaliwa na angekuwa mfalme wa Wayahudi. Aliamua kuwaua watoto wa kiume wote waliokuweko huko Bethlehemu na viungani mwake kuanzia miaka miwili na kupungua kwa kuwa alihofia uongozi wake ungachukuliwa. Yeroboamu hata ingawa alimjua Mungu wa Israeli aliyewatoa katika nchi ya Misri, aliamua kutengeneza miungu mingine kwa hofu kuwa wana wa Yuda wangeenda kuabudu kule Yerusalemu, na kutoa dhabihu zao huko, huenda mioyo yao ingemrudia Rehoboam aliyekuwa mfalme wa Israeli na basi uongozi ukairudi nyumba ya Daudi. Huu ni mfano wa uhalisia wa Biblia kama kitabu cha fasihi anavyosema Nelson (1995)

Mighani vilevile imejitokeza kwa kuwasilisha wahusika wa kihistoria wanaoaminika waliishi katika jamii fulani. Wamitila (2003) anaeleza kwamba mighani huchanganya historia na chuku ya kifasihi kiasi kwamba ukweli wa kihistoria unaelekea kufunikwa na sifa za kifantasia, yaani mambo ya kiuwazaji ambayo labda hayawezekani kufanyika; kuweko kwa matendo ya ukiamaumbile, miujiza, maajabu na uchawi. Katika kitabu cha 2Wafalme 2:11-14; kuna mfano wa mighani ya Eliya kuchukuliwa mbinguni kwa upepo wa kisulisuli.

> "Ikawa walipokuwa wakiendelea mbele na kuongea, tazama! Kukatokea gari la moto, na farasi wa moto, likawatenga wale wawili, naye Eliya akapanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli. Naye Elisha akaona, akalia, baba yangu, baba yangu, gari la Israeli na wapanda farasi wake! Asimwone tena kabisa; akashika mavazi yake mwenyewe, akayararua vipande viwili. Kisha aliokota lile vazi la Eliya lililomwangukia, akarudi akasimama katika ukingo wa Yordani; akalitwaa."

Ni kama tendo la ukiamaumbile kwani si kawaida binadamu kuchukuliwa mbinguni bila kupitia kwa kifo. Elisha anashuhudia kuchukuliwa kwa Eliya mbinguni na kisha analia huku akimwomba Mungu wake, kisha anararua mavazi yake na kutwaa lile vazi la Eliya liliomwangukia (2Wafalme 2:11- 12. Hapa wahusika Eliya na Elisha wanaaminika waliishi katika jamii ya Uyahudi na wote walikuwa manabii. Hii inawasilisha uhalisia wa kazi ya fasihi katika Biblia.

Katika kitabu cha Mwanzo 25: 30 – 34, kuna mazungumzo kati ya Esau na Yakobo kuhusu haki ya mzaliwa wa kwanza.

> "Esau akamwambia Yakobo, tafadhali unipe hicho chakula chekundu nile, kwa kuwa ninazimia mimi. Yakobo akamwambia, kwanza niuzie haki yako ya mzaliwa kwanza. Esau akasema, tazama mimi ni karibu kufa, itanifaa nini haki hii ya uzazi? Yakobo akamwambia, uniapie kwanza; naye akamwapia, akamuuzia Yakobo haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Yakobo akampa Esau mkate na chakula cha dengu, naye akala, akanywa kisha akaondoka akaenda zake . hivyo Esau akaidharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza."

Haya ni mazungumzo kati ya Esau na Yakobo kuhusu haki ya mzaliwa wa kwanza. Mazungumzo yenyewe yanawasilishwa kwa usemi halisi ambapo msemaji anasema moja kwa moja kuonyesha uhalisia wa kauli zinazotolewa na wahusika, ishara ya uhalisia wa kazi ya fasihi katika kitabu hiki. Escarpit (1973) kama alivyorejelewa hapo awali anasema kwamba fasihi lazima ichukuliwe kama ilivyo na uhusiano usiotatanika na maisha ya jamii. Fasihi ni taasisi ya jamii inayotumia lugha kama mtambo wake. Isitoshe fasihi huwasilisha maisha. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba Biblia inasaidia pakubwa katika udumishaji wa fasihi simulizi.

### 4.4.4 Ukuzaji na uendelezaji wa stadi za lugha

Jinsi tulivyoona hapo nyuma, fasihi simulizi hutegemea usemi na matamko. Hatuwezi kushiriki katika mambo haya pasi na kuongea au kutamka au kuimba. Kwa njia hii, fasihi simulizi ina mchango mkubwa wa kuboresha uwezo wetu wa kuzimiliki na kuzimudu stadi za lugha. Tanzu kama vitanza ndimi vilisaidia kuhakikisha kuwa utamkaji ni mzuri; vitendwaili na mithali huukuza uwezo wa kuwaza haraka na vyema, hadithi nazo huukuza uwezo wa kukumbuka.

Nelson (1995) kama alivyorejelewa katika mapitio ya maandishi anaeleza kwamba ufasihi wa Biblia unatokana na usanii na hujaribu kuelewa habari aliyotaka kupasha mwandishi na jinsi ambavyo ingeeleweka katika mkao wa asili wa kihistoria na utamaduni. Hii inahusisha maarifa kuhusu muundo wa mwandishi, matumizi ya lugha, historia, utamaduni na mambo kuhusu wakati na mahali ilipoandikwa. Katika vitabu vilivyotafitiwa, stadi za lugha zimedhihirika kwa wingi, hasa katika vitabu vya Zaburi, Mithali na Mathayo; na lugha kutumika kwa hizi stadi za lugha ambazo ni sawa na tanzu bainifu zinaonyesha jinsi Biblia inavyochangia katika ukuzaji wa lugha, hivyo kuiendeleza fasihi simulizi. Mbali na vitendawili, methali na nahau, kuna tashbihi, tashhisi na takriri ambavyo vimejidhihirisha katika kazi hii.

#### 4.4.4.1 Tashhisi

Tashhisi kwa mujibu wa Ndungo na Wafula (1993) ni mbinu ambapo vitu ambavyo havina uhai wala tabia za binadamu hupewa sifa za bindamu. Kwa mfano kitu ambacho kwa kawaida hakiwezi kutembea, kusema, kuzaa wala kufa kinaweza kupewa uwezo huo katika mbinu hii. Wamitila (2003) anaeleza tashhisi kama mbinu ambapo kitu kisichokuwa na uhai kinapewa sifa

za uhai. Mifano kadhaa ya tashhisi ilijitokeza katika vitabu vilivyofanywa utafiti, hasa kitabu cha Zaburi na mithali.

Zaburi 98:7-8.

> “Bahari ivume, mito ipige makofi, milima iimbe pamoja kwa furaha”.

Tunajua ya kwamba bahari, mito na milima ni vitu visivyo na uhai, lakini vimepewa sifa za binadamu za kuvuma, kupiga makofi na kuimba kwa furaha. Binadamu wanahimizwa hapa kumwimbia na kushangilia Mungu kwa yale ambayo amewatendea. Wote walio na uhai wanahimizwa kumfurahia Mungu kwa makofi na furaha.

Zaburi 90 : 2.

> “Kabla haijazaliwa milima”.

Milima sio viumbe vyenye uhai ambavyo huzaliwa na kufa. Tashhisi hii imehusisha kuwepo kwa Mungu tangu jadi na jadi, yaani Mungu amekuwa Mungu tangu milele hata milele.

Zaburi 104:13.

> “Nchi imeshiba mazao ya kazi zako”.

Aliye na uhai ndiye anayeweza kuhisi njaa, ale na apate kushiba. Visivyo na uhai daima havili wala haviwezi kushiba. Nchi imepewa sifa ya uhai kuashiria wanadamu ambao wamepata mahitaji yao yote kutoka kwa Mungu hata wakatangaza kwamba wameshiba, kumaanisha wametosheka na yale wanayopewa na Mungu.

Mithali 6: 24.

> “Maagizo yakulinde na mwanamke mwovu, asikupate, na kukuponya na ubembelezi wa mgeni”.

Maagizo yamepewa sifa ya uhai. Ikiwa utayashika maagizo basi utaepukana na mwanamke mwovu kwani hutaenda karibu naye wala hutasikiza ubembelezi wake.

Mithali 8.1

"Hekima halii? Ufahamu hatoi sauti yake?"

Hekima na ufahamu vimepewa sifa ya binadamu ya kulia na kutoa sauti. Binadamu anahimizwa tu kuwa na hekima na ufahamu ili aweze kuyaepuka maovu yaliyojaa ulimwenguni. Kinacholia mara nyingi husaidiwa; lazima tujue kwa nini kinalia.

#### 4.4.4.2 Takriri

Ndungo na Wafula (1993) wanaeleza takriri kama mbinu ya kusisitiza ujumbe. Aidha husisitiza hisi na wakati. Baadhi ya takriri zilizojitokeza katika utafiti huu ni pamoja na:

Zaburi 124: 1 – 2

> "Kama si Bwana aliyekuwa pamoja nasi, Israeli na aseme sasa; kama si Bwana aliyekuwa nasi Israeli na aseme sasa. Kama si Bwana aliyekuwa pamoja nasi, wanadamu walipotushambulia."

Hapa uwepo wa Bwana miongoni mwao ndio unaosisitizwa.

Zaburi 124: 3 – 5

> "Papo hapo wangalitumeza hai
> Papo hapo maji yangalitugharikisha
> Papo hapo yangalipita juu ya nafsi zetu"

Hapa, wakati unasisitizwa, 'papo hapo', kumaanisha kwamba adui zao hawangewapa muda wowote. Wangewaangamiza mara moja.

Zaburi 129 : 1 – 2

> "Mara nyingi wamenitesa tangu ujana wangu; Israeli na aseme sasa. Mara nyingi wamenitesa tangu ujana wangu, Israeli na aseme sasa, mara nyingi wamenitesa tangu ujana wangu, Lakini hawakuniweza".

Hapa msisitizo ni idadi ya mateso yake katika ujana wake. Ameteswa mara nyingi.

Zaburi 131: 1 – 3

> "Wala macho yangu hayainuki

Wala sijihusishi na mambo makuu

Wala na mambo yashindayo nguvu zangu”

Neno ‘wala’ limerudiwa kusisitiza jinsi mwandishi anavyojitenga na maovu na kutojihusisha nayo.

Zaburi 89 : 13

“Mkono wako ni mkono wenye uwezo: mkono wako una nguvu, mkono wako wa kuume umetukuka.”

Hapa kinachosisitizwa ni uwezo wa mkono wa Mungu; una nguvu.

“Ee bwana, mito imepaza

Mito imepaza sauti zake

Mito imepaza uvumi.”

Kifungu ‘Mito imepaza’ kimerudiwa rudiwa ili kusisitiza umuhimu wa yale yanayosemwa. Mbali na tashbihi, kuna tashhisi pia katika hicho kifungu. ‘mito imepaza sauti zake’. Mito imepewa sifa ya kitu kilicho na uhai ingawaje tunajua kwamba haina uhai. Kwa hivyo inatusaidia kudhihirisha jinsi Biblia inavyochangia katika ukuzaji wa fasihi simulizi hasa kwa mchango wake mkubwa wa koboresha uwezo wetu wa kuzimiliki na kuzimudu stadi za lugha.

Zaburi 131:1

“Bwana, moyo wangu hauna kiburi

wala macho yangu hajainuki

Wala sijishughulishi na mambo makuu

wala na mambo yashindayo nguvu zangu.”

Hapa aidha, kuna matumizi ya takriri ambapo neno ‘wala’ limerudiwa rudiwa kusisitiza jinsi msemaji alivyojitenga na mambo makuu. Hii inasaidia kuhakikisha kwamba utamkaji ni mzuri na kwamba mzungumzaji ameimudu lugha vilivyo.

#### 4.4.4.3 Tashbihi.

Wamitila (2003) anaeleza tashbihi kuwa ulinganishi wa moja kwa moja unaodhamiriwa kusisitiza sifa fulani na pia kutujengea picha ya aina fulani akilini. Ulinganishi huu unaonyeshwa kwa matumizi ya viungo: kama, mfano wa, sawa na, mithili ya na ja. Mifano ya tashbihi katika vitabu tulivyovisoma ni pamoja na;

Zaburi 125:1.

"Wamtumainio Bwana ni kama mlima sayuni."

Wale watu walio na matumaini yao kwa mungu wamelinganishwa na mlima zayuni. Mlima kwa kawaida hautingisiki, kumaanisha kwamba hao watu wako imara na wala hawataogopa mambo yoyote yale wanayoyapitia.

Mithali 7: 2

"Uzishike sheria zangu kama mboni ya jicho lako."

Hapa umuhimu wa sheria ya Mungu Umelinganishwa na mboni la jicho, sehemu ya jicho amabayo ni ya muhimu sana na kila mirika inafichwa dhidi ya adui. Hii tashbihi inaonyesha jinsi lugha ilivyotumika kwa ustadi katika Biblia katika ile hali ya kuikuza na kuiendeleza fasihi simulizi.

Kutokana na utafiti huu, ni bayana kuwa fasihi hutokana na fasihi, ila hoja zinazotungwa zinaweza kubadilika na kuundwa tena kutegemea mazingira.

### 4.4.5 Uhifadhi wa fasihi simulizi.

Mrikaria (2007) kama tulivyoeleza katika usuli uk. 2, anasema kwamba fasihi simulizi hapo awali ilirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine huku ikihifadhiwa kichwani, lakini baada ya mwingiliano wa wageni toka pande mbalimbali za dunia, ilianza kubadilika kutokana na mila, desturi na tamaduni zilizoingizwa kutoka kwa wageni hawa. Kimball (2008) anasema kwamba maandishi ya Biblia yalitumika kama masimulizi ya mdomo kwa muda mrefu sana, yakahaririwa na kuhaririwa tena, ndipo baadaye yakawekwa katika maandishi. Hayo maandishi kwa sasa

yanatumiwa kama hifadhi ya fasihi simulizi. Katika utafiti huu, Biblia imedhihirika kama hifadhi ya fasihi simulizi kwani tukitazama kitabu cha Zaburi:

Zaburi 78:1-

> “Enyi watu wangu, sikilizeni sheria zangu,
> Tegeni masikio kwa maneno ya kinywa changu.
> Na nifunue kinywa changu kwa mithali,
> Niyatamke mafumbo ya kale.
> Mambo tuliyoyasikia na kuyafahamu,
> Ambayo baba zetu walituambia.
> Hayo hatutawaficha wana wao,
> Huku tukiwaambia kizazi kingine,
> Sifa za Bwana na nguvu zake,
> Na mambo yake ya ajabu aliyoyafanya.
> Maana alikaza ushuhuda katika Yakobo,
> Na sheria aliiweka katika Israeli.
> Aliyowaamuru baba zetu, wawajulishe wana wao,
> Ili kizazi kingine wawe na habari,
> Ndio hao wana watakapozaliwa,
> Wasimame na kuwaambia wana wao”.

Fasihi simulizi mwanzoni ilihifadhiwa kichwani na kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hapa tunaona jinsi Daudi alivyokuwa akiwakumbusha wana wa Israeli kupitia kwa mithali na mafumbo, ambavyo ni vipera vya maumbo ya fasihi simulizi, mambo waliyoambiwa na baba zao. Ilibidi wana wa Israeli waambiwe ili wao pia wawaambie wana wao ili kila kizazi kiwe na habari hiyo. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba Biblia ni hifadhi ya fasihi simulizi kwani kabla ya haya yote kuwekwa katika maandishi ilibidi yahifadhiwe kichwani ndiposa kurithishwa kizazi hadi kizazi.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.

## 5.1 Muhtasari wa tasnifu.

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu la kuhakiki kwa kina mwingiliano matini wa maumbo ya fasihi simulizi na matini teule za Biblia. Katika kuafikia lengo hili , kulikuwa na madhumuni matatu ya utafiti: Kuchanganua vipengee vya fasihi simulizi ambavyo vinapatikana katika Biblia; Kupambanua mwingiliano taaluma wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia; Kutathmini mchango wa Biblia katika udumishaji wa fasihi simulizi. Ili kuweza kuafikia madhumuni haya, matini teule za Biblia zilisomwa kwa kina na kuchanganuliwa. Data ilikusanywa maktabani kwa kudurusu maandishi na kuchanganuliwa kisifa. Matokeo ya maandishi yaliwasilishwa kwa maelezo katika aya mbalimbali. Tanzu nne kuu za fasihi simulizi ambazo ni hadithi/simulizi, maigizo, semi/ tanzu bainifu na ushairi simulizi zilijadiliwa kama maumbo ya fasihi simulizi.

Nadharia ya mwingiliano matini iliongoza utafiti huu. Mihimili mitatu ya nadharia hii ambayo ilitumika katika utafiti huu ilikuwa: Kila matini ina uhusiano na matini nyingine, yaani matini zote zinafaidika zaidi kutoka kwa matini nyingine. Matini za Biblia zimejitokeza zikichukua sifa na maumbo asilia ya kitamaduni ya tanzu zingine za fasihi simulizi; Matini huundwa na watunzi wengine kwa njia nyingi. Hii ilionekana katika mwingiliano uliohusu mazungumzo baina ya matini za fasihi asimulizi na matini teule za Biblia; Fasihi hutokana na fasihi. Waandishi wa Biblia kwa mfano, walitumia matini za awali za fasihi simulizi katika uandishi wao na hoja zao zikaweza kubadilika na kuundwa tena kutegemea mazingira.

Utafiti ulihitimisha kwamba kuna maumbo ya fasihi simulizi katika vitabu teule vya Biblia vilivyosomwa. Maumbo haya yalibainika pamoja na vipera vyao. Vipera vya hadithi vilivyobainika katika utafiti huu ni pamoja na visasili, hekaya, mighani na mbazi. Maigizo yalijitokeza kama mazungumzo, mawaidha, michezo ya kuigiza na miviga. Nazo semi zilikuwa na vipera vyake kama vitendawili, nahau, tashhisi, tashbihi na takriri. Vipera vya ushairi simulizi vilivyobainika vilikuwa nyimbo na maghani. Vilevile ilibainika kwamba maumbo mengine yanpatikana katika vitabu fulani zaidi ya vingine. Si yote yanapatikana katika vitabu vyote. Maumbo kama vile hadithi/ simulizi yanapatikana sana katika vitabu vya Mwanzo, 1Wafalme, 2Wafalme, Mathayo na Luka. Maigizo yalidhihirika sana katika vitabu vya Mwanzo, 1Wafalme, Zaburi, Mathayo na Luka.Tanzu bainifu/ semi zilibainika sana katika Zaburi, Mithali, Mathayo na Luka; Ushairi simulizi nao ukadhihirika katika Zaburi, Mithali na Luka.
Nadharia ya mwingiliano matini iliongoza utafiti huu. Mihimili mitatu ya nadharia hii ambayo ilitumika katika utafiti huu ilikuwa: Kila matini ina uhusiano na matini nyingine; Matini huundwa na watunzi wengine kwa njia nyingi; fasihi hutokana na fasihi.

### 5.1.1 Maumbo ya fasihi simulizi katika Biblia

Kwa mujibu wa utafiti huu, ilibainika kwamba maumbo makuu manne ya fasihi simulizi yanapatikana katika Biblia pamoja na vipera vyao. Umbo la hadithi kwa mfano lilidhihirika kwa vipera kama vile visasili, hekaya, mbazi na mighani/visakale. Umbo la maigizo lilibainika kwa vipera vyake kama vile mazungumzo, mawaidha, miviga na michezo ya kuigiza. Umbo la semi/ tanzu bainifu lilionekana kupitia kwa tanzu kamakama methali, vitendawili, nahau,tashhisi,

tashbihi na takriri. Mwisho, kulikuwa na umbo la ushairi simulizi ambalo vipera vyake vilikuwa nyimbo na maghani.

Hadithi zilibainika katika vitabu vya Mwanzo, 1Wafalme, 2Wafalme, Mathayo na Luka.Vipera vya visasili na hekaya vilibainika zaidi katika vitabu vya 1Wafalme, 2Wafalme na Mwanzo. Mbazi zilipatikana zaidi katika vitabu vya Mathayo na Luka, nayo mighani ikadhihirika katika vitabu vyote isipokuwa kitabu cha Mithali. Umbo la maigizo nalo lilidhihirika katika karibu vitabu vyote. Utanzu huu ulibainika kwa sifa kama; matumizi ya maelekezo jukwaani, kuwepo kwa hadhira na matumizi ya maleba. Vipera vyake vilivyobainika ni pamoja na mazungumzo katika kitabu cha Mwanzo, 1Wafalme, Mathayo, na Luka. Mawaidha kutoka vitabu vyote ila 2Wafalme; Miviga katika Mwanzo, 1Wafalme, 2Wafalme, Mathayo na Luka; kisha michezo ya kuigiza katika 1Wafalme, 2Wafalme, Zaburi, Mathayo na Luka. Umbo la tanzu bainifu lilidhihirika kwa wingi. Methali zilibainika katika Mithali na Zaburi. Vitendawili katika vitabu vyote ila kitabu cha Mwanzo na 1Wafalme. Nahau, tashbihi, tashhisi na takriri vilidhihirika sana katika Zaburi na Mithali. Ushairi simulizi nao ulidhihirika kupitia kwa vipera vyake viwili; nyimbo na maghani, ambavyo vilipatikana zaidi katika Zaburi, Mithali na Luka.

Kutokana na mifano iliyotolewa, ni dhahiri kwamba maumbo ya fasihi simulizi yamejidhihrisiha wazi katika vitabu teule vya Biblia vilivyochanganuliwa. Haya yanaingiliana vilivyo na nadharia ya mwingiliano matini ambapo nguzo yake ya kwanza inaeleza kwamba kila matini ina uhusiano na matini nyingine. Matini za fasihi simulizi na matini za Biblia zimeonekana zikiwa na uhusiano hasa kupitia kwa maumbo ya fasihi simulizi.

### 5.1.2. Mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia

Mhimili wa pili wa nadharia ya mwingiliano matini ulikuwa kwamba matini huundwa na watunzi wengine kwa njia nyingi. Utafiti uliofanywa ulionyesha kwamba matini za fasihi simulizi huingiliana na matini teule za Biblia, hasa matini za vitabu vilivyofanyiwa utafiti. Mwingiliano wenyewe ulijitokeza kwa kuzingatia mambo mbalimbali. Kwanza, kuna mwingiliano kimtindo ambapo ilibainika kwamba ujenzi wa vitabu katika Biblia ulitokana na mitindo tofauti ya maelezo yanayochukua maumbo ya kimasimulizi. Fasihi ni taasisi ya jamii inayotumia lugha kama mtambo wake, na huwasilisha maisha ya binadamu. Sifa mojawapo ya

mtindo katika fasihi simulizi ni urudiaji ambao unaweza kuwa na vipengele vya muundo kama virai, maneno, sentensi au vifungu fulani. Hii sifa imedhihirika katika uchunguzi uliofanywa. Sifa nyingine za kimtindo zilizobainika katika utafiti huu ni kwamba Biblia inao wahusika ambao ni binadamu pamoja na wanyama; matumizi ya tamathali za usemi au mbinu bainifu, mtindo wa ishara na taswira.

Pili, mwingiliano matini wa fasihi simulizi na matini teule za Biblia ulibainika kupitia kwa sifa za fasihi simulizi. Baadhi ya sifa za fasihi simulizi zilizobainika katika utafiti huu ni pamoja na matumizi ya mazungumzo yakihusisha utendaji kwa njia nyingine za mawasiliano ili kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Aidha fasihi simulizi huwasilishwa kwa hadhira iliyo hai. Baadhi ya kazi za Biblia kama ilivyobainika ziliwasilishwa kwa njia ya mdomo na kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Aidha, mwingiliano wa matini za fasihi simulizi na matini teule za Biblia ulibainika kupitia kwa dhima ya fasihi simulizi katika jamii. Baadhi ya majukumu ya matini za Biblia kama ilivyobainika ni pamoja na kumfanya binadamu kuweza kujieleza, kujielewa na kujifahamu. Katika kutekeleza haya, Biblia inampa binadamu maadili na kumburudisha kwa kumpa elimu, ujitambuaji na ujijuaji, ujamiishaji na ukuzaji wa stadi za lugha. Biblia vilevile imesaidia kuhifadhi historia na tamaduni hasa tamaduni za Kiyahudi.

Mwisho, fasihi simulizi na matini za Biblia zimeingiliana kwa kuzingatia usanaa. Matini za Biblia zimeandikwa kwa ubunifu kama ilivyo kawaida ya maumbo ya fasihi simulizi ili kuwasilisha maudhui na dhamira ya mtunzi. Maumbo ya fasihi simulizi katika vitabu vilivyofanyiwa utafiti yamejitokeza kama mbinu za sanaa kwa kudhihirisha usanii wa mtunzi.
Utafiti huu kwa hivyo umeonyesha kwamba matini za fasihi simulizi huingiliana na matini za Biblia zilizoteuliwa. Kuna mwingiliano kimtindo, mwingiliano kwa kuzingatia sifa za fasihi simulizi, na mwingiliano kwa kuzingatia usanaa. Mhimili wa pili wa nadharia ya mwingiliano matini ambao unasema kwamba matini huundwa na watunzi wengine kwa njia nyingi ulitumika kupambanua mwingiliano wa matini

### 5.1.3 Mchango wa Biblia katika udumishaji wa fasihi simulizi.

Biblia inachangia pakubwa katika ukuzaji wa fasihi simulizi. Kwanza, inasaidia kuhusisha fasihi simulizi na matini zake teule hivyo ikipandisha hadhi ya fasihi simulizi. Vilevile, Biblia

inaendeleza usanii wa fasihi simulizi hasa wasanii wa fasihi simulizi kupitia kwa maumbo yapatikanayo ndani yake. Vilevile, stadi za lugha zinakuzwa na kuimarishwa tukizingatia kwamba hatuwezi kushiriki katika usemi na matamko pasi na kutumia lugha. Aidha, ni wazi kwamba Biblia inaweza kutumiwa kama rejea ya fasihi simulizi hasa tunaposhughulikia maumbo ya fasihi simulizi. Hii itawawezesha watu wengi kusoma Biblia hasa wasomi katika viwango vyote vya elimu, hata wale wasio wa dini ya kikristo kwani watagundua kwamba mbali na kuwa kitabu cha kiroho, Biblia inao utajiri mwingi wa fasihi simulizi hasa kupitia kwa maumbo yake.

## 5.2 Mahitimisho

Utafiti huu ulibainisha kwamba maumbo ya fasihi simulizi yanapatikana katika Biblia, hasa katika vitabu vilivyoteuliwa. Aidha, kuna mwingiliano taaluma kati ya fasihi simulizi na matini teule za Biblia kupitia kwa maumbo ya fasihi simulizi ambayo ni dhahiri katika vitabu teule vilivyochanganuliwa. Vilevile, Biblia inachangia pakubwa katika ukuzaji wa fasihi simulizi. Hii itaifanya Biblia kutumika kama rejea ya fasihi simulizi.

## 5.3 Mapendekezo

Utafiti huu unapendekeza yafuatayo;

1. Biblia itumiwe kama rejea ya fasihi simulizi, hasa katika utambuzi wa maumbo ya fasihi simulizi.
2. Wasomi wa fasihi simulizi wahimizwe kutumia Biblia kama mojawapo wa vitabu vya fasihi simulizi hasa wanapochanganua maumbo ya fasihi simulizi.
3. Mwingiliano matini wa fasihi simulizi na taaluma nyingine uhimizwe. Hii itasaidia katika uhifadhi wa fasihi simulizi.

## 5.4 Mapendekezo kuhusu utafiti wa baadaye.

Utafiti huu unapendekeza utafiti wa baadaye ufanyiwe mambo yafuatato;

1. Maumbo ya fasihi simulizi katika vitabu vya Biblia ambavyo havijatafitiwa yafanyiwe utafiti;
2. Maumbo ya fasihi simulizi ambayo hayakudhihirika katika vitabu hivi yachunguzwe katika vitabu vingine, hasa ngonjera;

3. Mwingiliano matini wa fasihi simulizi na taaluma nyingine mbali na dini, ufanyiwe utafiti.

## MAREJELEO

Abrams, M. H. A.(1981). *Glossary of Literary Terms*. New York: Holt, Reinehart and Winston.

Allen, G. (2000). *Intertexuality*. London and New York: Routledge Psychology Press.

Alexlrod, R. & Cooper, C. (1988). *The St. Martin's guide to writing.* New York, St. Martin's Press

Bakhtin, M.M. (1986). *Speech Genres and other Late Essays*.Texas: University of Texas Press.

Balisidya, M.l. (1983). *Tanzu na fani za fasihi simulizi*, kutoka kwa mulika namba 19, Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili,; Journal of African Christian Thought, vol.4 chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Bediako, K. (2001). *Scripture as the hermeneutic of culture and tradition, no.1* Bible history.htt:www.biblehistory

Bodumbe, C. (1994). *The corruption of words. Matatu*: Zeitschrift fir Africanische Kutur und Gesellschaft.

Bray, G. (1996). *Biblical Interpretation; past & present.* Leicsster Apollos.

Cross, (1974). *Prose and poetry in the Mythic and Epic texts from Ugarit*. Harvard Theological Review.

Eagleton,T. (1983). *Literary Theory. Introduction.* Oxford:Basil Blackwell.

Escarpit, L. (1973). *The Book Hunger*. Paris.

Finnegan, R. (1970). *Oral literature in Africa:* Nairobi Oxford University press.

Finnegan, R. (2012). *Oral literature in Africa.* UK: Open book publishers CIC limited. http: //www.open book publishers.com.

Grimm, J (1812). *Children and Household Tales.* Kinder –und Hausmarchen.

Gunkell, (1862-1932). *educational teaching bible.* Retrived from http: //www.sbl – site.org/.*aspx*…11/5/14 at 10.00 am.

Harold L. & Charles, J.W. (1983). *A handbook of Christian Truth:* Fleming H. Ravell Company, U.S.A.

Helmer, R. (1949). *Oral & Written Transmission in the Old Testament.* Some Observations Studia, Theologica.

Ighile, M. O. (2013). *Challenges and prospects of teaching oral literature in Africa*. Academia Education Team. Retrived from http: //www.academia.edu//1159717. 11/5/2014.

Ipara I. na Waititu, F. (2004). *Ijaribu na Uikarabati*. Marudio ya K.C.S.E. Kiswahili; Oxford University Press, Nairobi.

Ingemark, C. (2005). *The Genre of Trolls. The case of Finland*. Swedish Folk Belief Tradition. Finland: Abo Akademi University Press. Http:www.abo.fi/stiftelsen/forlag/

Jamii ya Biblia ya Kenya na Tanzania (1997). *Biblia. Maandiko matakatifu ya Mungu*. The Bible Societies of Kenya & Tanzania. Nairobi & Dodoma.

Karama, S. (1968). *Utenzi wa Nabii Yusuf*. Mombasa: Haji Mohammed & sons.

Kimball, C. (2008). *Creation myths and sacred stories*; Oxford Reference online educational. Oxford University Press.

Peter K. J. (2012). *Mchango wa mbazi za Bibilia katika ukuzaji wa fasihi andishi ya Kiswahili*. Ku.ac.ke/cgi./opak detail. Thesis, Kenyatta Universit

Kombo, D.K. & Tromp, D.L.A. (2006). *Proposal and Thesis writing*: An introduction. Nairobi.Paulines publications.

Kristeva, J. (1969). *Desire in Language: Asemiotic approach to Literature and Art*. New York: Columbia University Press.

Lee, S. (1998). *The case for Christ.* Zondervan: Zondervan Publishing house.

Lemon, L.T. & Marion, J.R. (1965). *Russian Formalist Criticism*:Four Essays. Lincoln:University of Nebraska.

Leo, S. L. & Tonny, K. M. (2006). *Kurunzi ya Kiswahili. K.C.S.E. Kitabu cha Marudio*. Focus Publishers Ltd, Nair

Magesa L. (2011). *The hidden Face of Mwalimu Julius Nyerere*. TUKI. Dar es Salaam.

Materu, (1983). *Fasihi simulizi na uandishi wa Kiswahili katika fasihi*. Makala ya semina za kimataifa ya waandishi wa Kiswahili: Dar es Salaam. TUKI.

Materu, M.L.B. (1987). *Tanzu na Fani za fasihi simulizi katika mulika namba 19. Dar es Salaam:* TUKI, chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Matei, K. A. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi kwa shule za upili*. Kenya' Oxford University Press. E. Africa.

Menkeln, H.L.(1946). *Treatise on the gods*. New York: Alfred A. Knopf.

Meyer, M. (2005). *The Bedford Introduction to Literature*. Bedford/ Martins.

Miruka, F.A. (2013). *Maumbo ya fasihi simulizi katika mashairi andishi*. Pendekezo la utafiti.

Mlacha, S.A.K. (1985). *Kiswahili katika Kanda ya A Frika Mashariki.* Dar es Salaam.

Mlama, P. (1973). *The role of music in African Traditional Theatre*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

M'Ng'aruti, L. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Jomo Kenyatta Foundation; Nairobi.

Mrikaria, S. (2007). *Fasihi simulizi na technology mpya.* Swahili forum 14: 197 – 2006.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya hadithi fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam Printing Press.

Mulokozi, M.M. (1989). *Tanzu za Fasihi simulizi katika mulika 21* TUKI Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (1996).*Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili;* Dar es Salaam. TUKI

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili Dar es Salaam,* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mushengyezi, A. (2003). *Twentieth century Literary Theory*. LIT. 224: Literature. Kampala: Makerere University.

Musokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa fasihi*: Nairobi. East African Edu. Publishers.

Mtesigwa, P.S.K. (1989). *Methali ni nini?* Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Periodical Volume 56. Dar es Salaam.

Mvumbi, F.N. & Ngumbi, E.K. (2015). *Companion to Research Methodology*. CUEA Press. Nairobi

Nelson, T. (1995). *Nelson's New illustrated Bible Dictionary*, "Bible", R.F. Young blood, F.F. Bruce, R.K Harrison & Thomas Nebon Publishers, Inc. Nashville, T.N.

Ngure, A. (2003). *Fasihi simulizi kwa shule za sekondari*. Nairobi, Phoenic Publishers. Ltd.

Njogu, K. & Chimera R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. Momanyi, C. and Mathooko, M (wahariri) (2006). *Fasihi simulizi ya Kiswahili*: Nairobi. Twaweza Communication.

Njogu, K. & Wafula, R. (2007). *Nadharia za uhakiki wa Fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation:Nairobi.

Nkwera, F. V. (1978). *Fasihi Sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Note & Jordan (2011). *Ideology and Intertextuality : intertextual allusions in Judith 16*: Retrieved from http://dx.do.org/10.4102/hts. on 14/1/15.

Ntaragwi, M (2004). *The challenges of education and development in post colonial Kenya*. Africa Development.

Okpewho, I. (1979). *The Epic in Africa. Towards a poetics of the oral performance*. New York: Columbia University Press.

Patton, M.Q. (2002). *Qualitative Research & Evaluation Methods*. 3rd Ed. London: Sage Publications.

Peter, A. A. (2012). *Muziki wa Kizazi kipya kama utanzu wa fasihi simulizi ya Kiswahili*. Pendekezo la utafiti.

Plekanov, G.U (1957). *Art and social life*. Progress publishers. Moscow.

Robert, A. (1981). *The art of Biblical narrative*: historical introduction; Paulist Press.

Saussure, F. (1959). *Course in General Linguistics*. The philosophical Library, New York City.

Senkoro, F. E. M. K. (2011) *Fasihi Mfululizo wa Lugha na Fasihi*. KAUTTU: Dar es salaam.

Strobel, L. (1998). *The case for Christ:* Zondervan Publishing house.

Third Millenium Ministries. (2012). *Maisha ya Abrahamu: Muundo na maudhui*. Biblical Ed. for the world. Dar es Salaam.

Tokunboh, A. (General Editor). (2006). *Africa Bible Commentary,* World Alive Publishers, Nairobi.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi Oxford University Press.

Vatican. (1993). *Ufasiri wa Bibilia katika kanisa.* Retrieved from www.vaticom.val.../ic.con.c faith.doe 19930415.inte….12/5/2014 saa 8.30 mchana.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia:* Focus Publications Ltd. Nairobi.

Wamitila,K.W. (2006). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers Ltd:Nairobi.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Worthrop, F. (1957) *Anatomy Criticism*. Princeton University Press.

Zondervan Corporation. (1987). *The Family Devotional Study Bible*. The Bible League

## VIAMBATISHI

## ORODHA YA UCHUNZAJI

## MAUMBO YA FASIHI SIMULIZI

**1 – HADITHI/ SIMULIZI**

| KIPERA | SIFA BAINIFU | NDIYO | LA |
|---|---|---|---|
| Hurafa | Ngano zenye wahusika wanyama | | |
| Hekaya | Huhusisha mhusika ayari | | |
| Visakale | Matendo ya mashujaa | | |
| Visasili | Hueleza asili ya kitu | | |
| Mbazi | Hadithi za kimafumbo | | |

**2 - MAIGIZO**

| KIPERA | SIFA BAINIFU | NDIYO | LA |
|---|---|---|---|
| Miviga | Sherehe za kitamaduni | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Sanaa ya maonyesho | Mpangilio wa mazungumzo yanayojenga mgogoro | | |
| Mazungumzo | Upitishaji wa ujumbe | | |
| Mawaidha | Magungumzo maalum | | |

**3- USHAIRI SIMULIZI**

| **KIPERA** | | **NDIYO** | **LA** |
|---|---|---|---|
| Nyimbo | Tungo zenye mahadhi | | |
| Maghani | Hadithi za ushairi zinazosimulia sifa | | |

**4 – SEMI/ TANZU BAINIFU**

| **KIPERA** | | **NDIYO** | **LA** |
|---|---|---|---|
| Methali | Semi fupi fupi za kuelexa mafunzo mazito ya jamii. | | |
| Nahau | Kauli zilizoundwa kwa lugha ya kawaida na zenye maana iliyofichika | | |
| Vitendawili | Kauli fupi za kimafumbo | | |